ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
42.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
43.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
44.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
45.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.

46.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
47.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
48.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
49.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
50.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
51. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
52.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
57.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
58.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
59.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
60.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
61.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
62.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
63.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
64.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.

66.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
67.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
70.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
71.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
73.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.
76.Mhe. Zahra Ali Hamad	Nafasi za Wanawake.
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Tatu – Tarehe 23 Juni, 2009

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 36

Uimarishaji wa Polisi Jamii Zanzibar

Mhe. Amina Iddi Mabrouk – Aliuliza:-

Tunaipongeza serikali kwa kuanzisha Polisi Jamii katika shehia mbali mbali, Unguja na Pemba kwa lengo la kupunguza uhalifu na wizi wa mali za wananchi na kuimarisha hali ya usalama zaidi nchini.

(a) Je, Mhe. Waziri hii Polisi Jamii inaongozwa na shehia gani.
(b) Kwa kuwa suala hili limeanza kutekelezwa. Je, ni shehia ngapi za Unguja na Pemba zinafaidika na zoezi hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wajibu mkubwa wa Jeshi la Polisi Tanzania ni kulinda maisha ya watu na mali zao. Wajibu huu umeelezwa katika Sheria ya Jeshi la Polisi Sura Nam. 322. Katika nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania, idadi ya wananchi huwa kubwa sana kulinganisha na askari polisi na hivyo kufanya Jeshi la Polisi kushindwa kutoa huduma kikamilifu kwa wananchi. Kwa ajili hiyo, zimebuniwa mbinu mbadala kushirikisha wananchi katika ulinzi wa maisha na mali zao ambao huitwa Polisi Jamii au Ulinzi Shirikishi. Kwa upande wa hapa Tanzania dhana ya Polisi Jamii au Ulinzi Shirikishi imeanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2006 kufuatia mabadiliko makubwa ndani ya Jeshi la Polisi yanayoendelea.

Mhe. Spika, mabadiliko hayo yamejikita katika mihimili mitatu ambayo ni **USASA, UWELEDI NA POLISI JAMII.** Tangu kuanzishwa kwa Polisi Jamii hapa nchini hali ya uhalifu imedhibitiwa kwa sehemu kubwa chini ya

dhana hii. Polisi hujenga ubia na wananchi na kuwashirikisha kikamilifu katika ulinzi wa maisha na mali zao. Wananchi kutokana na kuwa na ubia wa Jeshi la Polisi huweza kuanzisha vikundi vidogo vidogo katika maeneo yao na kufanya ulinzi kwa kushirikiana na askari polisi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa jibu kama ifuatavyo:

Mhe. Spika,

(a) Hakuna sheria yoyote inayoongoza Polisi Jamii. Hata hivyo, taratibu zinaendelea kwanza kutunga sera yenyewe ya Polisi Jamii na baadae kutunga sheria hiyo.

(b) Shehia zilizofaidika na zoezi hili ni 28 kwa Unguja na 20 kwa Pemba.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba Polisi Jamii ipo hivi sasa na imeanza tangu mwaka 2006. Lakini kuna masikitiko kwamba hivi sasa watu wengi tayari wamepewa taaluma hii katika kusaidia huo ulinzi wa jamii. Lakini cha kusikitisha kwamba baadhi ya watu wakipeleka taarifa polisi wanatoa ile siri ili mtu akirudi huku mtaani anaadhibiwa. Je, kwa kufanya hivyo hii Polisi Jamii itaendelea.

Swali la pili Mhe. Waziri amekiri kwamba hivi sasa hakuna sheria inayosimamia suala hili. Je, mwananchi akipata matatizo katika kufanya kazi ya Polisi Jamii serikali itamlinda vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, katika visiwa kama vyetu ambavyo watu wanajuana na sio tu wanajuana lakini watu wamehusiana kidamu, tatizo alilozungumza huwa linachukua muda mrefu kuondoka. Kwa hivyo, ni vizuri tukaendelea na suala hili la Polisi Jamii mpaka hapo wananchi watakapojua umuhimu wa kutunza hizi siri. Maana yake wakati mwengine anayezungumzwa kuna mtu ni jamaa yake, sasa kama mtu jamaa yake lakini yumo ndani ya polisi ndipo hayo matatizo yanapotokezea. Hili ni tatizo na ndio maana tukasema kwamba polisi wanajaribu kusimamia sana nidhamu ya askari wao ili suala hili tuliweze.

Matatizo ambayo yanaweza yakamkuta mtu katika kufanya kazi hiyo. Mhe. Spika, Jeshi la Polisi linajitahidi lenyewe lifuatilie masuala ya ukamataji na operesheni yoyote inahitajika kutokea baada ya kupata hiyo taarifa. Mwananchi yeye mara nyingi hashirikishwi katika masuala ya operesheni, hii ni kwa sababu ya kumlinda asije akapata matatizo ya kuumizwa mwili wake. Kwa

hivyo, wanachotakiwa wananchi ni kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ambalo ndio litafanya hiyo kazi na sio yule mwananchi mwenyewe.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kweli na mimi nikiri kwamba askari polisi wanafanya kazi nzuri na wanasaidia sana kupunguza uhalifu. Lakini kwa sababu baadhi ya vijana wanafanya kazi hizi wana uwezo wa kuwa askari polisi kamili, wana elimu na *physical* wapo *fit*. Je, kwa nini serikali inapofanya uajiri wa Jeshi la Polisi haizingatii kuwachukua baadhi ya hawa vijana kuwaajiri, ili kuona kwamba wengine wanapata kuraghbika kujiunga na Jeshi la Polisi kwa tamaa kwamba wakifanya vizuri wanaweza kuajiriwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, nakubali kwamba baadhi ya vijana pamoja na kwamba hawajawa askari lakini wanayo talent ya uaskari. Sasa kama ikiwa zile sifa za kijana huyu zinakamilika kwa kuajiriwa katika Jeshi la Polisi, polisi huwa wanawachukua vijana hawa na kuwaajiri, hilo linafanyika.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Katika utaratibu huu wa kuanzisha Polisi Jamii katika maeneo je, Jeshi la Polisi ndio limeshindwa kabisa haliwezi kumudu kufanya kazi zake.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, Jeshi la Polisi halijashindwa kufanya kazi zake. Kinachotokea wanaolindwa ni wengi na maeneo ni makubwa na askari wanakuwa wachache sasa hapo ndio yanapotokea matatizo. Ndio maana tukaanzisha utaratibu huu wa Polisi Jamii ili angalau lile jambo linapotokea habari ipatikane ili Jeshi la Polisi lianze kufuatilia. Lakini halijashindwa, uchache wa askari ndio unaosababisha lazima tupate kushirikiana. Sio hapa Tanzania tu lakini hata nchi nyingi duniani wanafanya hivyo.

Nam. 101

Ajira kwa Walimu

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza:

Hivi karibuni tulisikia tangazo la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali la kuwataka wale vijana waliomaliza kusomea ualimu na wapo nje hawajaajiriwa kuwa wafike Wizara ya Elimu kwa maelekezo muhimu. Vijana hao ni wale elfu mbili ambao walikuwa nje zaidi ya miaka miwili wakisubiri ajira kutoka serikalini. Pia tulisikia kuwa kuna mazungumzo na wenzetu wa Tanzania Bara

kuwa kama wanazo nafasi za ajira watusaidie kwa wale vijana wanaotaka kufanya kazi huko.

(a) Je, Mhe. Waziri vijana hao wataajiriwa lini.

(b) Je, Mhe. Waziri mazungumzo na wenzetu wa Tanzania Bara yamefikia hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 101 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Wizara haijatoa tangazo la kuwaita vijana waliohitimu mafunzo ya Ualimu mwaka 2007 na 2008 ambao hadi hii leo hawajaajiriwa. Hata hivyo, ni kweli kwamba baadhi ya vijana waliohitimu mafunzo ya stashahada na shahada ya Ualimu mwaka huu, wameleta maombi ya kutaka ajira ya Ualimu.

Pia tuliwahi kuwadokeza wenzetu wa Tanzania Bara kuhusiana na wahitimu wetu ambao kwa wakati ule hatukuweza kuwaajiri.

Baada ya maelezo hayo napenda kujibu kama hivi ifuatavyo:-

(a) Tunatarajia kuwaajiri baadhi ya vijana waliohitimu mafunzo ya cheti cha ualimu mwaka 2007 na 2008, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010. Mazungumzo yamefanyika kati ya Idara ya Utumishi Serikalini, Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara yangu, ili kuwaajiri baadhi ya vijana hao kwa skuli zenye upungufu mkubwa wa walimu hasa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, na Mikoa miwili ya Pemba. Kwa wahitimu waliomaliza stashahada na shahada za Ualimu wataajiriwa wote.
(b) Hatujapokea ombi lolote la kutoka Tanzania Bara la kuwataka walimu wetu.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, kwa kuwa wahitimu wetu wanapomaliza vyuoni inabidi wakae muda mrefu kabla hawajaajiriwa. Wizara haioni kuwa wengine wanakwenda katika sehemu nyengine kutafuta kazi kwa sababu hapa hawajaajiriwa.

Lakini swali la pili hii kuajiri walimu inatafutwa nafasi baada ya watu kuhitimu au inatafutwa nafasi baada ya kujulikana ikifika kipindi fulani watu watahitimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya vijana ambao waliomaliza mafunzo ya ualimu huwa wanakwenda katika sehemu nyengine kutafuta ajira nah ii inatokana na kwamba inawezekana pengine wanakaa muda mrefu hawajaajiriwa. Lakini pia lengo na madhumuni ya kuwafundisha vijana wetu ni kupata ajira ama hapa ndani au sehemu nyengine yoyote ile ambapo wanaweza kupata ajira.

Mhe. Spika, jibu (b) ni kwamba nafasi ya ajira inategemeana na hali halisi na uwezo pamoja na mahitaji ya ajira kwa wakati ule. Mhe.Spika, tunaposomesha ni kwamba tunawajengea uwezo watu wetu kuweza ama kuyatumia mafunzo yale kujiendeleza ama kupata ajira. Kwa maana hiyo, kufundisha ni suala jengine na kuajiriwa ni suala jengine.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza niipongeze serikali kwa kuwa kilio chetu kuwa skuli zetu zina upungufu wa walimu Mhe. Waziri ametupa matumaini kwamba karibuni ataajiri wahitimu kwenda kujaza nafasi hizo. Lakini atakumbuka kuwa mapungufu tuliyonayo ya walimu katika maskuli yetu ni walimu wa fani maalum kama vile Hisabati, Kemia, Fizikia na Baiolojia. Je, hao wahitimu atakaotujazia katika skuli zetu kuziba hayo mapengo watakuwa kwenye fani hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kwamba tuna mapungufu makubwa ya walimu wa Sayansi ikiwemo Hisabati, Baiolojia na masomo mengine. Mhe. Spika, hao walimu ambao tunatarajia kuwaajiri wengi watakuwa ni walimu wa msingi na hasa katika sehemu zile ambazo zina upungufu.

Mhe. Spika, tunapozungumzia upungufu kuna upungufu wa aina mbili. Kuna upungufu ambao ni walimu hasa wa msingi lakini vile vile kuna upungufu wa walimu wa sekondari ambao ni hasa katika masomo haya ya Sayansi kama Hisabati. Lakini hata huku chini Mhe. Spika, bado tuna upungufu wa walimu kama vile Mkoa wa Kaskazini Unguja na Micheweni na Wilaya ya Mkoani. Hao ndio ambao tunafikiria hivi sasa kuwaajiri hasa kujaza ule upungufu uliopo kwa masomo haya ya kawaida. Tunajua kwamba bado upungufu wa masomo ya Sayansi upo na serikali inafanya jitihada ya kuweza kulipunguza tatizo hilo.

Nam. 18

Ukosefu wa Maji Wilaya ya Mjini

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:

Mradi mkubwa wa maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Awamu ya Kwanza ulielekezwa Wilaya ya Mjini, ili kuondoa tatizo kubwa la ukosefu wa maji katika wilaya hii. Kwa bahati mbaya, hadi hii leo bado kuna ukosefu wa maji katika maeneo mengi ya mji.

(a) Kwa kuwa mradi huu umekamilika na kuzinduliwa rasmi, lakini bado maji hayapatikani kinyume cha matarajio, Je, Mhe. Waziri ni tatizo gani linalosababisha maji yasipatikane.

(b) Mamlaka ya Maji inachukua hatua gani kuliondoa tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mradi wa maji katika Mkoa wa Mjini/Magharibi unajengwa kwa awamu mbili. Awamu ya mwanzo iliyokamilika na kufunguliwa rasmi katika mwezi wa Agosti 2008, ilipangwa ihudumie zaidi maeneo ya Wilaya ya Mjini. Hata hivyo, kutokana na muundo wa mtandao huo wa maji, pia ulitoa matawi yaliyounganishwa na mtandao wa maeneo ya Wilaya ya Magharibi na hivyo kusababisha maji kutolewa kwa mgao kwa maeneo ya mjini na maeneo ya magharibi. Hadi itakapokamilika awamu ya pili utaratibu wa mgao kwa kiasi fulani utapunguza upatikanaji wa maji kwa maeneo ya mjini. Aidha, panapotokea tatizo la kuharibika kwa pampu zaidi ya moja kama ilivyotokea katika mwezi wa Februari, 2009 upungufu wa maji hujitokeza kwa kasi zaidi na kuathiri maeneo mengi.

(b) Mhe. Spika, hatua za kupunguza tatizo la maji ni kukamilisha ujenzi wa awamu ya pili ambayo itasaidia maji katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi. Vile vile Mamlaka ya Maji inajitahidi kuwa na akiba ya pampu hasa zile zenye uwezo mkubwa ili panapotokea maharibiko kuweza kukabiliana nayo kwa haraka. Ili kupeleka maji katika maeneo ambayo hayapati, mamlaka inaandaa mradi mdogo na kununua vifaa vya kufanikisha kazi hizo kama ilivyofanya kwa baadhi ya maeneo

yakiwemo ya Mpendae, Magomeni, Kilimahewa na Mwembemakumbi ambapo kazi zinaendelea.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza naipongeza serikali kwa nia njema kabisa ya kuhakikisha kwamba tatizo la maji linaondoka katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi na nchi nzima kwa jumla. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri au mbaya wananchi wetu wengi wamepokea furaha hii ya kuondokana na tatizo la maji katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi lakini tatizo liliopo sasa hivi ni bei kubwa ya ulipaji wa maji kwa shilingi 4,000/=. Hicho ni kilio ambacho kila mwananchi wa nchi hii kama itafanywa sensa basi atatoa ishara kwamba ni nzito.

Je, Mhe. Waziri kwa kuwa tuna makampuni makubwa hapa nchini kama ya ujenzi, viwanda vya maji, mahoteli ya kitalii, vituo vya kuoshea magari, vituo vya kufyatulia matofali. Hivyo Mhe. Waziri haoni kwamba mwananchi akapunguziwa bei angalau shilingi 1,500/= ili hayo makampuni niliyoyataja yafidie katika kugharamia tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni hivi karibuni tumeanza utaratibu wa watu kuchangia maji na tulilipitisha hilo ndani ya Baraza hili. Mhe. Spika, gharama ya shilingi 4,000/= kwa mwezi kwa matumizi ya nyumbani kwa ghafla unaweza ukaiona ni nyingi na ni nyingi kwa umasikini, lakini hiki ni kiwango kidogo na huwezi kukipata popote Afrika nzima. Haya kwa wastani kwa kila siku katika nyumba ambayo mwananchi anapata maji analipia shilingi 133/= kwa siku, lakini fedha hizi zinakuwa nyingi kwa sababu mwezi huu hukulipa 4,000/=, mwezi ujao hukulipa 8,000/=, mwezi ujao hukulipa 12,000/=, inakwenda hatimaye mtu anafika anadaiwa 40,000/= kwa kudunduliza.

Lakini nataka niwathibitishie kwa kweli kiwango hiki ni cha chini kabisa ukilinganisha ukitilia maanani ili kuyapata maji haya kuna gharama kubwa. Kwa mfano, kwa wastani kila mwezi Mamlaka ya Maji inalipa kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya umeme ambao unatumika kupata hayo maji kwenye vituo vyetu hivi vya pampu.

Lakini wazo la kwamba tupunguze bei hii kwa matumizi ya nyumbani na tuongeze bei mahotelini, viwandani, wapiga matofali nini kitakachotokea, itakuwa sasa ni mzigo mwengine kwa mwananchi ambaye anahitajika kuwa na nyumba bora ambaye anahitaji matofali, bei ya matofali kule nayo itapanda. Kwa hivyo Mhe. Spika, bado bei hii ni ya chini kabisa.

Kwa mfano, ukenda misikitini, misikitini tumeweka kwa mwezi shilingi 3,000/=, watu wote wale wanaokwenda pale kwa kila siku kwa jumla yao wanalipa shilingi 100/= tu, niseme ni sawa sawa na senti ndogo tu kwa watu wale. Kwa hivyo, bado gharama hii ni nafuu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri alivyotangulia kusema kwamba kakubali kuwa hali ya wananchi wetu ya kipato ni ndogo sana. Kwa bahati mbaya katika ulipaji huu wa maji katika sehemu nyengine moja kwa moja kwa mara ya mwanzo kunakwenda risiti za malimbikizo ya miezi kadhaa ya nyuma. Kwa maana hiyo, lile deni kubwa alilolizungumza kuwa lina tabu limetokea bila ya wahusika kujitayarisha.

Je, Mhe. Waziri kwa haya madeni ya nyuma kwa nini wasingelisamehewa wakaanza kulipa pale walipoambiwa leo tunakuletea risiti hii ili ulipie maji.

Swali (b) kuna wengine nasikia tayari wameshakatiwa maji kwa sababu ya kushindwa kulipia maji hayo. Ni vigezo gani vilivyotumika hasa wakati sote tunakubali kuwa hali ya wananchi wetu ni masikini mpaka hawa watu wakakatiwa maji wakakosa huduma ambayo ni muhimu na ni ya lazima.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kama nilivyokuwa nikijibu swali la nyongeza la Mhe. Ali Suleiman Ali, tarehe ambazo watu walitakiwa waanze kulipa maji kwa kweli walijulishwa kupitia vyombo vyetu vya habari na wakawa wanajua. Nasema bahati mbaya kila mmoja akawa amepuuza. Lakini alipuuza kwenda kulipia kuchangia hayo maji shilingi 4,000/= na wakati huo huo maji anayatumia. Kwa hivyo, ile shilingi 4,000/= ikaongezeka mpaka hapo uamuzi wa kuanza kuchukua hatua za kwenda kukata maji ukajitokeza.

Kwa hivyo, bado wale ambao walikuwa na hili deni watalazimika kulipa kwa sababu maji hayo tayari wameshayatumia na hili wazo la watu wachangie maji tumelipitisha hapa Barazani tukalikubali sote ili kuwa na maji na huduma hii endelevu kwa watu wote.

Mhe. Spika, jibu (b) ni kwamba kigezo kilichotumika ni kile kile kwamba walipaswa walipe hawakulipa na yule ambaye alikuwa amelipa hakukatiwa maji. Kwa hivyo, naomba kutoa wito kwa wale ambao hawajalipia madeni yao basi waharakishe kwenda kulipia huduma hiyo.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, sijui kama

wizara inaelewa kwamba wito huu umeitikiwa vizuri lakini tatizo ambalo linajitokeza ni kituo kimoja cha kulipia maji. Kwa hivyo, mtu anakwenda zaidi ya siku tano pale hajafika kwenye eneo la kulipia matokeo yake siku ya saba maji yanakatwa. Sijui Mhe. Waziri kama analielewa tatizo hili na litaondoka lini.

Swali (b) Mhe. Waziri anaelewa kwamba kuna watu mpaka leo hawajapata risiti za kulipia maji na neno fedha si kitu cha kufanyia masihara, ni sawa sawa na kodi ile. Kama watu wetu wa *ZRB* na *TRA* watakaa tu wawasubiri watu waende wakalipe tunaweza tukawafungia biashara watu wote. Sasa hili nalo Mhe. Waziri analichukulia uzito gani na anawaambia nini wananchi kuhusu kuondoka kwa tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli sasa hivi tuna kituo kimoja tu ambacho wananchi wanakwenda kulipia huduma hii. Ni kweli kwamba ipo haja ya kuwa na kituo zaidi ya kimoja, lakini kwa sasa hivi ni mapema mno kuanzisha kituo chengine. Hata hivyo, msongamano huu wa watu kuwa wengi pale umetokana tu na kwamba hili zoezi la kukata kwa hiyo kila mmoja sasa hivi anakimbilia pale ili kuepuka asikatiwe. Nina imani kabisa baada ya mwezi mmoja ambao watu wengi watakuwa tayari wameshakwenda kulipa bili zao basi ule msongamano utapungua.

Mhe. Spika, jibu (b) kwa kweli sina taarifa kama kuna upungufu wa risiti na hivyo wale ambao wanakwenda kulipia maji huwa wanakosa risiti. Ni imani yangu kwamba risiti zipo, lakini kama risiti hakuna kama Mhe. Mwakilishi aliuliza basi nitahakikisha kwamba risiti zipo na mwenye kulipia anapewa risiti.

Nam. 65

Mgawanyo wa Madaraka

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Katiba ya Zanzibar 1984 Toleo la 2003 Ibara 5A imeeleza wazi juu ya dhana ya mgawanyo wa madaraka (*Separation of Powers*). Zanzibar tunafuata mfumo wa madaraka wa mamlaka tatu nayo ni Mamlaka ya Utendaji (*Executive*) Mamlaka ya Kutunga Sheria (*Legislature*) na Mamlaka ya Kutekeleza Utoaji Haki (*Judiciary*). Katika mamlaka hizo hakuna mamlaka itakayoingilia mamlaka nyingine isipokuwa kwa kufuata maelekezo ya Katiba.

(a) Je, Mhe. Waziri dhana hii inatekelezwa kwa kiasi gain ?

(b) Dhana ya vyombo hivi vitatu ni kuleta maendeleo katika nchi yenye Utawala Bora. Je, maendeleo hayo yamepatikana kiasi gani ?

(c) Je, Mhe. Waziri, kwa sasa huoni kuwa Serikali (*Executive*) ina nguvu zaidi ya Baraza ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 65, lakini kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi kwanza naungana naye katika kukubali kwamba katiba ya Zanzibar Toleo la 2003 Ibara ya 5A imeeleza wazi juu ya dhana ya mgawanyo wa madaraka (*Seperation of Power*).

Katiba ambayo imeweka mfumo kwa Zanzibar wa kuwa na mihimili mitatu katika kuendesha nchi. Kwa maana hiyo, kuna muhimili wa kiutendaji yaani (*Executive*), ambapo Kiongozi wake ni Mhe. Rais wa Zanzibar, kuna Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shuguli za Umma yaani (*Legislature*) Kiongozi wake ni Mhe. Spika na kuna Mamlaka ya Kutekeleza Utoaji Haki kwa maana ya Mahakama (*Judiciary)* Kiongozi wake ni Mhe. Jaji Mkuu.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 65 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, dhana hii inatekelezwa kwa kiasi kikubwa hapa Zanzibar na ushahidi uliopo miongoni mwao ni kuwepo kwa mamlaka hizo kihalali, hii ni kusema kwamba Zanzibar inayo Mamlaka ya Utendaji, inayo Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma (Baraza la Wawakilishi) na pia inayo Mamlaka ya kutekeleza utoaji haki.

   Aidha kila Mamlaka inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Kikao hiki hapa ni moja ya vielelezo tosha vya kuona moja ya Mamlaka inayofanya kazi zake vizuri. Vile vile kumekuwa hakuna maingiliano katika utendaji wa mamlaka moja na nyengine.

b) Mhe. Spika, kumekuwa na maendeleo makubwa katika dhana ya kuwa na Mihimili hii mitatu. Miongoni mwao ni kule kuweza kusimamia shughuli za serikali, ambapo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaweza kufuatilia maendeleo yanayotekelezwa na serikali. Pia kumekuwepo na mabadiliko makubwa katika kutafuta haki.

Hivi sasa wananchi wetu wa Zanzibar wanajua kutumia Mahakama ipasavyo. Aidha kumekuwa na suala zima la kuzitumia rasilimali za taifa katika maeneo ya kimaendeleo kwa nia ya kuwa na maendeleo endelevu, haya yanafanywa na serikali.

c) Mhe. Spika, Serikali haina nguvu kuliko Baraza na wala Baraza halina nguvu kuliko Serikali, isipokuwa kila Mamlaka inafanya kazi kwa mujibu wa Katiba na Sheria husika.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini haoni kitu kimoja kinakosekana hapa kwetu kwenye hii mihimili mitatu, yaani ile *check and balance* haipo. Je, hili si tatizo ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, nadhani *check and balance* ipo na ndio maana Baraza hili linaipima serikali utendaji pamoja na utekelezaji wake *(Makofi)*.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba anisaidie ufafanuzi. Kwa kuwa kwenye Mamlaka tatu, mbili zinafanyakazi moja kwa mfano *Executive* Wajumbe wake wamo kwenye Baraza la Wawakilishi ambao ni Mawaziri na *Legislature* tumo humu tunachanganyika nao. Hivyo, haoni kwa siku za mbele ipo haja kwa Mawaziri wa Serikali wasitokane na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, analolizungumza ni suala la Kikatiba, kama utafika wakati wa kufanya marekebisho ya Katiba, basi tatizo halitakuwepo *(Makofi)*.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Waziri kwa kuwa wizara yako ndiyo inayosimamia suala zima la Usimamizi wa Katiba, Sheria pamoja na Utawala bora.

(a) Mfumo huu tunaoutumia wa *Western Ministers* ambao hutumika sana kwa nchi za *Commonwealth*, haukidhi matakwa ya Katiba juu ya dhana nzima ya *separation of power*.

(b) Kuendelea na mfumo huu ambao umeshaanza kuleta matatizo kati ya mihimili hii, pengine unaweza kusababisha matatizo zaidi siku za baadaye.

(c) Je, wizara yako inashauri nini juu ya kuondosha tatizo hili ambalo linaashiria ukiukwaji wa Katiba ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Mjumbe hakueleza hasa matatizo gani yanayotokea kwenye mfumo huu. Lakini kuhusu suala la *Western Ministers* na tunajua siku zote tunapoanza kitu basi ni vyema kuanza na kile tunachokifahamu.

Kwa sababu sisi tulitawaliwa na Waingereza na tulijifunza mfumo wa Kiingereza, kwa hivyo tulipoanza shughuli hizi tulianza na mfumo wa Kiingereza. Ninadhani tutakapokua pamoja na kupea tunaweza kusema kwamba sasa tubadilike.

Lakini sijayafahamu matatizo, labda hayo ataandika swali jengine kamili kwa ajili ya kueleza matatizo ambayo anayoyaona hivi sasa. Kwa hivyo, wizara yangu haiwezi kutoa ushauri wowote bila ya kujua yale matatizo ambayo Mhe. Mjumbe anayo na wala hakuyataja, isipokuwa amesema tu kwamba yameleta matatizo na hakuyachambua.

Nam. 39

Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Afya na Nyumba za Madaktari

Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Aliuliza:-

Naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kujenga Vituo vya Afya na Nyumba za kileo za Madaktari katika maeneo mbali mbali, Unguja na Pemba kupitia msaada wa TShs. 3 Bilioni wa *ADB,* ili kupunguza matatizo yaliyokuwepo kabla ya hapo.

(a) Je, Mhe. Waziri ni nyumba ngapi na vituo vya afya vingapi vimejengwa chini ya mradi huu ?

(b) Je, ni maeneo yepi yaliyobahatika kujengwa nyumba na vituo hivyo kwa upande wa Unguja na Pemba ?

(c) Serikali imejipanga vipi kuendeleza mradi huo baada ya mradi huo kumalizika ?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa niaba ya serikali tunazipokea pongezi za Mhe. Mwakilishi kwa moyo mkunjufu. Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inaendelea kujenga Vituo vya Afya katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba kupitia mkopo wa Tshs. 3 Billioni kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*).

(a) Mhe. Spika, mradi huu utajenga nyumba 20 Unguja na 20 Pemba. Aidha, vituo vya Afya 4 vitajengwa upya na vyengine 2 vitafanyiwa matengenezo makubwa.

(b) Maeneo yaliyobahatika kujengwa nyumba za wafanyakazi ni haya yafuatayo:-

Kwa Upande Unguja:

1. Bambi
2. Kiboje
3. Ndijani kwa Baniani
4. Uzi
5. Uzini
6. Bumbwini
7. Donge
8. Kombeni
9. Matemwe
10. Mahonda
11. Kidoti
12. Kibuteni
13. Ukongoroni
14. Mfenesini
15. Bwejuu
16. Kitogani
17. Kizimbani
18. Tumbatu Jongowe
19. Nungwi

Kwa Upande Pemba:

1. Bogoa
2. Fundo
3. Junguni
4. Kangagani
5. Kengeja
6. Kiuyu Mbuyuni
7. Kiuyu Kipangani
8. Kisiwa Panza

9. Konde
10. Mgelema
11. Ziwani
12. Makoongwe
13. Makongeni Mtambwe
14. Mtangani
15. Pujini
16. Shamiani Muambe
17. Tundauwa
18. Ukunjwi
19. Wambaa
20. Wingwi

Vituo vitavyojengwa upya kwa upande wa Unguja ni Mahona na Pemba ni Kengeja, Konde na Kojani.

Vituo vitavyofanyiwa matengenezo kwa upande wa Unguja ni Chwaka na Matemwe.

(c) Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imekusudia kuendeleza mradi huo kwa awamu ya tatu baada ya kumalizika wamu hii.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naomba nichukue fursa hii kwa kumpa pongezi Mhe. Waziri kwa kujenga majengo haya.

(a) Swali langu lipo hapa, kwamba nani hasa wanakusudiwa kukaa kwenye majengo haya vituoni.

(b) Je, wizara imeshatayarisha Hati Miliki ya majengo haya, ili siku moja asijekupewa asiyehusika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, waokusudiwa kukaa kwenye nyumba hizi ni madaktari wetu, yaani Clinical Officers watakaa, Wakukaa pamoja na wengine ambao wanahitajika kwa ajili ya kutuo huduma muhimu kwenye kituo.

Kuhusu suala la Hati Miliki tunamhakikishia Mhe. Mwakilishi kwa kuwa hilo ni jambo la mwanzo kwa sababu hawa wahisani au washirika wa maendeleo, kitu cha mwanzo wanachokihitaji ni Hati Miliki. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi kwamba nyumba zote zimepatiwa Hati Miliki kwanza na baadaye ndio zikajengwa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri ametaja majengo mengi yaliyokwisha kujengwa kwa ajili ya makaazi ya madaktari. Lakini napenda kumuuliza Mhe. Waziri. Je, hivi vituo vilivyobakia kwa mfano Kangani na kwengineko tutegemee lini kujengwa majengo haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, vituo vilivyobakia tutavijenga kwa mradi utakaokuja. Kwa sababu kama nilivyosema kwamba mradi huu unamalizika mwaka 2010 na tutaangalia huko usoni Mwenyezi Mungu akitujaalia tutakapoendelea nao, naamini hilo tutaliangalia kwa jicho maalum, ili kupunguza matatizo kwenye vituo vyetu.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa madaktari wengi baada ya saa za kazi huwa wanakwenda kwenye vituo binafasi kwa lengo la kuongeza kipato, na nyumba zilizopo ziko vijijini.

Kwa kweli kuna mifano mingi kwa muda mrefu nyumba za madaktari zilikuwepo, lakini madaktari hawapendi kuhamia huko. Je, kwa sasa wizara yake imepanga mikakati gani ya kuhakikisha nyumba zilizojengwa madaktari wanazikaa, ili kupunguza tatizo la daktari hasa nyakati za usiku *(Makofi)*.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, tutahakikisha kwamba nyumba hizi wanakaa madaktari wanakaa na hasa kusudio letu kwa kuwa huo wakati wa usiku ndio wawepo kwenye hizo nyumba. Kwa sababu kuna huduma za mchana, lakini kuna matatizo yanayotokea usiku, hilo ndilo kubwa na nia hasa kwani mchana mtu anaweza kwenda sehemu yoyote kwa ajili ya kupata huduma, lakini tatizo linakuja usiku.

Kwa mfano, mama anataka kujifungua, mtu pengine amegongwa na nyoka au amepata jaraha wakati wa usiku. Kwa hivyo, tumepanga makusudi nyumba hizi madaktari wawepo karibu na wananchi kwa wakati wote kwa lengo la kutoa huduma kwa wananchi wale.

Kwa hivyo, nia na madhumuni yetu ndiyo hiyo. Kwa upande wetu sisi wizara tutafanya kila jitihada kuona hawa wanaopangiwa kukaa kwenye hizi nyumba wanakaa, yaani tutafuatilia kwa hatua zote.

Nam. 17

Walinzi Binafsi Kupatiwa Silaha

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Katika nchi yetu ya Zanzibar, zipo Kampuni Binafsi za Ulinzi, zinazolinda sehemu mbali mbali, kama mahoteli, maduka, na ofisi. Lakini kazi hizo huzifanya kwa kutumia mapanga na marungu.

Kwa kuwa walinzi hawa ni Raia wa Tanzania, na wengi wao wamepitia sehemu ya uaskari. Je, Mhe. Waziri huoni kuwa kuna haja ya walinzi hawa, wakapatiwa silaha za uhakika zaidi kama magobore, ili kukabiliana na matokeo yoyote ya uhalifu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 kama ifuatavyo:-

Ni kweli katika nchi yetu ya Zanzibar zipo Kampuni Binafsi za Ulinzi zinazolinda sehemu mbali mbali kama mahoteli, maduka na taasisi nyenginezo.

Kampuni hizi zinasajiliwa kwa Sheria ya Makampuni ya mwaka 1953 ya Sheria za Zanzibar. Lakini kupatiwa silaha za uhakika kwa kampuni hizo kunaweza kukaleta hatari zaidi katika nchi yetu. Hivyo wizara yangu italichukulia suala hili na kulifanyia utafiti zaidi kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama vilioko katika nchi yetu, ili kuweza kufikia mwafaka kwa lengo la kudumisha amani na utulivu wa nchi yetu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.
Hivi sasa katika nchi yetu tumeshuhudia walinzi wa sehemu zetu za vikosi wakipatwa na janga ambalo hatukulitarajia na wenzetu hawa walikuwa na silaha za kisasa kwa ajili ya kujihami kwa lolote litakalotokea. Lakini kwa kuwa walinzi wetu wanalinda sehemu mbali mbali tena ni za hatari, kwa mfano kuna fedha, wageni pamoja na mambo mengine hasa kwenye mahoteli.

Kwa kweli silaha zao wanazoendelea kutumia ni kama nilizozitaja za marungu na mapanga. Je, kwa kuwa serikali yetu ina utaratibu mzuri ambao Mhe. Waziri amesema atalichukua suala hili kwa ajili ya kulishughulikia kwa haraka.

Lakini kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanazo Kampuni Binafsi za Ulinzi na silaha hizi za magobole, kwa ajili ya kujihami kwa lolote ambalo litakalotokezea kuhusiana na uhalifu.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Waziri huwezi kuchukua kigezo hicho cha mara moja cha kufuatilia wenzetu wa Tanzania Bara wamefanya vipi, ili kupata manusura ya silaha zile kwa wale wanaokabidhiwa pamoja na usalama wetu, ili wasiende kinyume na taratibu walizokalia kwenye ulinzi huo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Spika, ukweli ni kwamba Kampuni Binafsi za Ulinzi, bado silaha ambazo watapewa ni hizi ambazo wanazoendelea nazo na huku tunaendelea na utafiti zaidi na *special* kwa Kampuni Binafsi za Ulinzi ambazo zimesajiliwa chini ya CAP 1 53 ya mwaka 1953. Kwa zile taasisi nyengine ambazo tunahisi ni taasisi nyeti basi ulinzi wao unakuwa sio wa marungu wala bakora, isipokuwa ni kwa silaha.

Nam. 14

Utolewaji wa Mafunzo kwa Madaktari wa Mifugo Vijijini

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza:-

Hivi karibuni Wizara ya Kilimo ilifanya mafunzo maalum ya muda wa miezi miwili kwa Madaktari wa Mifugo wa Vijijini katika Shehia tisini, ili kuwapunguzia wafugaji matatizo ya kufuata wataalamu hao Mjini. Mafunzo hayo yalisaidiwa na *IFAD*.

(a) Je, Mhe. Waziri mafunzo hayo yalilenga eneo lipi.

(b) Je, ni Shehia ngapi Unguja na Pemba wamepata mafunzo hayo ?

(c) Je, mafunzo hayo yamo kwenye mradi gain ?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mafunzo ya watoa huduma za mifugo vijijini *Community Animal Health Workers (CAHW's),* yalilenga katika kutoa huduma za mwanzo katika maeneo ya uthibiti, uchunguzi na utibabu wa magonjwa ya mifugo.

Aidha, wahudumu hao walipatiwa taaluma ya lishe na ulishaji bora wa mifugo, uwekaji wa kumbukumbu za uzalishaji, matibabu, uzazi na vifo pamoja na utunzaji wa taarifa muhimu mashambani. Vile vile taaluma ya elimu kwa wafugaji ilitolewa, ili kuwashajiisha wafugaji wetu wafuge kibiashara badala ya mazoea.

b) Jumla ya Shehia 50 za Unguja na 40 za Pemba zilifaidika na mpango huu, ambao ulijumuisha Wilaya 5 ukitoa Wilaya ya Mjini Unguja na Wilaya 4 za Pemba. Kila Shehia ilitoa mtu mmoja na kufanya idadi ya wahudumu wote waliopewa mafunzo hayo kuwa 90.

c) Mafunzo hayo yamo kwenye Mradi unaojulikana kwa jina la Mpango wa Kuimarisha na Kuendeleza Sekta za Kilimo na Mifugo (*ASSP/ASDP- L*).

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Mafunzo mengi yanayotolewa na Wizara ya Kilimo wale wanaopelekwa au wanafunzi wa mafunzo hayo mara nyingi huwa masheha. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri afahamu kwamba sheha hana muda huo wa kwenda kuwafundisha wenziwe au kutubi wanyama kama ilivyokusudiwa au lengo la mafunzo hayo.

(b) Madaktari au Mabwana Shamba wanaowekwa kwenye vituo uwezo wao umeshakuwa mdogo na kweli hawawezi kutoa mchango mzuri. Kwa hivyo, ni vyema hawa kawapatiwa mafunzo angalau ya cheti kwa ajili ya kutoa msaada unaostahiki.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza suala hili sitaki nikubaliane naye kwamba mafunzo tuliyotoa tumewapa masheha, kama masheha walishiriki basi walikuwa ni wasikilizaji tu na kuhakikisha kwamba yule mtu ambaye ameteuliwa kwenye shehia yake naye amehudhuria kwenye yale mafunzo, yaani ni kama ushahidi na wala sio kama tulikuwa tukiwapa mafunzo masheha.

Swali lake la pili kwamba Mabwana Shamba ambao wako kwenye vituo vyetu wanaonekana hawa taaluma ya kutosha. Kwa hivyo, lengo kubwa la serikali la kuanzisha Chuo cha Kilimo kilichopo Kizimbani ambacho hivi sasa tunao wanafunzi wengi. Moja ni kuwapeleka kwenye eneo hili na hivi sasa wanasoma katika ngazi ya cheti pale Kizimbani.

Kwa maana hiyo, kila baada ya miaka miwili wanapomaliza mafunzo tutakuwa tunaendelea kuwagawa kwenye vituo vyetu hivi, kwa ajili ya kuwapatia huduma wananchi wetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kumuwezesha mfanyakazi haitoshi kuzingatia kiwango cha elimu tu, lakini pamoja na nyenzo.

Hivi karibuni nilibahatika kupatiwa mafunzo na mtaalamu mmoja wa kilimo ambaye kwa kweli fani yake ni *degree* moja. Lakini kwa kuwa mfanyakazi huyo alifika kwangu kutoka Ole kwa baskeli, hivi wakulima wangapi watafaidika na elimu ile ?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ufupi ni kwamba tumekuwa tukisema tunapoulizwa swali hili la Mabwana na Mabibi Shamba kuhusu vipando, jibu letu linakuwa azma ya wizara na serikali kwa jumla ni kuwapatia kila mmoja vipando vya uhakika.

Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kupitia Baraza lako hili tukufu kwamba mpango huu unaendelea na kesho tukijaaliwa tutatoa vipando vingi sana kwa Mabwana na Mabibi Shamba *(Makofi)*.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Wilaya ya Micheweni Jimbo langu linaongoza kwa ufugaji wa mifugo tofauti kama vile ng'ombe, mbuzi na wengineo. Je, miongoni mwa shehia 6 zilizomo ndani ya Wilaya ya Micheweni ni watu wangapi waliopata kushiriki mafunzo ?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nafikiri jibu lake ni lile ambalo amelizungumza mwenyewe ni kwamba katika 6 sita ni watu wangapi ambao wamepata mafunzo hayo. Jibu ni watu 6 kutoka shehia sita. Kwa sababu kama nilivyojibu mwanzo kila shehia za Unguja na Pemba zimepata nafasi moja kwa ajili ya mafunzo hayo ambayo yalichukuwa muda wa miezi mitatu.

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi asubuhi ya leo kunipa nafisi ya kutoa mchango wangu kuhusiana na Bajeti ya Serikali ambayo imewasilisha mbele yetu. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, pia nikushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii. Lakini nitoe pongezi kwa Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake. Vile vile niunge mkono kwa asilimia mia kwa mia maelezo ambayo Waziri Kivuli ameyatoa hapa na katika hili ningemuomba sana Mhe. Waziri aifanye ni *working document* kwa sababu haikuacha kitu na mapungufu kama yapo, basi ni madogo ya kibinaadam, lakini kwa mujibu wa haja na hoja basi inakidhi kuwa ni jambo la kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nataka nije kwenye suala zima la ongezeko la mshahara, kwanza nachukua nafasi hii kushukuru kwa sababu naambiwa hata kama ni kidogo ushukuru sasa nashukuru kwamba kima cha chini cha mshahara kimefikia laki moja kwa upande wa serikali ya SMZ na hii ilikuwa ni ilani ya Chama cha Wananchi CUF mwaka 2005, kwa hivyo kama ingelikuwa ni serikali yetu sisi sasa hivi ingelikuwa ni laki tatu, lakini si viabaya na wao wameanza kusogea. Lakini pamoja na pongezi hizo bado kima ni kidogo mno napenda nifuate maneno ya mama yangu Mhe. Mkongwe Nassor Juma yeye alisema hataki kufanya jambo lolote kubwa, lakini akatwambia sote tuna akili zetu, sasa kwa sababu tuna akili zetu tunafahamu kwamba bado hiki kima ni kidogo mno hata kama tumeongeza.

Sasa ombi langu mimi ni kwamba ule utaratibu ambao Mhe. Waziri ametuambia hapa kwamba watakwenda kwa mwendo mdundo watoe elfu kumi kwanza, halafu waje watoe tena baadae. Mimi ningeomba hii laki moja ianze moja kwa moja kuanzia mwaka huu mpya wa fedha angalau inaweza kuleta faraja kidogo na nyongeza nyengine zikafuata baadae.

Mhe. Spika, nilikuwa nikitizama taarifa ya habari siku ambayo Mhe. Waziri aliwasilisha bajeti hii, basi hata yule msomaji wa Channel Ten aliposema kwamba kima cha chini kimeongezwa ni laki moja basi alikuwa anasoma huku anacheka, TV za bara wao wana utaratibu wao na mishahara yao ni mikubwa, lakini inaonyesha jinsi gani hiki kima kilivyokuwa kidogo, yeye alifanya kama kichekesho lakini mimi nasema sio kichekesho na tumepiga hatua ila bado hakijatosha tufikirie kwamba kuna haja ya kuongeza tukenda mbele zaidi.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye suala zima la changamoto zinazokabili maendeleo ya Zanzibar ambayo katika page ya kumi na tisa hapa Mhe. Waziri ametueleza changamoto ambazo zinatukabili, mimi nimezipanga hapa kama alivyosoma miongoni mwa changamoto hizo ni kasi ya ongezeko kubwa la watu, uzalishaji mdogo na kiwango kidogo cha usafirishaji wa bidhaa nchi za nje. Mhe. Spika, kwa nia njema kabisa na suala zima la kujenga mimi sitaki nitofautiene na Waziri moja kwa moja, lakini nasema bado hajagusa hasa changamoto inayoikabili Zanzibar katika masuala mazima ya kufikia maendeleo au kuwa na uchumi unaoimarika.

Mhe. Spika, ukizungumzia suala la kazi ya uongezekaji wa watu basi jibu lake ni rahisi na wenzangu wameshazungumza hapa, tunafanya uzazi wa mpangilio na wengine hawazai tena kutokana na matatizo mbali mbali kwa hivyo lile ongezeko halitokani na kuzaa, lakini ongezeko linatokana na uingiaji wa watu uliokuwa hauna kidhibiti na bahati mbaya sana siku mbili tu zilizopita kumeshasherehekewa wakimbizi na wameshapewa uraia wa Tanzania kwa maana hiyo tusubiri boti zije, anayetoka Rwanda na anayetoka Burundi atakuwepo hapa na sisi hatuna udhibiti huo. Sasa hapa jibu la rahisi kuhusiana na changamoto hii ni kurejesha passport ajulikane nani anaingia nani anatoka, anayeingia anaingia kwa madhumuni gani hivi ndivyo ulimwengu unavyokwenda kwa hivyo hiyo mimi sioni kama changamoto ya tishio, ni changamoto ambayo tunatakiwa kuwa wajasiri wenyewe tukaamua na kudhamiria basi itakaa sawa.

Mhe. Spika, ukija katika suala la uzalishaji mdogo mimi nadhani vile vile haidhuru hapa patahitaji fedha nyingi lakini ni tatizo ambalo tunaweza kujikwamua nalo kwa kupata vifaa vya kisasa, wataalam wa kutosha na nyenzo tukaweza kufanya mambo yetu kama wengine wanavyofanya.

Ama kwa upande wa kiwango kidogo cha usafirishaji bidhaa nchi za nje hili pamoja na kuhitaji wataalam katika sekta nyengine, lakini ni suala zima la kuwa wabunifu tukaweza kuboresha bidhaa zetu, nilisema nitoe mfano kwa huu mkoba wangu ambao ni mkoba wa ukili lakini, nimekuja nao barazani na naweza kwenda nao shughulini na matembezi, kwa sababu umeboreshwa kiwango chake kwa hivyo tatizo ni hili tu huu huu unaweza kusafirishwa ukenda zake Marekani, pamoja na kwamba ile mikoba yetu ya ukili ya kawaida tunakwenda nayo sokoni nayo ni kivutio na kitu ambacho kiutalii kina hadhi yake. Lakini huu natoa ni mfano tu kwamba changamoto hizi bado ni nyepesi mno na tunaweza kuzikabili tukiamua wala halitokuwa tatizo ambalo tutaambiwa uchumi wetu una matatizo kutokana na changamoto hizi.

Mhe. Spika, changamoto ambayo naiona mimi sasa hivi ndio tatizo katika kukabiliana na maendeleo ya nchi yetu kiuchumi na mambo mengine yote ya

maendeleo ni suala la muungano wetu ambalo sasa hivi umedumu kwa miaka arubaini na tano, yameshasemwa mengi katika hili na sijui kama bado tumeshikwa na hofu, tunakuwa waoga au tumeshikwa na kitu gani. Lakini bila ya kukaa tukaamua muungano ambao utakuwa hauna manung'uniko kwa pande zote mbili Zanzibar haiwezi kujikwamua kiuchumi abadan, mifano hata kama tutaandaa kitu kwa mfano tunataka kufanya jambo kubwa katika nchi midam litakuwa linahitaji kupata msaada sisi kutoka nje tayari Muungano ndio kikwazo chetu. Lakini hata ukienda katika masuala ya fedha kuna BOT hii imekuwa ni jinamizi kuanzishwa kwa BOT kuna *asset* za Zanzibar na tuna shea zetu, nini tunapata hatukioni asilimia 4.5% imetokea wapi pia haipatikani Mhe. Waziri kasema kwa mara ya kwanza ndio mwaka huu tumepewa hivi kweli miaka 45 tunafikiriwa leo kwa kupiga kelele nyingi na tutaendelea kupiga kelele kadiri Mwenyezi Mungu atatujaalia kuwemo ndani ya chombo hiki.

Lakini Zanzibar ili ikomboke huu muungano ni kikwazo kwetu na sisemi hili kwa sababu hatutaki muungano laa hasha muungano tunautaka, lakini uwe muungano usiokuwa na manung'uniko sio wa kukamuana tu au kutozana nguvu imefika pahala imekuwa kama lazima vile.

Mhe. Spika, jana Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Mazingira alipokuwa akijibu suala hapa kuhusiana na habari ya bahari kuu na meli la uvuvi lile lililokamatwa, katwambia sheria namba tatu ya mwaka 1989 kuhusu bahari kuu kwamba hiyo ndio iliyofanya sheria lile jambo kuwa la muungano, tuchukulie hivyo hivyo sawa. Kiutaratibu lazima jambo likishapitishwa kule lije kwenye chombo hichi sasa mimi nauliza tuambiwe ni kikao kipi na mwaka gani kilichoridhia suala hili, hiyo sheria iliyochukua masuala ya bahari kuu kuwa ni masuala ya kimuungano na kama haikufanyika hivyo ina maana hii sheria ni batili, sasa kwa nini tunaitekeleza. Kama haikuridhiwa maana yake tuendelee kilichokuwa chetu ni chetu hatukukiridhia sasa hiyo sheria inakuwa sio halali, sasa haya ndio masuala ambayo nasema ndio changamoto za kuziangalia kwa sababu kikwazo cha sisi kwenda mbele ni suala la muungano. Kika unapokwenda unaambiwa kuna mwamvuli na mwamvuli wenyewe sijui unapigwa na upepo kwa sababu naona tunaoana tu hautufuniki wala hautusaidii.

Mimi bado Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri kwamba changamoto yetu haya yote yana majibu yake rahisi tu, tunaweza kukaa pamoja tukayamaliza, lakini tatizo letu ni kwamba hatwendi pahala sababu ni muungano, OIC sitaki kuielezea kila mtu anafahamu kilichokwaza ni Muungano na wenzetu wamesema watafanya hili na lile lakini hawajafanya chochote kwa sababu wao hawana shida, wana mambo yao wanafanikiwa yanakwenda hawashughuliki.

Mhe. Spika, sasa nataka nizungumzie hii bajeti yetu kwa ujumla kama ilivyoelezwa hapa kwamba wataalam wa uchumi walivyoipitia walitwambia kwamba inaonekana bajeti ya Zanzibar ni nzuri kule ile ya wenzetu, uzuri wake ni kwamba asilimia hamsini nzima au zaidi ya hamsini ndio imelenga kwenye maendeleo jambo ambalo ni zuri. Lakini sasa tatizo la kuthibitisha hilo ni takwimu bajeti yetu imekuwa na upungufu sana wa takwimu kwa hivyo inashinda kufikia kuthibitisha hiyo hali, aidha kama ingekuwa takwimu zipo, basi ni jambo la kujivunia kwamba Baraza la Wawakilishi linajadili bajeti ambayo ina ubora zaidi kuliko ile ya bara pamoja na wataalam wengi na maprofesa waliokuwa nao.

Lakini pia nilikuwa na wasi wasi katika hiyo bajeti kwamba isije ikawa upande huu wa maendeleo tunategemea sana wahisani, kwasababu kutokana mchango ambao umeonekana hapa katika page ya 28 kati ya fedha hizo shilingi milioni 18,522. sawa na 9.6% ndio ambayo inatolewa na serikali miongoni mwa zile fedha ambazo zimetakiwa kuwa za maendeleo na 90.4% itakuwa inatoka kwa wahisani. Sasa hapa kidogo pamenipa mashaka na mashaka yangu ni kwa sababu kama tunavyoelewa sasa hivi kuna hili suala la mtikisiko wa kiuchumi duniani pengine mimi nikijichukulia mfano kama amenijia Mhe. Haji akawa na mambo yake akataka nimsaidia na nikamwambia nitakusaidia laki mbili kwa mfano, lakini nikatokezewa na matatizo nikashindwa kumpa hata robo ya ile laki mbili.

Sasa wasi wasi wangu uko hapa kwamba kutokana na msuko suko wa kiuchumi duniani je hii 90% tunayoisubiri kwa wafadhili tunaweza kuipata, kama hatuwezi kuipata na mimi nina suala la kujua *rescue plan* yetu iko je, wenzetu tumeona wamejilabu sijui kama wanazo mkononi au ni maneno matupu, lakini wameshasema kwamba wana 1.7 trion kwa ajili ya kufanyia hayo mambo. Je kwa upande wetu sisi tuna kiasi gani au kuna mpango gani ulioandaliwa kuhami mambo kama haya yanapotokezea.

Mhe. Spika, nikiendelea mchango wangu nakuja kwenye suala la vipaumbele vya serikali katika ukurasa wa 53 vinajionyesha, kuna mambo yanayohusiana na utalii miundo mbinu, viwanja vya ndege, barabara, chuo cha Utalii, Nishati, Maji sasa hapa mimi Mhe. Spika, nimekuwa sijaelewa kidogo kwa sababu naona tunaweza kuwa na vipaumbele vingi. Mimi nadhani kama tumepanga kuwa na mambo sita vipaumbele sana sana vitakuwa ni viwili sasa hii kuwa na vipaumbele vingi kama hivi naona itakuwa ni matatizo hata kimoja kuwa kitatimia, kwa sababu tutataka vyote tuvikamilishe, lakini itashindikana lakini kila kimoja utakigusa gusa tu. Kwa hivyo, mimi ningeshauri hapa tuone kwamba kuna haja ya kuwa na kipaumbele kimoja au viwili ambavyo mwakani Mhe.Waziri akija tena Mwenyezi Mungu atufikishe sote atupe hadithi iliyokamilika, isije ikawa vipaumbele hivi na mwakani vikawapo tena kwa

sababu havijakamilika. Sasa hilo nilikuwa napenda tulione katika suala zima la kupanga vipaumbele kwa sababu vikiwa vingi utekelezaji utakuwa haupo.

Suala jengine nilikuwa nazungumzia kuhusu vianzio vya mapato vimeelezwa humu vingi tu. Tunaingia kwenye kodi ya majengo na mambo chungu nzima, lakini kama walivyozungumza wenzangu ni vyema basi tungejua katika kodi ya majengo tunatarajia kukusanya kiasi gani, au unapokuja kwenye vianzio vyengine hivi kwa upande wa utalii kuna kodi chungu nzima ambazo Mhe. Abubakar Khamis Bakary alizitaja hapa, tungekuwa tunaambiwa basi katika kodi zile tunatarajia kupata kiasi gani na tuambiwe watalii wangapi walikuja au wanatarajiwa watakuja wangapi na kila mmoja atatupa kiasi gani, kwa hivyo lengo letu au matarajio yetu ni kupata kiasi hiki. Nadhani hiyo kidogo itakuwa katika suala zima lililozungumzwa kwamba bajeti ingependeza zaidi kuwa na uwazi, lakini imeficha ficha mambo mengi.

Kama ilivyotajwa habari hii ya 4.5 percent tumeambiwa tutapewa kiasi kadha, lakini kutokana na ngapi kwanza tujue hiyo misaada ya kibajeti ndio tutajua hiyo misaada iliyotajwa humu, isipokuwa mimi sikubaliani na kupewa 4.5 percent na tuna sababu ya kusema hivyo, sitaki niseme maneno mengi, lakini share yetu ni kumi na moja na hatuoni kama wenzetu wana dhamira ya kutaka kutupa hiyo share yetu kwa sababu kila siku wamekanyagia hapo hapo, anapandisha mafuta tu, lakini gia habadilishi kila kitu 4.5 percent na kwa bahati mbaya pale tulipokuwa tumenyamaza kimya labda watu walikuwa wanaogopa kusema hata hiyo 4.5 ilikuwa haipatikani. Sasa hivi ndio wanaanza kutupa kwa kelele zetu na tutaendelea kuzipiga kweli kweli, mpaka ije hii kumi na moja kama itakuwa muungano wenyewe upo, kama utakuwa haupo tutakuwa tumeandaa mambo mengine ambayo ya kuona jinsi gani hatukosani sisi na wao kila mmoja anaridhika na mwenzake yaani nakusudia muungano ambao haupo hivi sasa, utakuwa mwengine ambao hauna manung'uniko na kero na vitu vya aina kama hiyo. Kwa hivyo, uwazi katika hii bajeti umekosekana vitu vingi vimejificha maswali yanakuwa mengi sana.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa na mimi nataka nizungumzie suala moja suala zima la program za ukimwi katika maidara mbali mbali ya wizara zetu za serikali. Kama alivyozungumza mwenzangu jana hapa kwamba ukimwi sasa hivi mpaka watoto wadogo wanaelewa sasa kuendelea kupanga, kutupa pesa kwa ajili ya warsha na semina zinazohusu ukimwi itakuwa hatufanyi vizuri katika kuendeleza nchi yetu. Tayari kitu kimeshafahamika vyombo vinaendelea kutueleza. Kwanza niipongeze Serikali ya Mapinduzi kwa kuzuia suala zima la kuwa na mambo ya ushindani wa kiurembo na mambo mengine, mimi kwa binafsi yangu naona kwa kiasi fulani linahamasisha mambo haya ya ukimwi. Huwezi kuwachukua wanawake shababi ukawaweka utupu halafu ukasema unapiga vita ukimwi.

Sasa hili kwa sababu hapa kwetu halipo ni hatua tumechukua, lakini bado serikali ichukue hatua ya kuona vivazi huko mitaani watoto wetu haidhuru sio serikali moja kwa moja jukumu lake, lakini linaanza kwetu sisi wazazi, lakini mzazi kama anashindwa, basi serikali iwe ipo inahami masuala kama yale. Kuna mambo hayapendezi kuna watoto wa kiume Mhe. Spika, tunawazaa wazuri tu tena kiume ume, lakini wanakwenda kukaa mtoto utamkuta kasukwa vinywele kama harusi wa kizamani na herini kaweka mtoto wa kiume, sasa haya yanakuwa yanaashirikia kushajihisha ukimwi kwa sababu wenzetu wameshapitisha mpaka sheria za harusi za wanawake kwa wanawake, wanaume kwa wanaume. Sasa huwezi kusema hapa kwetu hayapo. Kwa sababu kwanza hatuna udhibiti wa watu wanaoingia wanakuja tu watu wa namna hizo.

Sasa haya ni lazima tuyaangalie vile vile, lakini suala la yale mafungu ambayo yamepangwa kwa ajili ya program za ukimwi ni uzuri yangehamishwa, mwenzangu jana alizungumza kwamba yaende yakatengeneza zile nyumba za Kengeja kule na mimi naungana nae mkono sana, lakini pia ukiacha maagizo ya Kengeja, zipo na shughuli yengine ambazo zinaweza kufanyika kupitia hili, kwa hivyo nilikuwa naomba sana suala hili lizingatiwe na Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kwanza kabla ya yote niwapongeze Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake wote katika wizara hii kwa kupanga bajeti hii kwa ukamilifu na yote yaliyokuwemo humu tukayafahamu kwa kina.

Mhe. Spika, kwanza kabla ya yote mimi nitaanzia na Wizara yako Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi pamoja na wetendaji wako ndani ya wizara yako, kama inavyoeleweka sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote majukumu yetu makubwa majimboni kuwasikiliza wananchi na kuwatekelezea yale ambayo yanawagusa, mara nyingi mzigo mkubwa majimboni unakuwa unawaelemea wawakilishi, wabunge na madiwani hususan wawakilishi pindipo wabunge wakiwa vikaoni, kwa hivyo mambo yote yanaelemea kwa wawakilishi. Wenzetu wabunge wakishamaliza bunge mara nyingi huwa wanapata safari ya kwenda nje kwa hivyo mambo yote ya jimbo yanamkabili mwakilishi na madiwani wake.

Kwa hivyo maana ya kusema hivyo Mhe. Waziri wizara yako ya fedha naweza kusema ndio wizara baba katika wizara baba, kwa hivyo kuna haja mambo mbali mbali ikiwemo maposho na mafao na matumizi mbali mbali ya waheshimiwa wawakilishi yakarekebishwa na ikaondolewa mapungufu yote

yaliyokuwepo ili kupewa kwa ukamilifu tukapata kuhudumia jamii katika maisha yetu. Kwa hivyo Mhe. Waziri mimi ningeliomba pamoja na watendaji wako wakaliangalia sana katika bajeti yao hii, ili angalau kule majimboni kikaonekana nini kinafanyika.

Mhe. Spika, kuna huu mfuko wa maendeleo ya jimbo kuweko kwa mfuko huu utasaidia kupunguza makero mengi majimboni, hii itasaidia sana wawakilishi wetu kwa yale maneno wanayosema wana vijiji na wananchi kuwa mwakilishi aoneshe maendeleo yake ndani ya jimbo sasa hapa itatusaidia. Kwa hivyo, naipongeza wizara hii kwa kupanga na kuweka mfuko huu wa kusaidia katika majimbo na maendeleo. Isipokuwa kubwa tu ninalomwomba watendaji wa mfuko huu wawe waungwana na wawe wakweli na uadilifu wa ukweli, isiwe kama tunakotoka huku kulikua kunasikitisha sana utakwenda kwenye mfuko huu kuanzia 2007 basi inafika mpaka 2010, huoni mafanikio wala kufahamishwa kama unahitajika au huhitajiki au hufai hupewa. Kwa hivyo kama tutakwenda na mfumo kama ule tutakwenda vizuri, kulikuwa na baadhi ya watendaji walikuwa wanakwenda na sifa hii kwa hivyo naomba kuanzishwa kwa mfuko huu wajirekebishe na waende kwa mambo mazuri, ili kuondoshea makero wananchi wetu katika majimbo yetu.

Mhe. Spika, ukweli husemwa tokea tunakotoka mwaka 1964 hadi hii leo tunajitahidi kuboresha maendeleo mbali mbali katika nchi yetu, lakini kuna wachache hawafahamu sijui au wanafanya maslahi yao au makundi yao na huwa wanadhorotesha mambo kwa makusudi, ili kuleta mdomo kwa wananchi. Kwa hivyo, nataka kuwambia baadhi ya watendaji wa mawizara wale waliokuwa hawawajibiki au hawatekelezi kazi zao kwa mujibu wa taratibu zilivyo baadhi ya siku tutakuja kumwomba Mhe. Spika, katika kanuni yetu apenyeze kineno kidogo yule mhusika wa wizara ambae kila tunavyoelekeza na kufahamisha kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu hafahamiki na wala haeleweki kwa hivyo aje hapa atupe maelezo ili na yeye asikike na wananchi kwamba kulingana na maslahi yote yeye kwa maslahi yake anatudhorotesha.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa nane kfungu cha kumi na nne naomba kunukuu kidogo.

Ukurasa wa nane kifungu cha 14 kinasema:

"*Kutokana na kushuka kwa uchumi duniani hususan Bara la Afrika kwa 2.0% mwaka 2009, kutoka 5.2% mwaka 2008".*
Kwa kweli viwango hivi kidogo vimeleta utatanishi na kutuyumbisha yumbisha lakini kwa upande wa nchi yetu hapa Zanzibar kwa sisi wananchi mara nyingi tunajua mapungufu tuliyokuwa nayo ya kushuka uchumi, kwa mfano hapo nyuma baadhi ya wananchi wetu walikuwa wakisafirisha matunda mbali mbali

kupeleka nchi za nje zikiwemo embe za Muyuni, wengine wakisafirisha vitu vya pwani ilikuwa ni njia moja wapo ya kujisaidia kupunguza ukali wa maisha. Sasa lakini ni kipindi kirefu bidhaa hizi huoni kusafirishwa wala huoni kushughulikiwa katika hali yoyote ile.

Kwa hivyo ningemwomba Mhe. Waziri katika mipango ya biashara kama hii ya matunda na bidhaa za pwani wakavipa mkakati wa nguvu na wataalam kuhamasisha wafanya biashara hizi ili wafanye kwa hali ya kuridhisha kwa kupata masoko nje na wao kujisaidia kimaisha.

Mhe. Spika, haya masuala ya uchumi wa ndani hapa kwetu sisi wananchi tunaweza kusema katika mwaka huu wa 2009, kidogo umeleta matumaini, kwa sababu baadhi ya vitu vingi tokea kupungua kwa bei ya mafuta ya petrol kidogo kumekuwa na unafuu ukweli husemwa, ukija upande wa Michele ilikuwa bei kubwa zaidi polo moja la kilo hamsini ilikuwa shilingi 45,000 mpaka 44,000 lakini hivi sasa imeshuka imefikia shilingi 30,000 mpaka 34,000. Ukija katika zana za ujenzi mabati yalikuwa bei ya juu shilingi 16,000 sasa hivi yamefikia shilingi 12,000 11,000 9,000 unayapata ya futi 10 na 8.

Kwa upande wa saruji kwa kweli hii ilikuwa na kiwango kikubwa sana ilifikia shilingi 18,000 mpaka 17,000 kwa mfuko mmoja, lakini leo imeshuka unapata kwa shilingi 12,000 elfu mpaka 11,000 na inaendelea kushuka.

Kuna vitu vingi tu vimepungua bei hata nondo kwa juhudi za serikali jinsi ilivyosimamia msimamo wa bei kwenye maduka na ushukaji wa mafuta. Kwa hivyo, baadhi ya wananchi wengi sasa wanashukuru kwa ushukaji wa bei kwa baadhi ya vitu.

Mhe. Spika, nije ukurasa wa 15 kifungu 26 kupanda kwa thamani ya mauzo ya karafuu duniani. Kama inavyoeleweka zao hili la karafuu ni uchumi ambao mkubwa kwa Zanzibar na umeanza kipindi kirefu. Mara nyingi utakuta katika masoko ya nje bei huwa inapanda kwa baadhi ya siku na siku nyengine inashuka. Kwa kipindi hiki katika bajeti hii kama alivyozungumza Mhe. Waziri kidogo mauzo ya nje yamepanda. Kwa hivyo, ningemwomba Mhe. Waziri kama kutakuwa na haja na akiangalia katika bajeti zake awaangalie sana wakulima wa zao la karafuu pamoja na wachumaji kama kutakuwa na haja ya kuongezwa, basi waongezwe ili kupata kuyashughulikia zaidi mashamba yale kwa kuyaimarisha na kupanda mikarafuu mingine mipya na kuyafanyia usafi wa aina mbali mbali, ili mazao yale yazae kwa wingi zaidi.

Kwa sababu kama inavyoeleweka zao hili halitabiriki, baadhi ya siku linapanda na baadhi ya siku linashuka. Kwa hivyo, kuna hatari kipindi cha mbele linaweza kuja kupanda zaidi na kama hatukuliimarisha vizuri tutakuja kuona

hatuna zao hili katika ghala zetu. Ningemuomba Mhe. Waziri kitapoingia chochote atizame kama kunaruhusu kuongeza nyongeza kidogo, basi waongezewe wakulima hawa ili wapate motisha wa kuyaimarisha mashamba hayo.

Mhe. Spika, nije katika suala la zao linalolimwa sana na kinamama waliokuwa mwambao wa pwanipwani la mwani. Kuna wenzangu wengi wamelizungumzia, lakini mimi nitalizungumzia kwa muono ninaoujua.

Mhe. Spika, zao hili kwa kipindi kirefu wananchi wetu limekuwa tegemeo lao kubwa, muda mrefu wanakuwa pwani kwa kushughulikia suala hili, huacha kazi zao mbali mbali kwa kushughulikia zao hili. Hivi sasa ni kipindi kirefu wakulima hawa hali zao zimekuwa duni, utakuta kutwa yuko pwani akifika nyumbani anachokimiliki ni kula yake tu na hiyo tena kwa mashaka mashaka. Mtu huyo humuoni kuwa na nyumba nzuri wala kupata hakiba ya kujiwekea baadae. Kwa hivyo, ningemwomba Mhe. Waziri kama huko nje soko limekuwa zuri, basi na wakulima wetu hawa waongezewe kidogo ili waingie moyo zaidi kulima zao hili.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 14 kifungu cha 24, hiki kimezungumziwa kuhusu wastaafu kulipwa madeni yao vizuri Zanzibar. Kitu nilichokuwa sijakiona katika bajeti hii wale wastaafu wa Jamhuri ya Muungano ambao wakiwemo maaskari wetu wa ngazi mbali mbali wa Muungano, sikuona jinsi ya kulipwa mafao yao. Kwa hivyo, namwomba Mhe. Waziri atapokuja kujumuisha anielekeze na wao wanafikiriwa vipi.

Jengine kuna suala la pencheni ambapo baadhi ya wenzangu wengi hapa wamelizungumzia, lakini kwa kuwa na mimi mjumbe huwa nafuatwa na jamii kuzungumziwa suala hili sina budi nilizungumze. Kwa kweli pencheni imekuwa ndogo kwa watu wetu ambao wanalipwa, kwa hivyo sasa kuna haja kama hali itakuwa imeruhusu baada ya kiwango kilichopo, basi wazidishiwe angalau nusu yake na wao wapate kujikimu kwa makero mbali mbali ambayo yanawakabili. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili utapokuja ujaribu kutufafanulia tujue namna gani ya kufanikisha pencheni ya watu wetu hawa.

Niende katika ukurasa wa 27 kifungu cha 50, Kodi ya Majengo. Ili kuimarisha kodi ya ndani, Mhe. Waziri hili kipindi kilichopita tulijadili sana suala hili na tukatoa ufafanuzi mzuri wa yale majengo yanayohusu kutolewa kodi. Kwa hivyo, hofu yangu ni kuwaomba watendaji katika sekta hii vile watavyoelekezwa ni kwamba wafuate maelekezo wasije wakazidisha yao ambayo hayamo ndani ya maelekezo. Kwa hivyo, wakipewa pima wasije wakazidisha nyanda. Kwa matatizo hayo baadhi ya watu wetu wengi wameshakuwa na hofu na wasi wasi kuwa baadhi ya vijumba vyao vidogo

vidogo vilivyo chini ya milioni 60, wana wasi wasi labda suala hili litawafika. Ningewaomba wataalamu wakipita wajaribu kuhamasisha vizuri na walenge mle mlimokusudiwa kwa mujibu wa vikao vilivyopita na kuvijadili ili kutoa hofu kwa watu wetu wasiohusika na kodi hizi za majengo.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 34 kuhusiana na mambo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa kuwa Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii atakuja na hotuba yake hapa, kuna haja nizungumze kwanza kwa kuwa limezungumzwa ndani ya bajeti kuhusu kampeni ya chanjo ya watoto wenye umri wa miezi 6 hadi miaka 10.

Mhe. Spika, watoto wenye umri huu mara nyingi hujitokeza katika vituo mbali mbali kwa ajili ya kufanya chanjo na mambo mbali mbali yanayohusika na hayo. Kwa hivyo, ninachotaka kukiomba ni kwamba tuwe waangalifu sana wataalamu wa shughuli hizi ili kuziangalia zaidi chanjo zetu na mipango mbali mbali inayohusika na chanjo, ili baadae tusije tukapata madhara kwa watoto wetu hao.

Mhe. Spika, maana ya kusema hivyo kuna kipindi fulani nilifanya ziara ya kutembelea Wizara ya Afya Kitengo cha Ulemavu wa Watoto wenye maradhi ya Mifupa. Kule kuna baadhi ya watoto chini ya miaka 10 ukitembelea siku za kliniki zao utakuta wengi walemavu, viziwi, mabubu, kwa kweli kimenitisha sana hicho na sijui sababu gani iliyosababisha vile. Kwa hivyo, ningeomba katika utaalamu huu tukaangalia zaidi isije ikawa kuna madhara fulani ambayo yanatokezea baadae ndio yanaathiri watoto wetu. Mhe. Spika, yasije yakatufika kama yaliwafika wenzetu kule Japan Hiroshima kupigwa bomu matokeo yake mpaka leo imekuwa kila anayezaliwa ana kasoro au ulemavu. Kwa hivyo, ningeomba hapa tuwe tunaangalia sana ili yasije kutokea madhara kama hayo.

Mhe. Spika, nikiendelea hapa hapa nimpongeze Mhe. Waziri wa Afya pamoja na watendaji wake kwa juhudi yao kubwa wanayoichukua katika wizara hii, kwa kipindi kirefu ilikuwa hairidhishi, lakini leo hii majengo mengi ukienda Wizara ya Afya yametengenezwa yamekuwa mazuri sana na baadhi ya vifaa vinaonekana na dawa tunashukuru zinapatikana, chache tu ndio utazoambiwa hamna ukatafute. Kwa hivyo, kwa hili nawapongeza sana Wizara ya Afya kwa juhudi waliyoichukua ili kusaidia na kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, yako mengine kwa Wizara hii ya Afya, lakini madhali mwenyewe atakuja kutoa hotuba yake nitakuja kuyaogelea wakati huo wa hotuba yake.
Mhe. Spika, kwa kuendelea nakuja katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa vile nayo imetajwa ndani ya bajeti hii. Nawapongeza sana Wizara ya Mawasiliano pamoja na watendaji wake na waziri wao kwa ujenzi wao

mkubwa wanaotuonesha katika mabarabara haya makuu ambayo yamepita katika sehemu mbali mbali ikiwemo vijijini na mijini.

Suala hili kwa kweli linafurahisha, barabara kuu zinapendeza na nzuri ingawa baadhi ya wengine kwa makusudi wanajifanya vipofu hawayaoni maendeleo haya, lakini ukweli kama si matatizo mimi ningemwomba Mhe. Waziri wa Nchi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa utani tu awachukue pamoja na fimbo yake akawagongee barabara ya Fumba ili kuwaonesha maendeleo yalivyo, barabara za Mfenesini, Wambaa, Makombeni na kadhalika jinsi zilivyotandikwa. Haya yote ni maendeleo ya wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kwa sababu hii ndio inayotoa bajeti ya kufanikisha hayo.

Mhe. Spika, ninachowaomba zaidi ni kufanya bidii kwa suala la barabara za *feeder road* kwa kuwa mara nyingi tumekuwa tukizizungumzia kila bajeti. Kwa hivyo, nimuombe hizi nazo zisimamiwe kwa dhati kabla ya kipindi hiki kumalizika angalau ionekane juhudi ya utekelezaji wake. Barabara hizi majimboni viongozi wetu wa majimbo pamoja na wananchi wanajitahidi kutia vifusi, lakini kwa baadhi ya maeneo havikai kwa sababu ya maporomoko ya vilima kwa siku za mvua inakuwa vinakwenda na maji, kwa hivyo, nguvu za wananchi na viongozi wa majimbo huwa zinapotea. Ningemwomba Mhe. Waziri suala la barabara za *feeder road* aliangalie kwa kina ili mle mwenye kero kubwa kama ndani ya Jimbo langu la Amani sehemu za Ziwatue amweke barabara pamoja na njia.

Vile vile kuna barabara moja ambayo mara nyingi huwa tunaizungumzia hapa na wakulima wengi wanakwenda kulima nikiwamo na mimi barabara ya Koani/Jumbi. Mhe. Spika, hii tumeshaizungumzia muda mrefu na kuna baadhi ya wakulima kule ndiko wanakopata riziki zao na kuna miradi mingi tu. Kwa hivyo, ningeliomba na hili nalo atizame mfuko wake ukiwa unaruhusu angalau wazifanyie ukarabati kwa kiwango cha lami mle mlimokuwa mzito zaidi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nije katika suala la kuzidishwa kwa ushuru wa vinywaji kama vile bia, sigara na ulevi mkali. Mimi ningeiomba wizara husika ikaangalia kwa makini ikiwa hii kuzidisha ushuru isijekuwa ndio changamoto ya kuzidisha yale maovu yanayotokana na vinywaji hivi. Kwa sababu kipidni kirefu hapa tumekuwa na vijana mitaani wanaleta kero sana ambao ni wanywaji wa vinywaji vikali kama vile kero la wizi mdogo mdogo na kunyang'anya watu vitu vyao kama vile simu na mambo mbali mbali ya kihuni. Kwa hivyo, ningeomba hapa Mhe. Waziri anayehusika na hili tukazidisha kasi zaidi au kama kuna bajeti pungufu, basi hapa walinzi wetu wakazidishiwa bajeti ili kuondosha makero haya.

Mhe. Spika, kwa kuwa nimezungumza mengi kwa hivyo, mimi pamoja na viongozi wenzangu na wananchi wangu wa Jimbo la Amani hotuba hii ya serikali naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na naomba niendelee na mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nataka niungane na waziri kivuli aliyesoma hotuba yake kwa niaba yetu na kwamba *document* ile kama alivyosema Mhe. Zakiya Omar Juma ni *working document*.

Mhe. Spika, katika Baraza hili wajumbe tulioko hapa na katika hafla hii au shughuli tunayoendelea nayo ya kujadili bajeti ya mwaka huu au mwaka wa fedha unakuja, Baraza hili linaweza likafanya mambo yafuatayo:-

Baada ya majadiliano ya kina na kutafakari kila kitu basi ama Baraza hili linaweza likaibakisha hotuba hii na mapendekezo haya ya makadirio na matumizi kama yalivyo, desturi ambayo tumezowea kwa bajeti zilizopita. Lakini vile vile Baraza hili linaweza likafanya mabadiliko makubwa ama kuongeza au kupunguza kubadili vipaumbele vya mambo mbali mbali yaliyopendekezwa hapa. Lakini baraza hili hili linaweza kabisa kabisa baada ya majadiliano hayo Mhe. Spika, wakaikataa kata kata bajeti yote. Sasa ni vizuri kwanza tujue majukumu haya tunayo sisi hapa na uwezo huo tumepewa. Kwa hivyo, mawazo ambayo yametolewa na kambi ya upinzani ni mashauri ambayo nina hakika kama sio yote, basi mengi kabisa yanaweza yakaingizwa katika hotuba hii ya Mhe. Waziri na hatimaye tukapitisha bajeti hii ikiwa angalau mwaka huu ina tofauti kidogo na tulivyozoea.

Mhe. Spika, katika bajeti ya waziri kivuli amenukuu nukuu mbali mbali za mawaziri watatu waliotangulia. Amenukuu nukuu za Mhe. Amina Salum Ali, Mhe. Suleiman Othman Nyanga na Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame. Naomba ili niweke vizuri mchango wangu ninukuu nukuu moja tu katika hizo ambayo katika *document* hii ya waziri kivuli iko ukurasa wa 8 ya Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame. Nukuu hiyo ni majibu ya swali nambari 58 la tarehe 31 Machi, 2009, yanasema hivi,

"Mhe. Spika, lazima nikiri kwamba kweli tuna matatizo na TRA na wafanyabiashara wetu kila tukijitahidi serikali kuwatetea bado TRA inawabughudhi hasa Dar es Salaam. Tumefanya mazungumzo mengi hata katika level ya Mhe. Waziri Kiongozi na Mhe. Waziri Mkuu kujaribu kutafuta suluhisho. Tunajaribu, tunakwenda, tunakubaliana mezani na wakuu wao wanakiri, lakini wale watendaji tumegundua kuwa ndio wakorofi. Sasa tunakuja na mkakati mpya alivyosema kwamba, tubadilishe sera, basi sera

yenyewe sasa nataka kushauri kwamba wale watendaji wakorofi tuwachukulie hatua zifaazo. Kwa sababu imekuwa zaidi ni utashi wa watu kuliko sera yenyewe ya serikali, hawaambiwi. Kwa sababu vima vya kodi ni hivyo hivyo na shirika ni hilo hilo kwa nini huku wawe hivi na kule wawe vyenginevyo. Kwa hivyo, tumegundua ni ukorofi wa baadhi ya watu tu". Hii ndio nukuu tu ambayo na mimi nimeinukuu katika *document* ya waziri kivuli.

Mhe. Spika, nimenukuu hivi kwa hoja ambayo naiwasilisha sasa. Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*). Mhe. Spika, historia ya *VAT* imeanza na Baraza hili haidhuru baadhi ya wajumbe sio. *VAT* si *tax* ya Muungano, wakati sheria inaanzishwa Bara ya *VAT* mwaka 1996, lakini ilitumika mwaka 1997, Baraza lako tukufu hili sio wajumbe hawa baadhi yao lilifanya semina hapa. Kumbukumbu zangu zinanambia kwamba semina hiyo Wajumbe wa Baraza kwa umoja wao walikataa, lakini kwa sababu zinazojulikana huko huko *VAT* nayo ikaigwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, wenzetu wa Bara walianza na asilimia 20 na sisi tukaiga asilimia 20, wenzetu sasa Bara kwa sababu zao wenyewe wamekuja na asilimia 18 wakati sisi bajeti yetu ni *VAT* ya asilimia 20. sasa Mhe. Spika, mimi nina mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza *VAT* kwa uchumi wa Zanziba kwa mawazo yangu na muono wangu *it is a wrong tax*, ni kodi ambayo haifai kwa hapa. Kwa hivyo, *VAT* hii tutakapoiondoa au pengine kuipunguza sana yatakayotokea ni haya.

Kwanza *VAT* iko kwenye mahoteli, sukari, mafuta, umeme na kwengineko; tukiiondoa *VAT* nina hakika *hotel occupancy* itaongezeka. Wageni wengi katika mahoteli watakwenda, lakini si hiyo tu, manunuzi katika maduka yataongezeka kwa kiasi kikubwa. Kama hiyo haitoshi Mhe. Spika, ukwepaji wa kodi utapungua sana, watu wengi wanakwepa kodi kwa sababu *tax* ni kubwa, *tax* ukiiondoa au kuipunguza, basi kunakuwa na vivutio kwamba kwa *tax* hii wacha nilipe, sasa hatimaye nini?

Mhe. Spika, hatimaye ni kwamba kama kweli nadharia na *practice* ya MKUZA iko katika vichwa vyetu unapomwondolea mtu *VAT* ya umeme mfano, uwezo wake wa kimaisha unauongeza, unapomwondolea asilimia 20 ya *VAT* ya sukari uwezo wa watu kunywa chai utaongezeka na matumizi mengine. Kwa kifupi Mhe. Spika, ukiondoa *VAT* au kupunguza kwa kiasi kikubwa nina hakika ile nadharia ya kumwwezesha mnyonge ambazo zimeingizwa humu karibu shilingi milioni ngapi sijui, uwezo wa mnyonge, Mzanzibari wa kawaida unaoboresha maisha yake utaongezeka.

Mimi ushauri wangu ni kwamba kama kutoka asilimia 20 kwenda 18 kunakuwa na upungufu wa bajeti yetu kwa bilioni mbili, hii mimi nilitaka upunguzwe mpaka asilimia 10 lakini wacha twende pole pole, nashauri kabisa *VAT* ipunguzwe hadi asilimia 16. tujiulize hivi ambavyo vimepangwa na serikali, fedha hizi zitapatikanaje ukipunguza *VAT* kutoka asilimia 20 hadi 16 kutakuta na upungufu katika bajeti yako ya kiasi cha bilioni nane.

Mhe. Spika, nina hakika kwa sababu ambazo nimezitoa kuongezeka kwa watalii mahotelini, kuongezeka kwa manunuzi, ukwepaji wa kodi na kama tutawawezesha *ZRB* kwa sababu ndio kazi ambayo tumewatuma hapa. *ZRB* kazi yao ni kukusanya kodi, nina hakika watakuwa makini zaidi na watakusanya kodi zaidi ya hiyo bilioni nane ambayo ni mapungufu, tutakuwa tumepata faida kubwa kwanza watu wetu wanyonge zaidi ya asilimia 80 Wazanzibari watapata unafuu wa maisha kwa kupunguza *VAT* hadi asilimia 16, ingawa ukiiondoa yote watapata unafuu zaidi, lakini nasema twende pole pole.

Si hilo tu, *ZRB* kama nilivyosema wakiwezeshwa na kama tutaongeza hatua nyengine kwamba *TRA* shughuli zake zifanywe na *ZRB* kwa nukuu ambayo nimeinukuu hapa. Wafanyakazi wa *TRA* ni wakorofi Dr. Mwinyihaji amesema, sera ni kuwaondoa au kuwachukulia hatua, hakuna hatua nzuri kama *TRA* isifanye kazi zake hapa, kwa sababu *ZRB* wana uwezo wa kutosha, wana nyezo nzuri za kukusanya kodi zote zile zinazokusanywa na *TRA* na hizi ambazo wanakusanya wao. Nina hakika kama ambavyo nina hakika ya kufa tukichukua hatua hizi Wazanzibari watajisikia kwamba kweli Baraza la Wawakilishi ni wabunifu na kweli wanatujali. Vyenginevyo Mhe. Spika, tutakuwa tupo pale pale kwamba lazima tuige Bara jambo hata kama si la Muungano na sasa hii itakuwa kama ni trend.

Mhe. Spika, mimi nashauri kwamba katika kipindi hiki tubadilike kidogo isiwe wanachofanya wenzetu na sisi tunafanya. Wao wanafanya kwa sababu zao za msingi. Walipofanya hivyo ni nani alishauriwa huku Zanzibar kupunguza asilimia 20 hadi 18. Haidhuru si ya Muungano lakini si tumewaiga, basi hawaoni hata hilo. Hakuna aliyeshauriwa nina hakika. Kwa hivyo, hilo nataka nifikie hapo na naamini kwamba kuna wenzangu wengine watachangia.

Mhe. Spika, kwenye misaada ya kibajeti asilimia 4.5, hii tumeambiwa imeanza tangu mwaka 2003/2004. Kwa hivyo, kuna miaka minne huko nyuma sisi hii tulikuwa hatupati kwa mujibu wa hotuba hii ukurasa wa 59. Kama ni hivyo na hii ni haki yetu, nataka nimuulize Mhe. Waziri kwamba ana sababu zipi anazozijua yeye ama kwa kuambiwa ni hao au kwa kufikiria tu. Kwa nini miaka yote hii kama kweli Serikali ya Muungano ilikuwa inapata. Kwa nini walikuwa wanatunyima haki hii?

Mhe. Spika, siishii hapo tu, ni kwamba kwa sababu ilikuwa haki yetu na ni haki yetu. Yafanywe mahesabu watulipe pamoja na *interest, arrears*, mwaka 2003/2004 tulitakiwa tupate ngapi? Mwaka 2004/2005 ngapi? Wasipofanya hivyo zile dhana zitakuwa sasa hivi si dhana kwamba kweli Muungano ni kikwazo katika uchumi wa Zanzibar na ni kwa makusudi nina hakika. Kama watatulipa haki yetu hii hasa katika mwaka huu wa fedha unaokuja basi Dk. Mwinyihaji Makame ataweka namba nne. Hakuna mradi, hakuna kazi za serikali za kawaida zitakazokwama kwa sababu ni fedha nyingi.

Mhe. Spika, nizungumzie zao la karafuu. Mhe. Spika, zao la karafuu kama serikali kweli inadhamiria kupunguza umasikini, basi ili wawapunguzie umasikini Wapemba na Wadonge maana yake humo ndio karafuu ninamoziona kwa wingi, wa-*liberalize* zao hili la karafuu tumekuwa tukisema sana.

Mhe. Spika, wengi tunakumbuka kuna kipindi bei ya karafuu ilikuwa kilo shilingi 3,000/=, Mhe. Zainab Omar Moh'd ni shahidi maana yake anapokaa yeye ni mikarafuu mitupu. Kwa Pemba hakuna kijiji chochote ambacho hakikuwa na gari ya abiria, hata kama hakuna barabara ilikuwa inatengenezwa, tulikuwa na gari za abiria kila kichochoro, kilo shilingi 3,000/= hiyo. Nyumba ambazo zilijengwa mpya na kuwekwa bati hazihesabiki. Ndio siku hizo zilikuwa nyingi sijui kama kulikuwa na watu ambao hawana waume. Kwa ufupi, masikini Mpemba na Mdonge alijisikia kwamba kweli sasa kumbe zao la karafuu lina thamani. Hiyo nasema ni bei tu kuongezeka.

Mhe. Spika, jana hapa Mhe. Abubakar Khamis Bakary alitoa mfano mzuri. Kwa nini tusiwaige Waganda walivyofanya, kwani kuiga jambo zuri kuna ubaya gani. Kahawa haiuziki kila siku hakuna bei wakulima wanalalamika mibuni ile inakatwa, wakasema hapa basi wakabuni *formula* nzuri sana. Kwa hivyo, tunaweza kubuni na sisi kwa sababu tuna mahoteli mengi, kila hoteli peleka vipakti vizuri umevi-*pack*. Tunacho kiwanda kule cha ku-*pack* karafuu na mafuta, *label* nzuri tu na matangazo mazuri ya kuvutia, kila hoteli weka tunawaambia tunakupeni hizi pakti 2,000. Mtalii anaondoka anacheka, utaambiwa bwana wee zawadi yako hii, anachukua kama vile ni zawadi kumbe kakaangiwa mafuta yake.

Mhe. Spika, Waganda waliuza kahawa mpaka ikawa hawana tena kahawa tena kwa bei ambayo walitaka wao. Kwa nini sisi tusifanye hivyo? Anakwambia mtu karafuu haina bei atakuamini nani? Serikali imefanya mpango gani? Kwa kweli kama hakuna kitu nyuma ya pazia katika suala la karafuu hebu tuigeni mpango huo tuone mkulima wa karafuu aliyeko Pemba na Donge na kidogo hapa Ndijani hatotononeka. Huu umasikini tunaouzungumza wengine tunauweka sisi kwa sera zetu ambazo hazitekelezeki, hata ukizitekeleza inaonekana hakuna uhalisia wa mambo yenyewe. Naamini kabisa ili

umkomboe mkulima wa karafuu popote alipo na mifano hiyo ambayo nimeitoa, namshauri kabisa Mhe. Waziri anayeshughulikia mambo ya Uchumi basi hili ni moja katika mambo ambayo tuyazingatie.

Mhe. Spika, nizungumzie ahadi za wahisani. Mimi nimekisoma kitabu hiki, katika program hizi 22 na miradi 65 nimewahesabu wahisani na taasisi zote ambazo humu zinaonekana kwamba zitasaidia program hizi na miradi hii, hawa hawazidi 36. Mradi huu *World Bank*, mradi huu *BADEA*, mradi huu Al – Youseif. Lakini humu ambao wameahidi na wameshukuriwa ni zaidi ya 50.

Sasa nauliza kama program zetu ni hizi 22 na miradi 65 na walioahidi ni zaidi ya 50, lakini wanaoingizwa humu ni 36 kwa kila mradi na program. Hawa wengine wameahidi nini na wameahidi lini? Ni kwa mwaka huu au mwaka gani? Lakini lazima iwe ni mwaka huu kwa sababu bajeti hii ni ya mwaka huu. Sasa Mhe. Waziri hapa aje atwambie wahisani hawa wameahidi kwa maandishi, au kwa hadithi tu, au njiani tu na watasaidia miradi ipi na ipi.

Mhe. Spika, nikiendelea na hayo ni kwamba katika bajeti ya mwaka 2008/2009 wafadhili ilikuwa wachangie shilingi bilioni 173.75 lakini wakatoa mchango wa asilimia 35.33. Wenzangu wameeleza na hata Waziri kivuli ameeleza lakini na mimi naomba hapa niendelee kukumbusha. Makadirio ya mwaka huu wa fedha unaokuja kesho ni shilingi bilioni 199, mwaka jana shilingi bilioni 173 wametoa asilimia 35, mwaka ujao shilingi bilioni 199 hatujui watatoa ngapi. Sasa makisio haya mbona yanaonekana hayana uhalisia. Ukweli hapo uko wapi, kama walitupa kiasi hiki na mwaka huu tunaomba zaidi ya kile pale. Ni sababu zipi za msingi na ni kwa sababu gani hasa walitoa 35 na mara hii tunasikia kwamba tunawakisia zaidi wakati kile kidogo cha mwaka jana hawakuweza kukitoa.

Mhe. Spika, si hivyo tu, mwaka jana ukichukua orodha ya walioshukuriwa kwa misaada yao na mwaka huu ni wale wale wa mwaka jana unawatoa tu kwenye kompyuta unawabandika pale, kama kuna tofauti basi ni mmoja au wawili. Kwa hivyo, hakuna tofauti ya wafadhili wa mwaka huu na mwaka unaokuja lakini kuna tofauti ya ahadi hizi ambazo zimetolewa. Mhe. Spika, hilo nasema nakumbushia.

Mhe. Spika, jengine ambalo ingekuwa vizuri sana hasa kwa uchaguzi wa mwakani ionekane kwamba Baraza hili kumbe wana mambo mengine wanaweza wakaingiza yakaonekana kuna mabadiliko. Mhe. Spika, katika zama za sasa walemavu ni watu maalum. Sasa hivi huwezi ukajenga jengo lolote rasmi kama hukuweka *provision* ya mlemavu. Mahospitalini utakuta kwamba kuna *track* maalum inachukua nafasi ya zaidi ya asilimia 20 ya lile jengo la

kuzunguka tu ili mlemavu na kigari chake aweze kupita. Au kuna lifti hata kama ni nyumba ya ghorofa mbili au tatu.

Mhe. Spika, sasa mimi nasema walemavu duniani ni watu maalum na sisi tuonekane kwamba tunawajali wenzetu kwa sababu kama alivyosema Katibu Mkuu wa CCM Luteni Yussuph Makamba kwamba kila mtu ni mlemavu mtarajiwa. Sasa rai hii ya kambi ya upinzani kwamba walemavu wote waliopo Zanzibar na watakaokuwepo tena basi wasaidiwe. Kama majengo tunayabadilisha kwa gharama kubwa ili kuweka *provision* ya wao wenzetu wajisikie wamepata ulemavu ule si kwa sababu waliutaka, wengine wamezaliwa nao, wengine ajali na wengine magonjwa, basi tuonekane kwamba tunabadilika. Ukifanya mahesabu walemavu wote kama wale wanaofikiriwa kupewa shilingi 50,000/= watapewa watu wazima, watoto wadogo sijui kiasi gani lakini kwa ujumla ni karibu shilingi bilioni 2.4.

Hivyo kweli katika bajeti hii ambayo ina shilingi bilioni 412 kuwapa 2.4 walemavu ambao si asilimia ndogo kuna ubaya gani. Mimi nafikiri tutakuwa tunajiongezea hadhi tu kuonekana duniani kwamba kweli sisi katika mambo ya kuwajali wenzetu walemavu na sisi tuko mbele, au *atleast we swim in the current*.

Mhe. Spika, nakuja miradi ya *MCC* yaani *Millennium Challenge Corporation.* Hii imeingizwa kwenye program hizi na miradi hii. Huu wa *marine cable* kutoka Ras Kilomoni mpaka Fumba inaonekana tayari ume-*take off.* Lakini kuna maneno ambayo nataka Waziri hapa aje atwambie ni maneno tu au kuna usahihi wake kwamba miradi ya barabara zile 5 za kilomita 35 Pemba hauta-take off mpaka baada ya uchaguzi. Lakini hii mingine tayari imeanza. Hii nakusudia ni miradi ya *MCC*. Program hii kwa mujibu wa bajeti hii kuna mabilioni ya fedha. Sasa je, program imepewa fedha kwa ajili ya *cable* yetu sasa hivi na nyengine itatoa baadae? Nafikiri hii nimefahamika. Hii iko katika kitabu cha 2 jadweli namba 7 na 8 ukurasa wa 27 na 29.

Mhe. Spika, nataka nimalize juu ya wakati na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndio anastahiki kushukuriwa kwa kutupa ihsani tukaweza kukaa hapa hali tukiwa tunatuta na maneno mengi yakitutoka mdomoni. Asingetaka sote tungeweza kukaa humu kila mmoja ikawa mdomo wake haufumbuki. Sasa kwa neema yake hiyo namshukuru na namswalia Mtume wake Muhammad (SAW) kwa kuwa ndio aliyemleta kutuongoza na miongozo yake ndio tunayotakiwa tuifuate.

Mhe. Spika, baada ya hayo, wenzangu wengi wamezama katika nadharia za ukuzaji uchumi. Lakini mimi si mchumi sijasoma uchumi hata siku moja. Kwa hivyo, nitaingia zaidi katika nadharia ya kuwaangalia wananchi na bajeti, watafaidika kiasi gani wananchi katika bajeti hii, lingefanywa lipi lingekuwa zuri zaidi kwa wananchi kwa bajeti hii, lipi nalihisi kidogo lina matatizo katika bajeti hii kwa wananchi. Huko ndio nitakakoogelea tukijaaliwa.

Mhe. Spika, labda nianzie tu kidogo kama alivyoanza bamkwe hapa kuhusiana na hii kodi. Mhe. Spika, walipaji kodi ni wananchi, iwe ya *VAT*, iwe ya nini, kodi zote zinalipwa na wananchi. Tajiri anapokwenda akachukua mzigo wake pahali popote pale kwa bei yoyote aliyoichukua, akifika hapa akalipa kodi yoyote atakayoilipa, hatimaye kodi hii inalipwa na wananchi.

Kwa sababu tajiri bidhaa yake aliyoileta anajua kainunua kwa kiasi gani, anajua kaisafirisha kwa kiasi gani, anajua kailipia ushuru wa kiasi gani, anajua shughuli za usafiri za ndani na nje kuingiza ghalani ni kiasi gani, anajumlisha zote hizo. Gharama zake za usafiri alizokwendea huko nje na kurudi, gharama za kulala na kufanya mambo yote atakayoyafanya zote anaziingiza mle katika hesabu, halafu anajua biashara yangu hii imefika hapa katika duka langu kwa kiasi kadhaa. Ikifika dukani anaingiza na faida yake pale, anajua kitabu hiki nikishakukiuza shilingi 5,000/= nitakuwa nimeshalipa gharama zangu zote pamoja na faida yangu ninayoitaka ya kujengea ghorofa. Mhe. Spika, atakayekuja kununua miwani hii ndie atakayelipa gharama zote zile za kodi.

Kwa hivyo, tunaposema kodi ya *VAT* na nyenginezo mlipaji ni mwananchi wakati ambapo chajio chake kinampa shida. Lakini kwa sababu ya ulazima wa kupata kitu anachokihitaji inambidi afanye njia yoyote juu chini, chini juu, ikiwa atanyang'anya, atakopa almuradi apate pesa anunue kitu kile ambacho ni cha lazima kwa maisha yake. Sasa kadri kodi unavyoipandisha ndio kadri mwananchi unavyompa mzigo mkubwa zaidi ama wa kuomba, kunyang'anya, kuiba au kufanya njia yoyote ya kupatia pesa apate mahitaji yake ya lazima. Mhe. Spika, naungana na wenzangu waliosema kuwa hii *VAT* ipunguzwe zaidi baada ya hapa.

Sitaki niseme ipunguzwe sana bora nikubaliane tu na bamkwe, asilimia 16 sio mbaya. Hatufanyi hivyo kwa jengine lolote isipokuwa tunafanya hivyo kumsaidia mwananchi yule aliyeko Matemwe, Wambaa, Uzini na Uzi ndio tutakayemsaidia tutakapofanya hivyo.

Mhe. Spika, nikiachana na hilo labda nije sasa katika lile tamko rasmi la bajeti ya mwaka huu, la kuwa hii ni bajeti ya maendeleo ya miundo mbinu kwa kuimarisha kilimo na utalii kama tulivyoambiwa katika ukurasa wa 50. Sasa ili tujue kama hilo ni la kweli basi Mhe. Spika, kuna haja ya kuangalia hiyo

miundo mbinu ya kuimarisha kilimo na kuangalia miundo mbinu ya kuimarisha utalii iliyoko na inayotarajiwa ifanywe ili mambo hayo yaweze kupatikana kwa kumsaidia mwananchi. Haikusudiwi kuimarishwa miundo mbinu ya utalii kwa kuwasaidia watalii hapana, tukiwa na lengo hilo bado. Bajeti hii inakusudia kuimarisha miundo ya utalii kwa kuwasaidia wananchi ili wapungukiwe na ule mzigo mzito wa kodi. Kwa sababu kadri watalii wakavyokuja wengi zikapatikana kodi nyingi za shughuli za utalii, pengine mzigo wa wananchi kule wa kodi unaweza ukawa mdogo zaidi.

Mhe. Spika, tukiangalie kilimo, kwa mujibu wa kitabu cha Mhe. Waziri kuna mambo yamefanywa katika kipindi kilichopita na pengine yatafanywa tena katika kipindi kijacho. Katika kipindi kilichopita tunaambiwa katika ukurasa wa 32 kuwa kuna mafunzo yaliyotolewa kwa wakulima. Lakini mimi ninalotaka niulizie hawa wakulima wanaopewa mafunzo haya wanapatikana vipi? Mafunzo haya yamepelekwa pahali gani? Yameenea? Yanakwenda kwa sheria? Yanakwenda kwa vijiji? Yanakwenda kwa wilaya?

Kwa sababu utakapochukua mtu mmoja mmoja kwa mfano kutoka kila shehia ukasema hawa nakwenda kuwapa mafunzo ya kilimo kwa ajili ya shehia ile tujue tumetia maji pakachani. Kwa sababu yule mtu mmoja utakayempa mafunzo ikiwa ana hamu atayatumia mafunzo yake yeye mwenyewe lakini usitarajie kama atamfundisha mtu mwengine. Kama yeye mwenyewe anahamu, kama hana hamu basi atakuja pale atakusikiliza utampa chai ataondoka atakwenda zake na mafunzo yake ndani ya kichwa chake.

Lakini ikiwa yanakwenda kwa mfano kwa shehia, shehia nzima ikakusanywa wakapewa mafunzo, tena mafunzo hayo yasiwe juu kijijini yawe mabondeni wakati wa kulima. Hayo ni mafunzo yanaweza yakaleta faida kwa sababu ni mafunzo yanayotolewa pahali ndipo na wakati ndipo na wanapewa watu ndio. Sasa sijui mafunzo haya yaliyotolewa ni ya aina gani.

Lakini Mhe. Spika, kilimo tunacholima hivi sasa hatujamsaidia mkulima, wala hatumsaidii mwananchi mwengine yeyote aliyekuwa si mkulima. Kilimo kwa zana hizi tunazolimia ambazo babu na babu na babu wa babu zetu ndio walizokuwa wakitumia. Wakati ardhi ilipokuwa bikra shina moja la muhogo lilikuwa haling'olewi zima, kila siku nyumba ya watu 6 au 7 mnang'oa mzizi mmoja tu wa muhogo. Kilimo hiki kilikuwa na faida. Lakini leo ambapo ukilima inabidi uvune nusu shamba kwa siku ndio upate chajio, kilimo hiki hakifai tena tunawaumiza tu wananchi wetu bure.
Mhe. Spika, umefika wakati wa kuhakikisha kuwa bajeti yetu inaweka nafasi ya kununua zana za kisasa za kuweza kuwapa watu wetu walimie. Si lazima matrekta makubwa makubwa yenye bei kubwa. Siku hizi kuna zana nyingi ndogo ndogo mtu mmoja tu anakamata mwenyewe kimashine chake

kinakwenda kidogo kidogo analima. Kwa hivyo Mhe. Spika, sidhani kama bajeti hii imeweka sehemu hiyo ya kununulia vifaa vya aina hiyo vya kuwapa wakulima walimie kwa njia yoyote tutakayowapa, ikiwa tunawakopesha, ikiwa tutawagaia, ikiwa tutawaazima, lakini almuradi kuwe kuna vifaa ambavyo vitasaidia katika kilimo cha hivi sasa.

Lakini pili Mhe. Spika, humu katika kitabu kuna suala la umwagiliaji maji, mmetajwa humu Kibokwa, Ngweni. Mhe. Spika, hili mimi linanipa mashaka kwa sababu siku zote ikija bajeti umwagiliaji maji ni sehemu zile zile hazibadiliki. Kwa nini kila siku iwe umwagiliaji maji ni sehemu zile tu, hivi wananchi wengine walioko katika sehemu mbali mbali wao hawastahiki kumwagilia maji, nao wanastahiki kumwagilia maji kama wengine. Kwa sababu rasilimali ya nchi ni yetu sote, sasa kila siku kuwapa rasilimali watu hao hao wengine ukawaacha. Hivi tunadhani ndio tunatekeleza katiba?

Mhe. Spika, kutokuwa na mito inayopita si sababu ya watu kuwa wasimwagilie maji. Sio sababu kuwa tena mpaka pawe na mto Mwenyezi Mungu kaujaalia unapita pale iwe tena ndio watu wa pale wafanye kilimo cha umwagiliaji maji. Ata si sababu pahali popote hivi sasa unaweza ukamwagilia maji ukitaka, lakini Serikali bado haijataka. Mhe. Spika, hili jengine ilikuwa Serikali ilikuwa iingize katika bajeti hii, sehemu nyengine ambazo hazina mito lakini zina mabonde ya kulima basi nazo ziingiziwe katika bajeti hii sehemu ya kumwagilia maji.

Mhe. Spika, kuna suali zima la mifugo katika kilimo mpaka sasa hizo sehemu ambazo mifugo imepelekwa bado hazijatumiwa kwa kilimo. Kwa sababu Mhe. Spika, Pemba kuna ng'ombe wengi sana na ndio maana ikafika pahali ikawa wanasafirishwa kuletwa Unguja, haidhuru sasa hivi wanakatazwa lakini walikuwa wakisafirishwa tena kwa wingi tu. Sasa hiyo ni dalili kuwa kuna ng'ombe wengi sana.

Lakini hebu tujiulize ni pahali gani ambapo kinyesi cha ng'ombe kinakusanywa kikafanyiwa mbolea hakuna, kwa sababu kila mmoja haja zizi. Ng'ombe wanalazwa misituni huko huko wanakochungwa kila mmoja kwa hivyo leo kaweka hapa, kesho kaweka kule, keshokutwa anaweka kule kwa hivyo hakisaidii chochote. Je, wakulima wameelimishwa katika hilo kuanzisha mazizi wa ng'ombe wao ili kila siku kinyesi kikaanguka pale pale ili baada ya muda fulani wakapata mbolea ya kutosha wakaitumia kwenye kilimo, hilo limeelimishwa? Hivi hili ni kubwa la kuwa Serikali ishindwe kuwaelimisha wakulima kitu kidogo kama hicho.

Mimi ninavyojua katika kijiji changu watu kila siku wanawake asubuhi wanafyagia mavi katika vibanda vya kuku wanayatupa jaani. Hivi kweli

kinyesi hiki cha kuku kinachofyagiwa kila asubuhi haiwezekani kuelimishwa wananchi wakakikusanya pahali kikawasaidia kwa mbolea? Sasa mafunzo gani yanayotolewa.

Mhe. Spika, wakulima wanalima kwa shida mazao yanapatikana lakini hivi bajeti na Serikali kwa jumla ina mpango gani wa wakulima kunufaika na mazao yao, Mhe. Spika, huwa tumbo linaniuma ninapokwenda dukani hapo au sokoni nikakuta chana ya ndizi za pukusa chana moja ikiuzwa shilingi elfu mbili, elfu mbili mia tano. Wakati katika kijiji ninachokaa wanunuzi wa ndizi wanaonunua wakazileta huku ananunua mkungu mzima ulio na chana hizo za elfu mbili hapa kumi mpaka kumi na tano wananunua kwa shilingi elfu moja. Hivi kweli mkulima tumemsaidia kiasi gani mkungu ule anaouuza yeye kwa elfu moja, hapa utauzwa kwa shilingi elfu ishirini mpaka elfu ishirini na tano, tumemsaidia nini mkulima huyu. Je, Serikali hili inalijua, imeliona, imelifanyia kazi, bajeti hii ina *provision* gani kutafuta masoko ya bidhaa wanazozalisha wakulima ili kuwasaidia wakulima waweze kukimu maisha yao na waweze kuchangia katika pato la taifa.

Mhe. Spika, tumeambiwa kuna tafiti mbali mbali za maradhi zilizofanywa katika kitabu hiki lakini tafiti hizi nina wasiwasi kuwa zinamalizikia ofisini, kwa sababu bado sehemu nyingi tunazoishi vijijini kuna maradhi mbali mbali ya mimea wala hakuna tiba yoyote inayofanywa kila siku yanaongezeka kutoka shamba hii kuambukiza shamba nyengine. Je, hili nalo bajeti yetu imeliona? Je, kuna madawa ambayo yameshapangiwa ya kununuliwa ya kupita katika hayo maradhi yaliyofanyiwa utafiti? Je, madawa hayo yamepangwa yaenee nchi nzima au yamepangwa kwa kijiji fulani na kijiji fulani ndio yapelekwe madawa? Haya majibu yake bado hayamo katika bajeti yetu.

Mhe. Spika, hayo ni kwa upande wa kilimo. Lakini ukija kwa upande wa utalii Mhe. Spika, ambao bajeti hii inazungumzia miundombinu, katika miundombinu ya utalii Mhe. Spika, inawezekana ikawa hapa Unguja angalau imepiga hatua lakini kwa upande wa Pemba miundombinu haijapiga hatua pamoja na kuwa ziko shughuli za utalii hizo chache zilizooko.

Mhe. Spika, katika miundombinu ya utalii moja ni barabara na barabara sitaki niziseme zinajulikana maana nikisema nitataja Wambaa kwa sababu kuna hoteli nzuri yenye bei kubwa inaitwa Fundolagon. Hii ni hoteli bei zake ni za aina yake hathubutu mbeba nyumba yake mgongoni kwenda Fundolagon hata siku moja, ile ni hoteli wanakuja watu maalum, kila kitu wanafanya huko huko *booking*, kulipa na kila kitu akifika anakuja pale analala bangaloo moja dola elfu moja mia tano kwa siku, anakaa wiki, wiki mbili na watoto wake anastarehe, bei ndogo ni dola mia tano mpaka mia tatu.

Sasa Mhe. Spika, hoteli kama hii miundombinu yake ya barabara hamna asiyeijua katika Baraza hili hasa Mawaziri wanaijua kweli kweli. Napenda tu nimuarifu Mhe. Waziri kuwa pamoja na kazi nzuri iliyofanywa lakini imeharibika kwa pahali padogo tu. Kuna sehemu pale kwenye krosi kuna bonde huku hapa juu pamechafuka hapapitiki ukenda kidogo ukiingia bondeni huko tena salama aleikum haitoki tena gari. Mimi ninashukuru kila mkipita mkiona huwa ninashukuru kwa sababu huwa sisemi uongo mnayaona yale mambo. Kwa hivyo Mhe. Spika, miundombinu ya barabara kila siku tunaambiwa kuna barabara sita za Kusini Pemba na kwa mujibu wa kitabu hiki tunaambiwa kwamba zilikwama lakini sasa hivi zinaendelea, sijui kama zinaendelea au zinataka kuanza. Kwa sababu kama kuendelea ilikuwa ziwe zimeshaanza lakini nadhani katika hizi sita hakuna hata moja iliyoanza mpaka hivi sasa. Sasa labda tuambiwe tu zitaanza lini hizi barabara na itaanza ipi kwa mujibu wa umuhimu.

Lakini Mhe. Spika, jambo jengine miundombinu ya utalii ni taaluma, sasa katika suali la taaluma tunacho Chuo cha Utalii kinafundisha vijana lakini bado daraja yao wanayofundisha ingali ndogo na tunapiga makelele sana kwa ma-P.O. Lakini kuna kitu kimoja hatujakiangalia, hoteli zina daraja, daraja inaangalia mambo mengi ndani ya hoteli na moja katika linaloangaliwa ni huyo P.O. wa hoteli ana elimu ya kiasi gani? Ni moja katika linaloangaliwa katika daraja la hoteli.

Sasa ikiwa tuna watu wetu tumewafundisha lakini hatuna wenye digirii, mwenye hoteli anaweza akamuacha asimchukue hata kama ni hodari wa kazi, kwa sababu atamteremshia daraja yake ya hoteli. Kwa hivyo atatafuta mwengine wa nje mwenye digirii tena inawezekana ata asiwe mzuri kama yule wetu, lakini anakimbilia nini, kumpandishia daraja hoteli yake. Kwa hivyo katika mafunzo yetu tunayoyafanya basi lazima tujuwe tunahitaji ku-*train* watu katika madaraja ya juu ili waweze kuwa ma-P.O. katika mahoteli makubwa makubwa.

Mhe. Spika, suala la chakula sitaki hata nilitaje kwa sababu wengi wameshalizungumzia vyakula vya mahoteli. Kwa hivyo hiki kilimo kama tutakielekeza vizuri, ndio hapo tutapata vyakula vya mahoteli vitokee hapa hapa kwetu. Mhe. Spika, kwanza niache kidogo wakulima nirukie wafanyakazi.

Mhe. Spika, tuna wafanyakazi wetu wengi na wafanyakazi wetu kwa uoni wangu wanashindwa kuwa *committed* katika kazi kwa sababu ya kuwa kazi sio inayowaendesha, hilo ndio linalowafanya kidogo *commitment* yao ipuguwe kazi sio inayowaendesha. Inabidi mtu afanye kazi akisha aondoke kazini ende akafanye kazi nyengine, tumesema kuwa wafanyakazi wamepewa nyongeza, nyongeza ambayo itatolewa kwa awamu. Mhe. Spika, dhana yangu ninahisi kuwa tunawadhihaki wafanyakazi na mtu akae ajiulize ningekuwa mimi ndie

yule mfanyakazi wa Manispaa anayetoka asubuhi na kiberenge kupita akichukua taka walizozikusanya watu majumbani na mabarabarani, kweli kuongezewa pesa hii mimi ningeridhika? Kwa sababu unapomfanyia mwenzako kitu basi kwanza jiangalie wewe mwenyewe ujifananishe laiti mimi ningekuwa yeye je ingekuwaje?

Kwa hivyo Mhe. Spika, ukiachilia kwanza kuwa ni kidogo, lakini pia suali la kukigawa ukatoa nusu nusu pia lina matatizo yake. Hivi sasa hizo zilizotolewa huko nyuma za nyongeza kuna wengine mpaka leo hawajazipata, sijui kama Mhe. Waziri anajua habari hiyo au hajui. Sasa ikiwa yeye nyuma hajaipata na hizi zitakazotolewa kwa awamu mmoja si atapata awamu moja na mwengine atapata awamu nyengine, mimi nadhani hizi kwanza kama huko kutolewa basi zingetolewa kwa umoja. Halafu wakati huo huo ikawa kunafikiriwa awamu nyengine zitafutwe nyengine lakini si hizi tena. Nilikuwa ninafikiria hapa Mhe. Spika, kwa kuwa tunataka kutoa nyengine zihakikishwe hizo za nyuma kwanza kama wote wanaohusika wamepata waulizwe wafanyakazi.

Mhe. Spika: umebakisha dakika tatu.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe.Spika, dakika zako tatu naomba nizimalizie katika suala zima la mikarafuu.

Mhe. Spika katika suala la mikarafuu kama kilivyoeleza kitabu hiki cha bajeti kuwa kuna miche laki tatu iliyopandwa na kupewa watu waoteshe, naomba niitanabaishe Serikali, kuotesha miche ni kitu kimoja, kuipanda miche ni kitu kingene, kuishughulikia miche ni jambo jengine. Miche ikaota na ikadumu ni kitu chengine, unaweza ukawa na miche laki tatu ukaipanda na isiwe. Unaweza ukawa na miche mia tatu ukaipanda isiwe. Sasa ukitegemea tu kwamba nimetoa miche laki tatu, kwa hivyo mikarafuu mia tatu tayari imeshapandwa ipo utakuwa umekosea.

La kufanya nini nini? Hii miche laki tatu ulioitoa lazima uifuatilie mule ilimopandwa je imeota, je inashughulikiwa, itafikia mpaka wakati wa kuzaa, kama hujafanya utafiti huo wa ufatiliaji basi miche hii inawezekana ukawa umeitupa na ikawa miche hii ni kazi ya bure.

Lakini la mwisho katika hilo la mikarafuu Mhe. Spika, mimi linalishagaza mchuma karafuu kufundishwa kuchuma karafuu hili sijalipata mimi maana sisi tunavyojua uchumaji wa karafuu huko kwetu tunarithi tangu wadogo tunachuma karafuu mpaka wakubwa tunachuma karafuu. Lakini kubwa katika yote katika karafuu ni suala la mauzaji ya karafuu na bei za karafuu, Mhe. Spika, Serikali inawatia umasikini wachumaji karafuu na mashughulikiaji karafuu. Kwa sababu zinapoanza karafuu Serikali hutia bei kubwa, wakati ule

wanaoshughulikia karafuu ndio wakati wao wa kukodi,wanakodi mikarafuu kwa karafuu zilizomo kwa bei ile inayouziwa karafuu wakati ule.

Lakini Serikali huenda mpaka ikifika katikati ya msimu ikateremsha bei chini, sasa kodi waliotumia, pesa za matayarisho za kuchumia karafuu walizozitoa zote hazirudi hata moja. Wengine jamani huuza nyumba kwa kuchumia karafuu, nyumba imekwenda mtu hana kitu tena, Serikali inapata faida kutokana na karafuu, lakini mkulima wa karafuu anapata umaskini kutokana na karafuu. Na suala hili sijui litakwenda mpaka lini, kwa sababu huu ni mwaka haupungui wa tano hali kama hiyo kila mwaka inatokea. Wanavyoamini wenye mikarafuu na wachumaji karafuu kuwa Serikali inafanya makusudi kwa sababu karafuu nyingi ziko Pemba kwa hivyo Wapemba wale hasara kila mwaka.

Mhe. Spika, kwa hilo naomba nimalizie hapa. Ahsante.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Kwanza kabisa naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa na afya njema na salama.

Mhe. Spika, kwanza nianze kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake wote. Mhe. Spika, nimpongeza Afisa Mdhamini Wizara ya Fedha na Uchumi Pemba pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano mazuri na wananchi wa Pemba kwenye maslahi ya maendeleo.

Mhe. Spika, mimi katika bajeti hii nitazungumzia kuhusu ukulima wa mwani. Ukulima wa mwa ni kwa sababu wakulima wakuu ni wanawake. Mhe. Spika, kwa sababu mimi natoka Mkoa wa Kaskazini Pemba wamenituma wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Pemba nije niwatetee katika Serikali kwa sababu ya hali ya ukulima wa mwani ni hali dhaifu sana.

Mhe. Spika, sababu ya kusema hivyo ni kuwa wakulima wa mwani wanapata athari mbali mbali za ukulima wa mwani kwa sababu ni kwenye bahari. Mhe. Spika, athari zenyewe tunazijua kwa sababu kwenye bahari kuna athari mbali mbali, huwa mna mabocho na wanyama wengine ambao wanahatarisha maisha ya binaadamu. Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri na naiomba Serikali walizungumzia suala hili la kuhusu mapato na bei ilivyokuwa ndogo sana.

Mhe. Spika, nielekee kwenye kilimo, kwenye bajeti ya mwaka 2008/2009 ilizungumzia kuhusu ukulima wa *irrigation*. Kwa kweli kwenye Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba yalitajwa mabonde mbali mbali likiwemo bonde la Makwararani na mabonde mengineyo. Kwa sababu mabonde yale katika

kipindi cha mwaka 1984 yalitumika kwa *irrigation*, lakini ilikuwa Wizara ya Kilimo wanaajiriwa wananchi ili kushughulikia mabonde yale.

Mhe. Spika, sasa wananchi wamejenga hofu kubwa kwa sababu mabonde yale waligaiwa na kulima kwa ajili ya kujipatia vipato vyoa binafsi, sasa hivi wamesikia hivyo wana hofu kubwa kama maeneo yale watanyang'anywa. Ninamuomba Mhe. Waziri atoe taaluma zaidi kuwafahamisha wananchi ili wasiwe na wote na wakae kwa kujipanga kwa ajili ya maslahi yao.

Mhe. Spika, nielekee Mkoa wa Kaskazini Pemba katika Wilaya ya Micheweni, kwa sababu Wilaya ya Micheweni kuna jengo la *Rest house.* Ninamuomba Mhe. Waziri jengo lile alifanyie utafiti ili limalize, kwa sababu wananchi wa Mkoa Kaskazini Pemba hususan Wilaya ya Micheweni na wao huwa wanataka wazungumze na viongozi wao wa Chama na Serikali kwa maslahi yao. Sasa ninamuomba Mhe. Waziri suala hili alifatilie iwezekanavyo ili na sisi tupate faraja wananchi wa Mkoa Kaskazini Pemba hususan Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Spika, kwa sababu mchango wangu si mkubwa mimi pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba ninaiunga mkono bajeti hii mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi kwanza ninachukua nafasi hii kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuweza kusimama hapa na kutoa mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani. Aisha ninachukua nafasi hii pia kukushukuru kwa kunipatia nafasi mchana huu ili niweze kutoa kwa kadri nilivyojiandaa. Na katika hilo Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kutoa salamu za pole kwa wenzetu waliotangulia, Mhe. Daud Hassan Daud na Mhe. Soud Yussuf Mgeni, lakini salamu za pole za pekee nitoe kwa wananchi waliopata ajali kwa meli ya MV Fatih na Pemba.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kusudi kwa sababu katika boti iliyoungua kule Tanga, wananchi wangu wa Jimbo la Kiwani walihusika sana, nilibahatika maiti wasiopungua watatu, nikapata majeruhi wasiopungua 15 na ndio ambao walioniwezesha kufanya utafiti mdogo kuona jinsi gani Serikali ilishiriki katika msiba ule.

Mhe. Spika, nilifanya utafiti ule kusudi kwa sababu sikuuona mchango wa Serikali wakati boti ile inapata ajali zaidi ya Mhe. Hamza kwenda kushuhudia maiti kule Mombasa. Jambo ambalo Mhe. Spika, mimi sikutarajia kuwa hivyo kwa sababu angalau Serikali ingeamua kuunda Tume na kuona kwamba ajali ile imetokana na nini, kuliko kwenda kuangalia maiti waliopatikana na kujua idadi yake.

Mhe. Spika, kama Serikali itahitaji kupata maelezo ya ajali ile basi ninawakaribisha ndani ya Jimbo la Kiwani waje wawaangalie majeruhi walioko na watawapa kwa undani kabisa nini kilitokezea na kwa nini ajali ile imetokezea.

Mhe. Spika, sasa nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye bajeti hii, nataka niseme kwamba kama ningeshawishika kuunga mkono bajeti hii basi ni kuhusu miradi midogo midogo. Lakini kutokana na udhaifu uliopo ninashindwa na sitoweza kabisa kuunga mkono bajeti hii kutokana na sababu nitakazozitoa.

Mhe. Spika, kama utakumbuka mwezi wa pili ulitutuma kamati zako kwenda katika mawizara mbali mbali, mimi nikiwa mjumbe wa P.A.C. niliungana na wenzangu kwenda Wizara ya Fedha. Na nikiwa kama mjumbe ndani ya kamati yangu niliitoa hoja hii kwamba miradi midogo midogo kwa kiasi kikubwa haiwafikii wananchi. Na nikasema kwamba miradi hii imekuwa ni chaka la wakubwa kula pesa, niliyasema hayo mbele ya Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na nikayasema hayo mbele ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Kwa hivyo mimi mategemeo yangu, yale yalikuwa ni maoni yangu lakini mbele ya kamati kwa hivyo ni maoni ya kamati kwa sababu wenzangu waliunga mkono na kwa bahati mbaya sikupata mtu kunifuata kunambia nitoe ufafanuzi.

La kusikitisha ni kwamba baadhi ya watendaji waliumwa na kauli yangu ile na walikwenda jimboni kwangu wakasema kwamba Mwakilishi wenu amezuia fedha zisiletwe. Nakataa mbele ye Baraza kwamba sijazuia fedha isiletwe, nilichozuia fedha za wananchi kuliwa na kama hilo ni kosa basi ninakubali kosa. Lakini kama si kosa Dr. Mwinyi anasema kwamba hii ndio hali ilivyo pesa hizi hatuwezi kuzipitisha hapa baadae zikenda kwenye mikono ya watu wachache. Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani hajakataa fedha kupelekwa kwa wananchi wa Jimbo la Kiwani. Amekataa fedha kupelekwa kwa wananchi wa Jimbo la Kiwani nusu nusu nyengine zikenda kwenye mikono ya watu.

Mhe. Spika, utafiti nilioufanya asilimia ishirini ya fedha hizi haziwafiki walengwa. Na kwa maana hiyo shilingi milioni mbili na nusu ambazo zinazotolewa kwa mradi fulani wananchi wanapata milioni mbili, laki tano zinakwenda kwenye mfuko wa watu kwa kisingizio kwamba kuna watu wametumika. Nani aliyetumika kama si Mwakilishi, mimi nina barua zaidi ya kumi pale. Kwa hivyo mimi niliwakopa zile pesa kama kulikuwa na mtu alitumika. Kwa hivyo hii fedha haifiki kwa wananchi na kwa sababu hiyo ninawashashika kabisa kutounga mkono hotuba ya Mhe. Waziri mpaka nipate maelezo.

Maelezo hayana kificho, fanya utafiti Skuli ya Mtangani Mwalimu Mkuu akazungumza mbele ya Kamati kwamba Mwakilishi kazuia fedha, kapata wapi

Katibu Mkuu atatusaidia kwa sababu mimi niliyasema mbele ya kamati. Sijazuia fedha za wananchi ninakataa kwa nguvu zangu zote wananchi kutumia kivuli kuliwa fedha zao. Mhe. Spika, Dr. Mwinyi akiyataka namwambia aanzie skuli ya Mtangani atayapata na mimi siungi mkono fedha hizi kupelekwa nusu nusu kwa kisingizio cha watu ndani ya miradi hii.

Na kwa maaana hiyo basi milioni hizi ambazo mara hii umezitenga ninamuunga mkono moja kwa moja Mhe. Ali Abdalla kwamba fedha hizi zigaiwe kulingana na majimbo. Kila jimbo wapewe milioni zao kumi na vyenginevyo itakuwa pesa hizo hazifiki. Mhe. Spika, ikiwa hivyo ndivyo, ikiwa milioni mia tatu sitini mimi naamini kwamba asilimia ishirini ni shilingi milioni sabiini na mbili. Ninaamini kabisa shilingi milioni sabiini na mbili hazitowafika walengwa.

Kwa utaratibu huu na kwa maana hiyo ikiwa utafatwa utaratibu huu maana yake milioni mia tano zilizotengwa, milioni mia moja zitaingia mikononi mwa watu. Kwa hivyo njia pekee ya kuwafika walengwa ni kwamba fedha hizi zigawiwe kwa majimbo kila mtu ajuwe milioni ngapi zipo na asubiri mgao wake. Mhe. Waziri Dr. Mwinyi nakuomba hili ulifanyie utafiti, kwa sababu ndani ya Wizara yako kuna watendaji wazuri sana, hatuwezi kwenda pale tukamkabidhi Dr. Hikman miradi mingi akafanya bidii akatupatia miradi baadae fedha isifike kwa walengwa. Mimi kama mwakilishi wa Jimbo la Kiwani ninalikataa na kama hili ni kosa nakubali kosa lakini nakataa kwa nguvu zangu zote.

Mhe. Spika, jengine kutoka hapo niende kwenye miradi ya barabara. Mhe. Waziri ametwambia kwamba bajeti hii ni bajeti ya miundombinu na nilipoangalia mpango wa utekelezaji nimeona kwamba barabara ya Mgagadu/Kiwani ilitengewa milioni 300,000,000 mwaka jana. Na nikashauri kabisa kabisa ikiwa haiwezekani basi si bora hii barabara tukaiwacha.

Kwa hivyo milioni 300,000,000 kwa mwaka jana alizozitenga Dr. Mwinyi Mhe. Waziri mara hii umenambia kwamba asilimia 72 fedha umezitoa, maana yake ni milioni 214,677,000 mimi sijaziona naomba unifahamishe zinatolewa wapi? Ziko benki? Ziko mikononi kwa mtu au kazi gani Kiwani imefanywa kufikia asilimia 72.

Mhe. Spika, wananchi wa Kiwani wamenambia nije niseme kwamba fedha hizi zimetolewa kwa kazi gani ni uchambuzi yakinifu, au ziko mikononi kwa mtu? Naomba maelezo hayo.

Mhe. Spika, lakini jengine kama hilo halitoshi ni kwamba barabara 5 za Kusini Pemba, Mhe. Spika, nadhani Serikali ifahamu kwamba kuna baadhi ya watu

wanatumia msitu huu kama siasa. Mimi sijapa kuona kabisa kabisa kwamba barabara ambao tayari mjenzi wake yupo ni NORAD lakini wanaambiwa wananchi watapatiwa ajira kila barabara wananchi 2000. Labda mara hii itaanzia Pemba lakini nina hakika kwa barabara ya Fumba haikutokezea hivyo.

Mhe. Spika, wananchi wa Kiwani, Mwambe, Kengeja, Mtambile zaidi ya 500 wameandikwa barabara ya Mtambile/Kengeja lakini ili uandikishwe basi utoe kipande chako cha uraia. Na kama Mhe. Waziri wa Mawasiliano atakumbuka nilimpigia siku nikamwambia naomba kazi watu watatu, akanambia hii kazi ina kampuni bwana. Lakini huku kuna watu wamechukua vipande zaidi 3000 kwamba watapatiwa ajira. Mhe. Waziri nilikuwa na maana hiyo kwamba ungenambia lete kipande chako basi ningejua kuwa kuna ajira, wananchi wanahitaji kupata hii ni haki yao na si jambo la siasa kabisa.

Kwa hivyo Dr. Mwinyi ikiwa kweli NORAD wanataka ajira watu 3000 kwa barabara zile na pengine barabara hiyo kuna teknolojia mpya ya kujenga kwa mkono, basi tuambiwe kwamba kweli NORAD wameagiza Wapemba watoe vipande vyao ili barabara ijengwe kwa njia ya mkono. Vyenginevyo itakuwa Mhe. Waziri wananchi wanatumiwa isivyo halali.

Mhe. Spika, nikitoka hapo sasa nije kwenye suala zima la MKUZA ambapo Mhe. Waziri kwenye bajeti yake ametwambia kwamba MKUZA umeleta mafanikio. Mafanikio ambayo kwa kweli kwa mimi ambaye niliyekuwa si mtaalam wa uchumi ninahitaji ufafanuzi wa kina. Katika kila sehemu ya MKUZA tuelewe kwamba kuna *technical waorking group* na hizi ndizo ambazo zinahitaji kufanya kazi mapema ili kufanikisha MKUZA.

Lakini taarifa ambazo tunazo ni kwamba vikao vya makundi haya nilivifanya tarehe kumi na tarehe kumi na mbili Juni wakati MKUZA unamalizika, tutegemee mafunzo ya wataalam hawa yangefanywa mwanzo ili wakatekeleza huo MKUZA, lakini MKUZA unamalizika ndio wanafanya mafunzo. Mhe. Spika, ikiwa hivi ni kweli naomba unisaidie MKUZA huu tutaupima vipi.

Lakini jengine inaonekana kwamba utaalam ni mdogo sambamba na fedha, upatikanaji wa fedha unakuwa mchache na ndio unaowafanya wataalam wetu wasiweze kufanya utafiti na kujipanga vyema.

Mhe. Spika, nikitoka hapo sasa naomba Mhe. Waziri anisaidie nimejaribu kuchambua vitabu nimeona kwamba karafuu imetengewa milioni 60 kwenye bajeti, lakini elimu kwa wakulima ni milioni 30, upandishaji wa ng'ombe wa maziwa kwa sindano ni milioni 40. Lakini hadhari kwa ajili ya kichaa cha mbwa ni milioni 430, sasa mkarafuu ndio uti wa mgongo, milioni 60, lakini athari za kuhofia kichaa cha mbwa milioni 430. Kwa kweli ni kichekesho

kikubwa sana, nadhani hapa kipaumbele hakikuzingatiwa. Kuna watu wengine huhofia mchawi wakaanza kufuga shetani. Ndio maana yake hiyo kwamba unahofia mchawi umekwenda kuchukua jinni, mimi nadhani hiyo sio sahihi.

Mimi nadhani kwamba elimu kwa wakulima, kilimo, mikarafuu na ng'ombe wa sindano ni fedha nyingi zaidi kuliko athari kwa wasi wasi wa kichaa cha mbwa. Wasi wasi wangu ni kwamba hizi fedha zitaingia kwenye mikono ya watu, kwa sababu mtu akikwambia kuna Mbwa Kojani mtapeleka pesa ndio maana yake. Sasa Mhe. Spika, hili siungi mkono nasema kwamba lirekebishwe.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba mapato ya serikali. Mhe. Waziri amejaribu kutuonyesha kwamba vyanzo vya mapato vitaimarishwa, lakini sambamba na usimamizi wa mapato ya serikali, mimi Mhe. Spika, nimekuwa nikishangaa sana kwamba kwa mfano mwaka jana PAC imesema kwamba kwa mujibu wa ripoti ya mkaguzi, ZRB wameshindwa kupata mapato kwenye VERA Club Hotel. Sasa sikuona msimamo wa serikali hadi hii leo. Mpango huu wa upotevu wa mapato ya serikali utasimamiwaje na hivyo nashindwa kuamini kwamba mapato ya serikali yataendelea kupotea na haya malengo ya serikali ya kukusanya mapato haya, basi bado yanaendelea kupotea na hayapatikani.

Kwa hivyo ushauri wangu Mhe. Spika, ni kwamba kila penye mwanya wa mapato ya serikali nadhani serikali ijipange vizuri na kudhibiti upotevu huu.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningependa kuligusia ni suala zima la uwekezaji. Wataalam wametwambia kwamba uwekezaji wa ndani wa Zanzibar ni 12%, lakini uwekezaji wa nje ni 88%, sasa ikiwa ndio hivyo nadhani serikali ingejitahidi ikajipanga na hii sehemu ya asilimia kubwa ya uwekezaji wa ndani ikaongezeka ili kusaidia mapato na kupata ajira kwa wananchi wetu, suala la upotevu ni suala la umma, lakini inaonekana kwamba kuna *private marine preservation area* na kama hivyo ndivyo maana yake sio sahihi. Duniani kote masuala haya ya hifadhi za fukwe ni mali ya umma, lakini inaelekea Zanzibar watu wanamilikishwa sasa inakuwa ni jambo gumu kwa wananchi kuona haki yao inamilikishwa mtu.

Jengine ambalo ningeomba nichangie ni kwamba tunaambiwa Zanzibar ni *Spice Island,* lakini la kushangaza hata pili pili hoho tunaagizia Tanzania Bara, sasa nadhani tungelijipanga tukaifanya Zanzibar kuwa *spice Island* kuliko kuagizia kila kitu kutoka Tanzania Bara.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetarajia bajeti hii kupunguzwa na kiukweli mimi sielezi ikiwa Dk. Mwinyihaji hakutwambia suala la mafuta, hakuna chanzo kizuri kwa mapato Zanzibar kama sio mafuta. Sasa kwa nini serikali iweke kigugumizi tunamsubiri Mhe. Mansour aje atwambie hii ndio bajeti ya

serikali, bajeti ilikuwa itwambie nini mpango wa mafuta. Sasa mimi Dk. Mwinyihaji nadhani ujisahihishe kwa hilo na niambiwe kwamba mafuta mpango wetu ni huu na tunategemea kupata nini japokuwa tunaambiwa hakuna, sasa tuambiwe nini lengo la serikali kwenye mafuta vyenginevyo sitounga mkono bajeti hii.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ningetaka ufafanuzi ni suala la msuko suko wa kiuchumi takwimu kidogo imenicheza hapa tumeambiwa kwamba uchumi wa dunia utashuka kwa 1.3%, lakini uchumi wa nchi ambazo zimeendela ni kwa 3.2% na nchi ambazo zinaendelea zetu sisi 100.6%. Kidogo hii naona kinyume nyume, wale matajiri uchumi wao ni 3.2% sisi ingawa si vizuri kusema omba omba lakini 1.6% naomba unisaidie ni takwimu sahihi au nimechanganya.

Jengine ambalo nataka nichangie ni suala zima la mfumko wa bei kwa mujibu wa bajeti ya serikali ya juzi mfumko wa bei Zanzibar ni 20.6%, lakini nilipochungulia vitabu vya BOT wanatwambia ni 24% sasa ipi sahihi, wakati BOT ndio mshauri wa uchumi wa serikali hizi mbili.

Mhe. Spika, sasa nakuja kwenye ongezeko la mishahara mimi ninao ushahidi kwamba nyongeza tokea Rais alivyozungumza Pemba mwaka jana katika shehere za Mei mosi mpaka leo, kuna watu hawajapata nyongeza ile. Sasa ukinambia kwamba kuna nyongeza ya awamu mimi nafananisha bajeti hii sawa sawa na Deci ndio upatu, kwa sababu nyongeza ya mwaka jana haijapatina mpaka hii leo, na leo Mhe. Waziri anatwambia anaongeza mwezi wa kumi na mwezi wa Januari, huo ni mzaha. Nadhani hii ni Deci ndogo ya Zanzibar. Sasa ikiwa hivyo sivyo, basi Mhe. Waziri jipange kwa nafasi yako wafanyakazi uwaongezee mshahara siku moja na wakati mmoja na wala isiwe shilingi elfu ishirini, kwa nini wakati mapato yapo isiwe laki moja na nusu. Kwa nini tunaambiwa mapato yamepanda, lakini wafanyakazi hawapati hayo mapato bahati mbaya mara hii hata wale wazee hukuwataja, mwaka jana tuligombana hapa ukataka shilingi elfu tano nikawa mkali sana kwamba uwape elfu kumi na tano, basi mara hii hukuwataja hasa, nataka unieleze wazee shilingi ngapi umewaongezea.

Mhe. Spika: bado dakika tano.

Mhe. Hijja Hassan Hijja: Mhe. Spika, kwa kuwa dakika zimebakia kidogo niseme kwamba wataalam wanatwambia kwamba pato la taifa na pato la mtu hupimwa kwa njia tatu, kuna *production approach na income approach* sasa nataka utwambie Zanzibar mnatumia nini, ili kujua kwamba mapato yamepanda mnatumia nini katika njia tatu maana mimi siioni kabisa.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba sitoridhika na wala siridhiki kwa miradi midogo midogo kupelekwa kwa watendaji moja kwa moja na badala yake rai pekee ya kuamua suala hili ni kila jimbo litengewe fedha yake, pamoja na Mhe. Waziri kutoa kauli kwamba mimi sikusema fedha zipelekwe Kiwani, lakini fedha inaliwa na ushahidi ukitaka nitakupa upo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi angalau kuzungumza machache juu ya bajeti hii ya serikali, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine kukutana ndani ya Baraza lako tukufu kwa mnasaba wa mjadala wa bajeti ya serikali inayolenga hatma ya wananchi wetu kwa mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako mimi naomba nianzie pale alipopataja Mheshimiwa aliyemaliza hivi punde, suala la mafuta hili limetugharimu muda mrefu hapa ndani ya baraza hili, suala la mafuta wananchi wa Zanzibar walikuwa na hofu kwa maamuzi yaliyotolewa hapa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu tukawarejeshea matumaini makubwa na hasa pale waheshimiwa wawakilishi walipoiomba serikali basi, baada ya maamuzi yale ambayo kila mmoja wetu aliyakubali tena kwa njia ya kura moja mtu mmoja. Wananchi wamerudi kutuuliza mbona sasa mnatafuna maneno juu ya suala hili, matarajio yetu Ndugu yetu Dk. Mwinyihaji Makame angekonga nyoyo za wananchi wetu kama angezungumza angalau kidogo juu ya suala hili. Mhe. Spika, hapo napaachia.

Mhe. Spika, jengine ni zao la biashara nje na ndani ya nchi bado karafuu ni tegemeo letu pamoja na kwamba utalii leo ni sekta kiongozi pamoja na mapungufu makubwa yaliyopo. Leo sio siku yake ya utalii, lakini kwa sababu ni vichocheo vya mapato yetu tutatumia neno lile alilolitaja mama yangu jana Mhe. Mkongwe Nassor Juma tutarashia rashia alimradi paeleweke tunachokizungumza ni nini. Pamoja na wengi waliolitaja zao la karafuu kwamba limebezwa na serikali ya Mapinduzi wazalishaji wa karafuu wanaendelea kukatishwa tamaa na mtindo huu wa serikali kulibeza zao hili.

Hali kadhalika suala la mwani ambao ni ajira kuu kwa akina mama hasa vijijini bado hapajatolewa nguvu za makusudi kwa bei angalau kupandishwa ile morari za watu wetu juu ya zao hili.

Mhe. Spika, sasa nije biashara Zanzibar kama wenyewe tutaendelea kubaki hivi tulivyobaki ile ndoto ya muda mrefu tuliyoirithi *centre of the trade of East and Central* itabaki kuwa historia, waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tukufu kupitia kiti chako Mhe. Spika, nadhani wakati umefika sasa kurejesha heshima

ya Zanzibar na Wazanzibar wake juu ya suala zima la biashara hii ni haki yetu, hii ni heshima ya nchi yetu sasa kuilevya levya hivi tunavyofanya mpaka sasa wafanya biashara wanatukimbia si kwa sababu wameshindwa na uzalendo, lakini kwa sababu wenyewe tumeridhia hili litukute. Matokeo yake ndani ya Zanzibar leo hali yetu ya maisha imekuwa mbaya mbaya sana, hali ya maisha ya wananchi wetu ni duni mno, lakini haya tunayachangia sisi wenyewe kama viongozi.

Mhe. Spika, mimi nauliza hasa kigugumizi kiko wapi hasa kuiambia serikali ya Muungano kwamba hivi hatutaki na tunataka hivi juu ya hali hii, mimi sioni kwamba watatupiga mabomu, sidhani hata kidogo kwa sababu popote penye nia njema kwanza ukweli hutawala, sasa hii mvungu mvungu hii kila kitu sasa kapu imewekwa ni kero yanayoanguka pale ni basi hayaulizwi tena. Mhe. Spika, nchi tunaipeleka pabaya nimeshasema na mwaka huu narudia kusema mimi Asaa ishaala kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hatoniuliza tena kwa jambo hili, nasema serikali inakuwa kiziwi, haitaki kusikia kwa nini mimi nasema kwa niaba ya watu sisemi kama Asaa, hawa watu wanatupotezea uchumi wetu, biashara Zanzibar haipo anayetaka ni hivyo na asiyetaka ni hivyo. Professor kasema pale wale wenye macho hawataki kuona, wenye masikio hawataki kusikia tunasema Zanzibar kufa kwake kibiashara ni muundo mbaya wa muungano tulionao, suala ni kukaa tukarekebisha muundo ili na sisi tuwe na afueni kuhusu suala la biashara. Kigugumizi hapa kinatokea wapi hii kukaa tukazungumzia kero zilizokuwa hazina ufumbuzi za nini. Tunapoteza muda wetu wote huku watu wetu wanateketea sasa hili ni kuamua baada ya kuendelea na kero kila asubuhi kero zinazuka, kwa sababu hazipatiwi ufumbuzi hatimae zitakuwa nyingi kuliko yale ya msingi.

Mhe. Spika, sasa mapitio ya uchumi wetu tumeyaona ni vipi yameanguka duniani na yataanguka hapa kwetu Afrika itashuka mpaka asilimia mbili, kutoka 5.2 ni vipi tumejipanga bajeti haikusema kukabiliana na hali hiyo, lakini kuna ongezeko la uchumi kupitia sekta hii ya huduma hasa usafirishaji. Lakini hata mambo haya ambayo tunaona ndio yanayotusaidia mbona anayaweka lege lege usafirishaji ni kweli unatusaidia uchumi wetu, lakini matokeo tunayaona wenyewe hatimae yanatusuta hukithamini hata kinachokusaidia ni vipi. Sekta ya usafirishaji nayo sasa imeshakumbwa na wimbi, biashara imeshakumbwa na wimbi kubwa.

Mhe. Spika, suala la VAT itaua kila kitu inamuanza yule mlaji ndio anayelemewa na mzigo wote anayetoka Unguja kwenda Pemba, anayetoka Unguja kwenda Dar es Salaam anayepanda ndege bandarini ndio lango kuu la wengi wanakotumia huko VAT ipo, VAT hii wenzangu wameshaizungumza haikuwa ya lazima hapa kwa sababu tuna ZRB yetu ina ufanisi mkubwa wa kutukusanyia mapato yetu lazima VAT. Hivi anayetwambia lazima VAT

hatuwezi kumjibu sio lazima hapa ni kwetu jamani, hivyo kwa nini kuwe na mtu anatushikilia hivi hatukiamini chombo chetu, kina mapungufu na kama kuna mapungufu tuyaondoe ni chetu wenyewe waweze kufanya kazi inavyostahiki. Natumia neno hili tunaimba *Good Governance* kwanza tutaipata humu kuweka mambo yetu *very transparent* kwenda kwenye utawala bora ndio hapo. Kuwa na uwazi katika masuala yetu lakini kuwe na ukweli hali kadhalika *Good Govevrnance* haitabaki kwa kuisema, lazima tu-*practice* leo tunashindwa hata kumwambia mwenzio mimi unaniathiri jamani hiyo haiwezekani.

Juzi mwenzi wa Mei kama sikosei nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki zilikutana Rwanda tuliyoipokea juzi, Burundi na hizi wanachama ikazungumziwa pia suala la ongezeko la thamani mambo ya kodi na mengineyo ZRB haikualikwa tunayo hapa, haikualikwa tukiuliza kwa nini labda Mhe. Waziri aje ajibu, lakini mimi sitopenda ukijibu tumewakilishwa hii kuwakilishwa kuna wakati wake na mahali pake, kutokuwakilishwa madhara yake ni haya. Kwa sababu ya kuwakilishwa imetoka ishirini mpaka kumi na nane wenzetu wana sababu zao, hatukuwakilishwa ina maana hatukupata kuchangia chochote pale sasa huo uwakilishwaji tunaoendelea kuudai hao wenzetu hawana nia njema, wenzetu wanalijua na watu wazima matokeo ndio haya hapa tumeshajipanga tulivyojipanga, lakini VAT ipo ishirini Zanzibar wenzetu wako kumi na nane, wafanya biashara wataelekea wapi *automatical* wanaelekea zao Bara.

Makontena tunayohisabu hapo tutoe hivi sasa wala sio kesho, lakini hicho kitakachokuja hao ambao wataumwa na uzalendo kupita kiasi walete bidhaa zao mlaji atamudu, na kila kinacholetwa kina VAT ndani yake nilimshauri ndugu yangu na leo natoa tena ushauri wa bure. Mhe. Waziri Kiongozi masuala haya mnayakalia kitako na wenzako, lakini ukipanda ndege ukirudi msimamo uko pale pale, sasa tuamueni wala huna haja ya kwenda tuamue tufanye yetu wenyewe ambayo yamo ndani ya mikono yetu kwa faida na maslahi ya nchi hii, vyenginevyo kutaka ruksa kutatupeleka pabaya hali itakuwa mbaya zaidi.

Mhe. Spika, nadhani tulifanya kosa sijui ni jazba ama ni kuamini kupita kiasi tulipomuaga mama aliyetuzaa, akatulea tukasema Afro mama tunakuaga sikama umetufanyia baya kwa heshima na taazima muungano kwetu ni usawa Afro. Mama kapewa mafungu matatu hana baya alilotufanyia ati tunamuaga kenda afanye nini sisi tuko wengi mama ni mmoja aliyetuzaa, sasa tunaona tunayoyapata. Sasa hapa mama ana huruma kwa kawaida nadhani tukirudi atatupokea nina hakika tukirudi atatupokea na tutanyonya kwa mama yetu na mazuri tutapata na radhi Mwenyezi Mungu ataifuta kwa sababu tumerudi, tutii kwamba haidhuru hatukuona ni kosa siku hiyo, lakini leo ndio tunaliona kumbe lilikuwa kosa hii ni dhana yangu Mhe. Spika, kufuatana na taasisi nzima mama

aliambiwa kaa pembeni tuna yetu tunataka kuyafanya na ikawa mlango uko wazi yamefika haya yaliyofika.

Mhe. Spika, VAT izungumzwe upya na mazungumzo yake Mhe. Waziri ni ZRB kupewa madaraka ya masuala yote ya makusanyo hili ndilo suluhisho kwa sababu hatukuanza nayo tokea pale Mzee Karume, kwani kuiambia basi tulikuwa hatujajua sasa hivi tumeshajua, tuliambia tumesoma hatukujua, lakini tumejifunza tumeelewa sasa kuna lipi.

Mhe. Spika, JFC ilikuwa ni matumaini makubwa ya pande zote mbili naamini hata wazo la kuambiwa tumuage mama yetu halikutoka kwa wote walioko upande wa pili, ni wale wachache walio na dhamira zao wako ambao wana nia njema hii ndio imani yangu, kwa sababu hiyo kilionekana chombo hiki kitasaidia pande zote mbili, mimi na wenzangu Kamati ya Uchumi na Fedha tulifika Dar es Salaam Makao Makuu tuliyokutana nayo ni *Secretariat* kurugenzi yote haipo. Kurugenzi ile ile inapohitajika na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kamati inasafiri wenyewe na kwenda Dodoma, mimi nilimwambia mwenyekiti wangu hichi chombo ni chetu sote leo, hapa sema watufuate Zanzibar sisi tunakaa mwezi wa sita waje tuzungumze nao. Yeye mwenyewe jana alisema dhana ya kutaka waje hapa aliitaja mimi sitaki kuirudia, lakini kile chombo ni cha muungano tupime tena hapa hata salamu kwamba tutakuja au hatuji hazijaletwa mpaka leo, chombo ni chetu kimezuiwa na nini kuna sababu gani hata wasije.

Mhe. Spika, pamoja na mengi tuliyoyazungumza tumekwenda BOT tukizingatia tulikuwa na agenda kubwa ya VAT, lakini tukawataka wenzetu watupe baadhi ya mambo waje wafundishe hapa kwa wajumbe wote wa Baraza na masuala tuliyouliza tukaambiwa yataletwa kwa maandishi, hadi asubuhi hii namuuliza mwenyekiti ananambia bado hajapata lolote mengine ni dharau kama sio kejeli. Hii ni dharau ya wazi chombo ni chetu sote au waseme kwa sababu masuala niliyouliza ya msingi mengine ni hayo kutaka kujua Wazanzibari hisa ilikuwepo ya kuanzisha au hapana. Niliuliza hili moja katika maswali 11 niliyouliza, nalo linaelekezwa kule kule kwamba aende Waziri Kiongozi akae na mwenzake mimi nikakataa *on the spot* kwa sababu ndio chinjio, chinjio zinakuwa zile kero. Makero ya msingi hivi Wazanzibari kwani hatuyajui? Haya ni kero kwa sababu ni mambo tu ya kusema hili la huku na hili la kule kwanini yatiwe kwenye kapu la kero.

Mhe. Spika, mimi nasema kwa sababu zana iliyokusudiwa *JFC* haipo na kwa makusudi haitakiwi iwepo wajumbe wa Zanzibar wajiuzulu wote haina faida yoyote. Tukae tuje tupange vyenginevyo kuinyanyua Zanzibar na suala zima la uchumi wetu.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia kidogo katika hotuba hii ya Makadirio na Mapato ya Serikali.

Mhe. Spika, nitakuwa na mchango mdogo tu, lakini kwanza nianze na vijiswali vidogo vidogo. Katika ukurasa wa 14 kifungu cha 23 mstari wa pili kutoka chini ulioanzia na sentensi ya serikali unasema kwamba, "serikali itahakikisha madeni yanalipwa wakati yanapoiva kwa utaratibu uliopo". Hayo ni madeni ya nje. Shilingi 60 milioni zimedhaminiwa na Serikali ya Muungano na shilingi milioni ishirini na nusu hazina mdhamini, hizi hazikudhaminiwa na Zanzibar wala sehemu yoyote. Katika kuona kwamba tunalipa madeni hayo kama serikali ilivyosema kwamba itahakikisha madeni yanalipwa wakati yanapoiva kwa utaratibu uliopo.

(a) Nikitaka kujua ni utaratibu gani ambao serikali itatumia kuweza kuona madeni haya yanalipwa?

(b) ni wakati gani ukifika madeni hayo yatajulikana kuwa yameiva? Na tunaposema madeni yakiiva huwa yanaiva vipi?

Mhe. Spika, swali la pili linakuja katika ukurasa wa 52 kifungu cha 97 ambacho wenzangu walizungumzia sana kwa ufafanuzi mzuri sana. Lakini sentensi inasema "kwa mara ya kwanza katika mwaka ujao wa fedha 2009/2010, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafaidika kupata asilimia 4.5 ya msaada wa kibajeti kutokana na mkopo wa GBSLON, tokea kuanza Tanzania kufaidika na mikopo hiyo mwaka 2003/2004. Ninataka kujua katika kipindi hicho mpaka tuanze kufaidika hivi keshokutwa hapa katikati palikuwa na nini tulipokuwa hatukufaidika napo? Pengine nitapewa ufafanuzi sitaki kuendelea.

Mhe. Spika, nianze na mchango wangu wa bajeti nije katika ukurasa wa 30 kwenye miradi midogo midogo. Dhana ya miradi midogo midogo ni kuoanisha nguvu za serikali na nguvu za wananchi katika kuibua miradi katika maeneo yao. Lakini dhana hii Mhe. Spika, inatufikisha pahala sisi wengine tusiwe na imani na kinachofanywa na serikali.

Mhe. Hija Hassan Hija amezungumza kwa ufasaha kabisa na kwa ukweli wa mambo. Lakini dhana hii vile vile inatuchonganisha, kwa maana ya kwamba wengine wanapata na wengine hawapati, wengine wanapewa na wengine hawapewi. Zaidi ya wanaopata utakuta mtu anaweza akapata mara mbili au tatu mwenzake hajapata, sasa moyo una sehemu, una wivu, tumechoka kutukanwa majimboni Mhe. Spika.

Mhe. Mwakilishi akionekana kwenye televisheni kwenye mradi fulani wewe utaulizwa sisi wawakilishi hatuna mbona hatuwaoni kufanya hivyo? Lakini lugha inayotumika pale siijui ni lugha gani kama ndio ile ya 2.5 milioni, tano zikenda kwa watu waliofanya kazi sijui, isipokuwa utaratibu huu kwa kweli haufai.

Jana niliambiwa Mhe. Ali Abdalla Ali amelizungumza suala hili kwa vizuri kabisa, kwa bahati mbaya jana sikuwepo alipokuwa anazungumza, lakini ametoa ufafanuzi mzuri na jinsi gani serikali ifanye ili kuhakikisha kwamba sote tunafaidika na miradi midogo midogo, wengine tuna miaka 10 wengine 15 katika Baraza hili, lakini hata kipindi kimoja hawajanufaika na miradi hii. Sasa hilo kwa utaratibu uliopo mimi sikubaliani nalo, lazima tuanze utaratibu mwengine wa kuona kwamba miradi ya wananchi inatekelezwa na inatekelezeka na Waheshimiwa wanahusishwa kikamilifu.

Nimekwenda kufuatilia miradi hii nilitaka kujenga soko Pete nikenda mpaka nikaghairi njiani nikasema potelea mbali basi, njoo kesho, fanya hivi, muone nani urasimu unakuwa mkubwa hakuna kinachofanyika.

Mhe. Spika, nina barua sitaki kuitoa hapa lakini ninayo ambayo niliomba nikafahamishwa nikaeleza lakini wananchi wetu hawaelewi utaratibu huo, hata ukimfahamisha hakuelewi. Sasa utaratibu mzuri ambao umeelezwa na Waheshimiwa Wajumbe mimi nadhani serikali ingekubali kuufuata mfumo ambao tunahisi sisi Waheshimiwa Wajumbe utatufaa. Kwa mfano, kuna miradi 29 kwa Unguja ambayo imegharimu shilingi 107 milioni na miradi 33 imegharimu shilingi 88.5 milioni, nikiuliza kati ya miradi 29 iliyotekelezwa Unguja ni majimbo mangapi yamefaidika, nafikiri hayafiki hata 15. sidhani, hapa napenda Mhe. Waziri uje utueleze ni majimbo mangapi yaliyofaidika na miradi hii 33. kwa sababu kwa dhana ile ile ya kwamba miradi 29 inawezekana majimbo 13 mpaka 14 ndio yamepata na kati ya majimbo hayo inawezekana mengine wamepata mara mbili na mengine mara tatu.

Mhe. Spika, sasa nataka nije katika kiini hasa cha mchango wangu katika bajeti. Mhe. Spika, ukurasa wa 36 kifungu cha 68 kinazungumzia upatikanaji wa maji safi na salama vijijini Unguja na Pemba. Naomba ninukuu,

Kifungu Nam. 68

> “Kazi ya usambazaji maji vijijini imekamilika kwa vijiji vya Jambiani Mfumbwi, Buyu, Mji Mpya, Kijichame, Ole Kianga, Shumba Mjini, Uroa Pongwe, Ole Kipangani, Dunga na Kiguuni”, ambapo wananchi wanafaidika na huduma ya maji safi.

Mhe. Spika, ni kweli, sitaki kuwasemea wenzangu kwa sababu sina uhakika nayo, lakini nataka kujisemea mimi katika jimbo langu. Nakubali tunafaidika na maji safi na salama na kwa hili naipongeza sana serikali, lakini hasa Mamlaka ya Maji kwa kutuwezesha na kufanikisha upatikanaji wa maji safi katika Kijiji cha Mfumbwi.

Nataka niseme sio kijiji cha Mfumbwi pekee, huu ni mradi wa shehia ya Jambiani Kikadini, unaunganisha Mfumbwi na vijiji vyengine vidogo vidogo vya shehia ya Kikadini. Kwa hivyo, ni bora ukaitwa mradi wa usambazaji maji shehia ya Jambiani Kikadini, kwa sababu hawafaidiki wananchi wa Mfumbwi peke yao, lakini wananchi wa Jambiani Shehia ya Kikadini wanafaidika na maji hayo.

Nguvu za Mamlaka ya Maji nimezipongeza, lakini mchango wa serikali *per se* haupo, nasema haupo na serikali iache kujikomba, kujipakapaka kwa miradi isiyogharamia, kwa sababu miradi ikishabuniwa sasa serikali inapiga kifua tumefanya hivi kumbe serikali yenyewe haikushiriki *total*.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipotakiwa aje awe mgeni rasmi katika uzinduzi wa maji safi na salama Jambiani Mfumbwi kwa bahati nzuri nashukuru alikubali kuja na akafanya hiyo kazi, kwa bahati mbaya mimi nilikuwa naumwa sikuwahi kufika, lakini nilikuwa nina mawasiliano ya karibu sana. Nataka nikwambie kwamba wananchi wa Mfumbwi walikataa walitaka usije wewe, walikataa walisema hatutaki, hatutaki, kwa sababu ya *commitment* ya serikali iliyokuwa pale ambayo haijatekelezwa mpaka leo.

Mhe. Spika, mradi huu ni wa wananchi, wananchi wamechangia karibu shilingi 18 milioni za kupatikana mabomba na vifaa vyengine. Wananchi kwa imani ya serikali yao wakaenda kuomba msamaha wasilipe kodi ya *VAT,* lakini kwa maelezo ya wizara na kwa muono wa wizara mwanzo walikubali namshukuru Mhe. Waziri alitupa barua ya *exemption* ikafanyiwa kazi, lakini majibu yaliyotoka *ZRB* hayakuniridhisha yana kiutaalamu taalamu na mimi nikafika pahala nikakubaliana na utaalamu wao kwamba aliyekwenda kuomba *exemption* ile ni mtu binafsi, haidhuru ni katibu wa mradi wenyewe lakini amejitia kama ni mtu binafsi.

Mhe. Spika, tukakaa na baadae tukarudi tena kwa Mhe. Waziri, yeye akatupa maelekezo, katika bajeti ya mwaka jana akanipa maelezo kwamba tuandike barua nyengine ya kuiridhisha wizara kuona kwamba waliohusika ndio walengwa wenyewe. Tukaandika barua hiyo tukawa tunafuatilia. Lakini cha kushangaza Mhe. Spika, tunapigwa mipira ukija huku mara waziri hayupo, mawaziri na watendaji wake wanagongana kwa kauli zao na ikafika pahala nikaona washauri wako Mhe. Waziri sio wazuri, hawakushauri vizuri.

Washauri wako wanajua kwamba tatizo la *exemption* lina matatizo kwa sababu wamesema kwamba hakuna sheria kama hiyo sijui kama ipo! Lakini waziri unaposema ni sheria, waziri unapozungumza ni amri, waziri unapotoa maelekezo lazima yafuatwe, lakini wafanyakazi wako wamepuuza maagizo yako na wamepuuza kwa makusudi au pengine kwa *exercise* ya *power* sijui vipi kama kwa kujiona wao ndio wao au wipi. Nitazungumza lugha mbaya mbaya, lakini nisameheni, kwa kujiona wao ndio wao na kwa maana hii hakuna ushirikiano kati ya waziri na watendaji.

Mhe. Spika, nimekwenda nina barua sitaki kuzisoma, lakini hizi zote ni za malumbano za kujibishana waziri na Katibu Mkuu, ingawa imesainiwa na mtu kwa niaba ya Katibu Mkuu, lakini nasema ni Katibu Mkuu. Taratibu zote tumefanya, lakini kosa Mhe. Spika, lilitokea tangu mwanzo, kwa sababu tangu mwanzo wamewaelekeza vibaya watu wangu.

Mhe. Spika, naomba nilisome hili somo ambalo limetoka *ZRB,* limeandikwa Kingereza samahani kama nitakosea.

APPLICATION FOR UTILIZATION OF VAT RELIEF TO TECHNICAL ASSISTANCE PROJECT MATERIAL AND EQUIPMENT

Please refer the heading above.

Zanzibar Revenue Board has recently received application for VAT relief in respect of the goods which are intended to be purchased in Dar Es Salaam Jambiani Development Committee. We therefore request you to assist the project in question in attaining the goods without VAT.

Enclosed herewith please find the proforma invoices and VAT relief form from our office as an evidence that the documents have been processed and recorded as follow:-

Hii ndio barua tuliyoipata imesainiwa na Seif Shaaban. Lakini fomu hii Mheshimiwa tulipoichukua kule ikakataliwa, kwa maana ya kwamba fomu hii ni 223 zilikuwa zinatakiwa mbili na 224 nafikiri ziwepo. Walipokuja afisini kwa *ZRB* wakaambiwa iko fomu nyengine hamkunijazia, cha kushangaza wakasema kwamba sisi hatuna uzoefu wa mambo kama hayo, hatujawahi kufanya *community* kama hizo, lakini ikaonekana hapa pana kasoro. Sasa tukafika hatua mpaka kwa waziri na yeye mpaka leo hatujapata maamuzi yoyote.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kiongozi shahidi hili suala analijua vizuri, aliwahi kutuita katika ofisi yake akatupa maelekezo mazuri tufuate ngazi za wizara, wizara tukaona tuanzie *ZRB*, *ZRB* tulipokutana na Kamishna Mhe. Moh'd Hashim akanambia mheshimiwa tatizo hilo liko wizarani rudi tena wizarani nikamwambia *never,* siendi. Kusema kweli sikwenda na sikutaka kulisema, lakini nasema hapa *purposely* kwamba kuonekana jinsi gani tumechukua hatua na jinsi gani wananchi wa Jambiani walivyokerwa na ahadi zisizotekelezeka za serikali. Huku ni kuipaka matope serikali yetu, wananchi wamepiga hatua kubwa kuweza kuchangia shilingi 18 milioni ni jambo la kushukuriwa, ni jambo ambalo serikali ilikuwa inahusika iwajibike yenyewe, lakini kwa msaada wenu hatukuuona na kwa hadithi hii ya njoo kesho, nenda kesho hakuna kitu inatuvunja moyo.

Mhe. Spika, sasa hadithi itakuwa ndefu, siombi, lakini kama akinitaka Mhe. Waziri Kiongozi tukae na Waziri mwenyewe na watendaji wakuu nitafanya hivyo, lakini juu ya kukaa kwenyewe kulizungumza suala hili suala moja ninalotaka sasa siombi, ni kuona kwamba pesa zile sh. 2,892,800 zirejeshwe kwa wananchi wa Jambiani. Kwa sababu hizi walikwenda wakalipa wenyewe tena baada ya kuona mapira yao hayatoki ikabidi wakachanga tena pesa hizo wakatoa ndio wakapata kuchukua mipira yao. Kwa hivyo, hili suala limetuweka pabaya, limeiweka pabaya serikali na ushahidi ni kwamba *chief* walimsusia walitaka asiende kwenye mkutano wao, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba nilitumia busara na maarifa pamoja na kwamba sikushiriki, lakini shughuli ile imefanikiwa tumeifanya vizuri isipokuwa deni hili wananchi bado wanalikumbuka.

Mhe. Spika, kama haiwezekani kwa sheria zenu za kifedha mtoe kauli hapa hapa mbele ya Baraza. Mimi nataka waandishi wa habari mweke hii msiweke mambo mengine, mweke hii kwenye vyombo vyenu vya habari ili wananchi wangu wasikie. Kwa sababu sasa wamesha-*loose interest* na mimi wananikosesha jimbo Mhe. Spika. Mhe. Waziri unanikosesha jimbo, lakini na mimi nitakufa na mtu sifi peke yangu.*(Kicheko)*

Mhe. Spika, nafikiri zifanywe taratibu, kama waziri alikosea kuandika barua ya kuombea msamaha basi ni mambo ya kuwekwa sawa, tusiwe na pingamizi na wananchi wetu kwa sababu wananchi wamechangia pakubwa sana.
Mhe. Spika, naomba nimalizie mchango wangu kwa juhudi za kuimarisha kipato ukurasa wa 56 kifungu cha 105. Mhe. Spika, katika kuimarisha mapato serikali imebuni njia mbali mbali za kuongezea mapato, moja wapo ni kuanzisha kodi ya ardhi kwenye matumizi ya bahari yanayoambatana na ujenzi wa gati (*jet*) katika mahoteli ya kitalii. Kodi hii inalenga kupunguza ujenzi wa gati hizo ili kulinda mazingira.

Mhe. Spika, hili nililizungumza kwenye kamati yetu ya wenyeviti, nikaonesha nia yangu kwamba sikubaliani nalo, sikubaliani nalo kwa sababu mbili, kwanza hapa mnatwambia kodi inalenga kupunguza ujezi wa *jet* hizi wakati kodi hii inalenga kusaidia mapato ya serikali. Kodi hii hailengi kupunguza ujenzi wa *jet* inalenga kuongeza mapato. Lakini *jet* tunazozizungumza ni kwamba zinachafua mazingira ya bahari, nambieni mahoteli mangapi yenye ujenzi wa hizo *je*t? Hii Unguja peke yake ni mahoteli mangapi yaliyojengwa hizo *jet* za kuweza kukusanya mapato hayo.

Mhe. Spika, *jet* hii ni kama daraja la mbao, linajengwa kuanzia kwenye ufukwe mpaka kufikia kwenye mito yaani maji mengi, kule wananchi wetu wanapita wakati huku maji yanakuwa makavu huwezi kupita na ngarawa lazima upite kwa miguu, lakini unapotaka kupita na ngarawa yako unapita kule ilikoishia *jet* kwenda sehemu nyengine. Lakini kule inakuwa hupiti sasa hivi, wananchi wamehodhi na wengine samahani si wananchi ni wawekezaji wamehodhi mpaka sehemu za kule, sasa inakuwa ugomvi baadhi ya raia na wawekezaji. Kwa hivyo, hili naona ni tatizo, tatizo hili mimi naona tusijaribu ku-*entertain* kuwa liwepo kwa sababu ya kutaka mapato, hili linachafua mazingira na linaleta matatizo na wananchi kwa sababu wananchi kwenye sehemu zao wanakuwa hawapiti kwa sababu ukipita sehemu za fukwe wakati watu wanakuwa wanapita na baskeli zao sasa hivi itakuwa hawapiti. Hii ni hatari Mhe. Spika.

Kwa hivyo, ujenzi wa *jet* hizi kwa kweli tuufikirie upya kama ni kuongeza kipato kwa ujenzi wa *jet* tutizame. Kwa sababu kama kwa suala hili ni kuwafanya wawekezaji wasijenge jet mimi naona si kweli, watajenga kwanza haijulikani ni kiasi gani wanatozwa kodi yao, kwa hivyo wataendelea kujenga na wakiendelea kujenga wataharibu mazingira na ugomvi utakuwa hawishi baina ya wavuvi na wananchi.

Mhe. Spika, naomba nimalizie hapo, lakini naomba nitoe tahadhari kwanza, sitoshawishika kuunga mkono bajeti hii kuu ya serikali kama serikali haijanambia kesho mnanipa shilingi milioni mbili na laki nane za wananchi wa Jambiani Mfumbwi. Vyenginevyo Mhe. Waziri *I swear upon god* kwamba sitounga mkono bajeti hii ya serikali, kwa sababu nikiunga mkono mtaniweka pabaya, nitakuwa na mimi nimo katika kuwanyang'anya wananchi waliotoa michango yao mfukoni mwao.

Mhe. Spika, baada ya hayo nasema nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa michango mmenisaidia kuendesha kikao hiki.

(Saa 7:00 mchana Baraza lilihirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuna wachangiaji kama 11 hivi, ambapo kuna na Waheshimiwa Mawaziri wawili watatu pia na wao watahitaji kuchangia, jumla naweza nikafanya kama wachangiaji 15. Nakusudia tuwamalize wote lakini pia Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame aje apate wasaa wa kutosha kesho kuweza kufanya majumuisho na ikiwezekana kipindi cha asubuhi, kama itakuwa hakumaliza basi tumalizie jioni.

Lakini tuna shughuli moja ndogo ya kawaida ambayo huwa tunaifanya kila mwaka nayo ile ya Mpango wa Uhai wa Mtoto tulitaka tuichomeke kesho jioni. Nafikiri Mhe. Waziri wa Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto pengine amearifiwa kazi ambayo nadhani itafanywa na Kaimu Waziri nafikiri pia ameshaarifiwa. Kwa hivyo, tujaribu kuumega muda kama kawaida.

Nilipata wachangiaji wengi hivi mwisho mwisho wakati huo tumeshaachia sana dakika 30 na nyongeza juu, kwa hivi mwisho mwisho sasa wakamiminika wachangiaji wengi hali ambayo inafanya itukwaze kidogo katika ugawaji wa muda. Lakini hata hivyo, tutajitahidi ili tuone wachangiaji wote wanapata nafasi.

Kwa sababu hiyo tu niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tujaribu kupanga pointi zetu vizuri ili tuweze kumaliza michangio kwa kiasi kikubwa leo labda tukiachia mawaziri wachache tu pengine kesho asubuhi. Tutumie kama dakika 15 kufanya shughuli hiyo.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin: Mhe. Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha jioni hii kukutana tena katika Baraza lako tukufu kuzungumzia bajeti ya serikali.

Mhe. Spika, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa mwanzo katika jioni hii. Kutokana na mnasaba wa maelezo yako Mhe. Spika, itabidi niende haraka na nianze na zile sehemu ambazo nazihisi ni muhimu sana katika mchango wangu kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, kwa hali hiyo naanzia na kuchangia kwenye kifungu cha 72 kinachozungumzia juu ya barabara. Mhe. Spika, katika kifungu hicho tumeelezwa kwamba kilomita 47.2 za barabara zimekamilika kujengwa kwa Unguja. Wakati Pemba ni kilomita 6.5 tu zilizokamilika kujengwa katika kipindi cha mwaka unaomalizika ambazo ni za Mkoani/Makombeni. Kilomita 24.9 Unguja zinakaribia kumalizika wakati Pemba hakuna hata kilomita moja ambayo inakaribia kumalizika kwa wakati huu.

Mhe. Spika, ukiangalia hali hii kwa kweli ni hali inayovunja moyo sana kwa sababu serikali imeelekeza nguvu zake upande mmoja tu wa kisiwa hiki. Mhe. Spika, unapolizungumza hili kuna watu huwa labda kama wanachukia hivi. Lakini kama wanachukia kwa nini serikali ikawa kila mwaka inarudia jambo hilo hilo. Kwa sababu asubuhi alipozungumza Mhe. Mohamed Ali Salim kuhusiana na zao la karafuu, alipoeleza kwamba inafanywa vile na serikali kwa sababu zile karafuu ni nyingi zinatoka Pemba kuna watu waliita paka hapa chu! chu! chu! Maana yake nini? Sasa kama hili linawakasirisha basi waiambie serikali iache kufanya utaratibu huu ielekeze nguvu zake sawa sawa katika visiwa vyetu hivi viwili. Vyenginevyo tutaendelea kusema mpaka pale serikali itakaposikia na kuzingatia.

Halafu Mhe. Spika, kwenye hii hii barabara nasema nashukuru sana kwamba ule wimbo wa kawaida wa kila mwaka unaoimbwa katika Baraza hili na serikali wa kusema kwamba barabara 3 za kaskazini zimeshawekewa saini kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo. Kwa sababu mwaka jana tulisikia habari hiyo, mwaka juzi tulisikia habari hiyo na mwaka huu habari hiyo imerejewa tena vile vile kwamba barabara 3 za kakazini zimeshawekewa saini na kibwagizo chake ni barabara 6 za kusini nazo zitajengwa. Lakini kujengwa kwa barabara hizo ni kwa maneno sio kwa vitendo. Sasa hili ni jambo linalosikitisha sana.

Mhe. Spika, kuna barabara hizi 6 za kusini zinazotajwa kila mwaka ambazo ni Mtambile/Kengeja/Kiwani, halafu barabara ya Mtambile/Kangani na kuna barabara ya Mizingani/Wambaa, barabara ya Kenya/Chambani na barabara ya Chanjamjawiri/Tundauwa.

Sasa Mhe. Spika, hadithi hii serikali itaiendeleza mpaka lini? Kwa nini hawako serious katika shughuli hii ya kulisimamia hili jambo ili wananchi wakaweza kunufaika na matunda ya serikali yao.

Mhe. Spika, nadhani serikali imenisikia na mwaka huu wa fedha 2009/2010 huu wimbo hautarejewa tena katika kikao cha bajeti cha mwaka unaofuata. Tutakuja kuambiwa hadithi nyengine kwamba kati ya hizi barabara 6 za kusini angalau 4 zimekamilika kujengwa na zile 3 za Kaskazini Pemba nazo zimekamilika ujenzi wake. Nina mategemeo hayo sana.

Mhe. Spika, baada ya hapo nakwenda kwenye nishati. Imetajwa katika kitabu cha bajeti kwamba kutakuwa na usambazaji wa umeme vijijini. Sasa Mhe. Spika, katika usambazaji huu wa umeme vijijini ningemuomba sana Mhe. Waziri na hasa nitakuja kuizungumza kwenye wizara husika lakini na hapa niitaje kidogo. Mhe. Spika, katika jimbo langu la Mtambile kuna shehia mpya imeanzishwa ya Minazini ambayo bahati mbaya hawajapata huduma hii ya umeme wala maji safi. Kwa hivyo, ningeomba wakati utaratibu unatayarishwa wa usambazaji wa umeme vijijini basi wizara husika ifikirie vijiji vya shehia hiyo ambavyo ni vijiji vya Kihumoni, Kidutani, Mtadoda, Mikinduni na Kivumoni. Mhe. Spika, haya niliona niyatangulize mapema kwa sababu ya muda.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 33 cha hotuba hii ya bajeti tumeelezwa kwamba kuna hatari ya uchumi kushuka kwa hizi nchi ambazo ziko Kusini mwa Jangwa la Sahara mpaka kufikia asilimia 2.9 katika mwaka 2009. Sasa Zanzibar ni miongoni mwa nchi ambazo ziko Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri. Baada ya serikali kuelezwa na wachumi wetu kwamba kuna wasi wasi wa kujitokeza hali hiyo. Serikali inachukua hatua gani ili kuweza kukabiliana na tatizo hilo ambalo litakuwa ni kubwa. Kwa sababu uchumi kupungua kutoka asilimia 5.4 mpaka kufika 2.9 ni kiwango kikubwa cha kupungua kwa uchumi. Sasa bila shaka kutakuwa na athari kubwa kwa nchi pamoja na wananchi wake. Je, serikali inachukua hatua gani kuweza kukabiliana na hali hiyo?

Mhe. Spika, vile vile katika hotuba hii tumeambiwa kwamba pato la mwananchi limepanda mpaka kufikia shilingi 639,000,000/=. Mhe. Spika, ikitajwa hii utaona kwamba ni fedha nyingi na kwa kweli sasa ichukue hiyo 639 milioni uigawanye kwa mwaka mzima, utakuta kwamba mtu mmoja pato lake litakuwa ni kama shilingi 100,750/=. Mhe. Spika, pamoja na kwamba fedha hii labda tunaiona ni kubwa lakini haitoshelezi kumwezesha mwananchi Mzanzibari kuweza kununua kilo moja na nusu ya mchele wa *jasmine* ambapo kilo moja ni kama shilingi 1,950/=.
Sasa yeye pamoja na kupanda kwa pato lake bado anashindwa kuweza kumiliki kununua hiyo kilo moja ya mchele wa *jasmine*.

Mhe. Spika, ongezeko hili pamoja na kwamba ni kubwa lakini bado kuna haja ya kuliangalia kwa makini zaidi ili kumwezesha huyu mwananchi kuweza kuyamudu maisha yake.

Mhe. Spika, ni kweli kutokana na utaratibu wa kiuchumi kwamba kuongezeka kwa pato hili la taifa hakuendani na kutononosha maisha ya mwananchi. Lakini

wachumi wangefikiria tufanye nini ili mwananchi na yeye aweze kutononoka kutokana na kupanda kwa pato la taifa.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba biashara yetu inategemea usafirishaji wa mazao mawili yaani karafuu na mwani. Mhe. Spika, ni aibu kabisa kuambiwa kwamba Zanzibar ni visiwa vya kiungo *(spice islands).* Hivyo tunasafirisha kiungo gani sisi nchi, hakuna. Sasa serikali imekuwa makini kiasi gani?

Hapo nyuma ilikuwa kuna viungo vinasafirishwa na kuiingizia serikali fedha za kigeni, lakini kila miaka inapokwenda mbele kwa kweli uzalishaji wa viungo huu ulianza kufifia na kufifia mpaka sasa hivi umetoweka kabisa. Mhe. Spika, nadhani kuna haja kwa serikali kuona kwamba sasa hivi umefika wakati wa kuwashajihisha wakulima kurudi tena kulima hivi viungo ili serikali iweze kuongeza wigo wake wa bidhaa zinazosafirishwa nje na kupunguza uagiziaji ili kupunguza ile nakisi katika urari wa biashara.

Mhe. Spika, Waziri kivuli alitwambia kwamba ilikuwa Zanzibar inazalisha tani 24,000 kwa mwaka zikashuka kidogo kidogo na serikali bado ikawa inaliangalia tu hilo tatizo lenyewe, haikuchukua hatua muafaka ili kuweza kurekebisha hiyo hali. Mpaka sasa hivi wastani wa uzalishaji wa karafuu ni kati ya tani 2,000 mpaka 4,000 kwa mwaka.

Sasa hii imetokana na kuwadharau wazalishaji wa karafuu kama alivyozungumza Mhe. Mohamed Ali Salim asubuhi. Kutokana na dharau hiyo wazalishaji wa karafuu wamevunjika moyo na wameacha kuyashughulikia mashamba yao ya mikarafuu. Mhe. Spika, mkarafuu ni mti ambao unapenda starehe, unapenda maji mengi na unapenda uwe katika hali ya mazingira yaliyokuwa safi kabisa. Hivi sasa mashamba ya mikarafuu yameachiwa magugu na hali ya hewa ulimwenguni imebadilika, idadi ya kiasi cha mvua kinachonyesha kwa mwaka kimepungua, kwa hivyo maji ardhini yamepungua.

Kutokana na hayo, bila shaka mikarafuu itakuwa imeathirika sana na matokeo yake ndio kama alivyosema Waziri Kivuli kwamba karibu asilimia 70 ya mikarafuu sasa hivi imekuwa ni mizee na mingi imekufa. Hii imepelekea kupungua kwa uzalishaji wa karafuu. Pia bei duni anayopewa mkulima nayo imesababisha wakulima kuvunjika moyo na kuacha kuishughulikia mikarafuu yao. Sasa nadhani ingekuwa vyema kwa serikali ikatanabahi na kuweza kuwaangalia hawa wakulima wa karafuu.

Kwa sababu katika bajeti hii mfanyakazi kaangaliwa lakini mkulima wa karafuu hajatajwa. Sasa Mhe. Spika, kweli serikali inategemea wafanyakazi tu, hawa wakulima wao hawana sehemu yoyote wanayochangia katika serikali. Kwa nini bajeti haikutwambia kwamba na wakulima nao wameangaliwa kwa

kiasi gani. Kwa hivyo, hili ni suala muhimu ili kuona kwamba wakulima na wao wanaangaliwa kwa ajili ya kuweza kuyashughulikia mashamba yao.

Mhe. Spika, utaratibu huu wa ununuzi wa karafuu kupitia Shirika la *ZSTC* na wao wakawa ndio wauzaji peke yao nalo linachangia katika kupunguza ushughulikiaji wa karafuu. Mara nyingi tumeishauri serikali ilibinafsishe zao hili ili wakulima waweze kuuza karafuu zao popote pale wanapotaka. Kama bei ikipanda au ikishuka itakuwa ni juu yao wenyewe namna gani ya kuweza kukabiliana na hiyo hali.

Lakini inavyoonekana Mhe. Spika, labda kuna kikundi cha watu kilichojificha nyuma ya serikali ndio kinachonufaika zaidi na hili zao la karafuu na kwa hivyo serikali inapata kigugumizi kulibinafsisha zao hili. Kwa hivyo Mhe. Spika, nadhani serikali sasa hivi umefika wakati kuliona hilo na ikachukua hatua muafaka katika kulibinafsisha zao hili la karafuu.

Mhe. Spika, la mwisho tumeelezwa katika bajeti hii kwamba serikali inakusudia kuimarisha utawala bora na kujenga demokrasia nchini. Ni habari njema kwa sababu utawala bora na demokrasia ni mambo yanayokwenda sambamba na hali hiyo ikiwepo katika nchi basi nchi inakuwa katika utulivu na amani kwa hivyo inaweza kujenga uchumi wake. Mhe. Spika, wasi wasi wangu kwamba haya kama yalivyo maelezo ya barabara na haya ni maelezo tu ya kwenye kitabu lakini hali halisi haiko kama ilivyo.

Mhe. Spika, katiba imempa haki mwananchi Mzanzibari kuweza kuchagua viongozi anaowataka. Sasa hivyo ndio katiba inavyosema lakini sasa hivi kunafanywa vipenyo vipenyo ili kumzuia Mzanzibari huyu kuweza kushiriki katika uchaguzi wa kuchagua viongozi anaowataka.

Mhe. Spika, kuna hii *ID* ya Mzanzibari, hiki kimewekwa kama ni kipingamizi kwa Wazanzibari wasiweze kuchagua viongozi wao kwenye uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwakani. Mhe. Spika, hili ni tatizo, kama ndio kuna kamati za ushindi katika kila ngazi ya nchi hii, basi kamati hizo za ushindi zitakuja kuipeleka nchi hii pahala pabaya. Ni lazima kama serikali imeamua kuanzisha hivi vitambulisho basi ivitoe kwa wanaostahiki bila ya pingamizi. Lakini sasa hivi imekuwa ni tatizo kwa Wazanzibari kupata hizi *ID*.

Mhe. Spika, mimi nasema kwa uhakika na kwa ushahidi. Ninae binti yangu alizaliwa mwaka 1989 na hii ni 2009 ana miaka 20. Kenda kujaribu kutaka *ID* hapati anatiwa huku akitiwa huku. Huo ni mfano hai kabisa wa ushahidi. Maana yake wale watu wengine unaweza kusema pengine wanadanganya lakini huyu nimemsimamia mimi mwenyewe na *ID* kaikosa. Sasa hii maana

yake ni kwamba kuna ajenda ya siri ndani ya serikali iliyoandaliwa na chama kinachoongoza serikali hiyo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria ya kuanzisha vitambulisho mtu kuwa hana kitambulisho ni kosa la jinai. Sasa kama hivyo ndivyo na serikali haitaki kuvitoa hivi vitambulisho, sisi tutawaambia wananchi wetu wote kwa amani kabisa waende polisi wamwambie Mkuu wa Polisi awakamate na awafungulie mashtaka ya jinai kwa kukosa hivi vitambulisho. Kama serikali haikuacha mtindo wake huu wa ubabaishaji kwa watu wetu, basi itafika wakati tukawaambia watu wetu waende vituo vya polisi ili wakamatwe wafunguliwe mashtaka ya jinai kwa ajili ya kukosa vitambulisho. Kwa hivyo, tunaitahadharisha na tunaitanabahisha mapema serikali kwamba ikiwa inataka tuendelee katika hali tuliyonayo sasa basi waache mizengwe yao katika utoaji wa hizi *ID*.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru na ninawapa nafasi wenzangu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mambo muhimu yanayohusiana na bajeti yetu. Mhe. Spika, kwanza niseme kwamba bajeti iliyoko mbele yetu ni muhimu sana kuliko takriban bajeti nyingi zilizopita. Umuhimu wa bajeti hii unatokana na vitu vitatu vikubwa. Kwanza tukumbuke kwamba hii ni awamu ya sita na hiki ni kipindi cha pili cha awamu ya sita. Takriban katika utendaji wa awamu ya sita ni kusema kuwa tayari tumeshakamilisha asilimia 95. Maana bajeti hii ndio itakayokamilisha ngwe hii ya awamu ya sita. Itaanza Julai mwaka huu na itamalizika Juni mwaka 2010. Kwa hivyo, ile lala salama ya serikali hii itamalizwa na bajeti hii, kama kuna mwiku au kiporo chochote kilichobakia na tunatazamia kwamba bajeti hii ndio ifanye mambo ya kukamilisha.

Mhe. Spika, la pili tutakumbuka kuwa mwaka 2010 ndio kile kipindi ambacho MKUZA kutoka 2007 – 2010. Kwa hivyo, ni kipindi muhimu kwa bajeti hii kutumika kama ni kipimo katika utekelezaji wa ule mpango wa serikali wa kupunguza umaskini.

Mhe. Spika, la tatu bajeti hii imekuja katika kipindi ambacho dunia nzima kwa kweli imekubwa na mtikisiko wa kiuchumi pamoja na mtikisiko wa fedha. Kwa hivyo, kwa umuhimu huo kwa wakati huu tulionao tulitazamia kwamba bajeti hii iwe ni bajeti maalum ya kujibu tatizo hilo la dunia ambalo takriban na sisi Zanzibar hapa ni sehemu yake. Mhe. Spika, kwa hali yoyote tunasema kwamba bajeti hii ni muhimu na ni lazima tuichangie katika umuhimu wa mambo hayo matatu.

Mhe. Spika, jengine nizungumzie Sheria Nam. 6 ya mwaka 2007 *section 3, sub-section 1* kwa ruhusa yako naomba ninukuu.

> *"The Government shall disperse not less than one percent of annual Government Recurrent Budget, in the grant observation of two political parties in pursuance of the provision of this act"*

Hii ni sheria iliyosema kwamba vyama vyetu vya siasa vinahitajika kupewa asilimia moja ya mapato yake ya mwaka. Lakini tangu kupitishwa sheria hii mwaka 1997 hadi leo ni miaka takriban 12 kama sikosei, katika chama changu bado hatujapokea gawio letu linalotokana na sheria hii. Sasa hili ni tatizo kwa sababu hivi ndivyo sheria ilivyoeleza na bado haijafutwa na tayari chama changu kimeshakudai Mhe. Waziri nakumbuka. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha atueleze kwa nini bado hajatekeleza sheria hii na kukipatia chama changu mabilioni yake ambayo yapo katika mfuko wako. Je, Mhe. Waziri huo utakuwa si uvunjaji wa sheria unaofanya kwa sababu tayari sheria imeshakuelekeza kwamba ufanye hivi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, Mhe. Waziri Mwenyezi Mungu amnusuru akiondoka leo katika dunia itakuwa chama changu kinakudai. Mwenyezi Mungu amjaalie asimuondoshe mpaka alipe deni la chama changu.

Mhe. Spika, nataka nieleze maana ya bajeti. Sasa hivi tunazungumza bajeti lakini wananchi wanaelewa nini, mtazamo wa bajeti kwa wananchi unakuwa ni upi. Mtazamo wa kwanza ni ule tuliouzoea kwamba bajeti ni mpango wa serikali katika kukusanya na kutumia kwa mwaka. Kwa hivyo, katika kila hali kibajeti tunategemea kwamba matazamio yetu tunatazamia kwamba mapato ya ndani ya serikali yawe yanaongezeka kila mwaka. Hii ni pamoja na urekebishwaji wa viwango vya kodi. Mhe. Spika, tunatazamia Mhe. Waziri anapokuja hapa atwambie kodi hii inafutwa, kodi inaongezwa, kodi hii inapunguzwa, ili tupate kujua katika viashiria ambavyo tunavitumia katika serikali yetu kukusanya tujue kwamba uchumi wetu unakua na haukui.

Kwa hivyo, mtazamo wa wananchi na sisi wengine ni kuona kwamba kila mwaka tunapata mapunguzo ya viwango vya kodi, kodi nyengine kuongezwa, kodi nyengine kufutwa, kodi nyengine kupungua ili tuone hali ya uchumi wetu inakwendaje. Lakini pia mtazamo wa wananchi katika suala zima la mambo ya makusanyo ya kodi basi ni kuona kwamba serikali iliyo makini siku zote inaongeza kodi katika suala la maendeleo. Hili kama waliotangulia kueleza kwamba bajeti hii kwa kuwa ulitwambia kwamba zaidi ya asilimia 50 inaelekezwa kwenye kodi ya maendeleo, basin a mimi naungana na wenzangu kwa hili kukupigia saluti Mhe. Waziri au serikali kwamba imeona umuhimu wa kuongeza matumizi katika sekta ya maendeleo.

Mhe. Spika, la pili maana ya bajeti ni suala zima la kuelezea hali ya uchumi ilivyo katika nchi. Bajeti inatakiwa ioneshe sura ya hali ya uchumi, aidha wananchi wafahamu kwamba uchumi wetu unakua au haukui. Tutakapoambiwa uchumi wetu unaimarika basi wananchi wanachokitegemea ni kuongezeka kwa kipato cha mtu mmoja mmoja. Bajeti iliyokuwa tunaambiwa inakua lakini wananchi wetu hawana fedha, yaani kipato chao hakikui, kwa hivyo ukuaji huo wa bajeti unakuwa na mashaka.

Vile vile bajeti inayokua ni kuongezeka kwa ajili tunatazamia vijana wetu wengi wapate ajira. Bajeti iliyokuwa inakua lakini haitoi ajira kwa vijana pamoja na wananchi kwa jumla, kwa kweli bajeti hiyo ukuaji wake unakuwa na wasi wasi.

Kuimarika kwa uchumi kuna kwenda sambamba na kuimarika kwa huduma za kijamii. Suala la msingi zaidi ni kupungua kwa kodi zinazowaumiza wananchi. Tunaposema kwamba uchumi wetu unakua hilo liende sambamba na kodi ambazo si za lazima kwa wananchi zipungue. Lakini kinachotokea Mhe. Spika, kwa kweli kila uchumi unavyokua katika nchi yetu kodi au michango kwa wananchi inazidi.

Mhe. Spika, hivi karibuni watoto wangu wanapokwenda skuli, basi nilikuwa na wasi wasi kwamba nyinyi watoto isijekuwa mnanitapeli, kwa sababu mara mchango wa buku pamoja na mambo mengine. Kwa hivyo, tutaona kwamba kwenye Sekta ya Afya pamoja na Elimu utaona michango inazidi na kuwaumiza wananchi, kitu ambacho hakiendani kabisa na ile dhana ya kukua kwa uchumi *(Makofi)*.

Suala jengine ambalo linashiria kuwa hali ya uchumi inakua ni jambo la kupunguza utegemezi, kitu ambacho kwa Zanzibar ni tofauti. Mhe. Spika, juzi Mhe. Haji Faki Shaali aliuliza swali kwamba kinachopigiwa kofi kwa upande wa Chama Tawala ni kitu gani? Kwa sababu kadri siku zinavyokwenda kwa kweli sisi tunaongeza na ile haitoi picha nzuri kuongeza wafadhili kila siku.

Isipokuwa tunachotegemea kama mwaka jana nchi zilizotusaidia ni 50 basi mara hii tuzitegemee kama nchi 20 na nyengine tuziambie basi, kwa sababu kwa kiasi fulani tunajizewa katika nchi yetu. Lakini hali hiyo sivyo ilivyo. Kwa kweli kila miaka inavyokwenda mbele wahisani pamoja na wafadhili wanazidi jambo ambalo linatupa wasi wasi katika suala zima la kukua kwa uchumi wetu.

Mhe. Spika, kuimarika kwa uchumi kinyume chake ni kudorora kwa uchumi. Kama nilivyosema mwanzo kwamba dunia yetu leo imekumbwa na msukosuko wa uchumi na fedha, Zanzibar nayo imo.

Kwa hivyo, kwa vyovyote tulitegemea kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar kama alivyofanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangulia kulieleza Bunge. Kwa upande wa Zanzibar tulitegemea Rais wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume naye atangulie kutupa ile *Economic Stimuli Strategic Plan* yake katika ku-*rescue* uchumi wetu.

Kitu ambacho katika bajeti hii hatujakiona sehemu yoyote ile. Kwa sababu yoyote ile, uchumi wa dunia unavyoyumba kwa vyovyote vile, utakuwa na mahusiano na uchumi wa Zanzibar. Kwa sababu Zanzibar tunasafirisha nje pia tunaagiza kutoka nje.

Mhe. Spika, kwa vyovyote vile ikiwa uchumi wa dunia unayumba, kuuza kwetu bidhaa zetu kama tunazo kutayumba. Lakini hata tukisema kwamba tunaagiza kwa sababu tayari viwanda vinafungwa, basi kwa vyovyote vile bidhaa zitakuwa chache. Kwa hivyo, bidhaa zitakapokuwa chache kuingia nchini, kitu kitakachotokea ni mfumko wa bei za vyakula au bidhaa muhimu.

Katika hili tulitegemea kwamba serikali ije na ile *package* ya kuunusuru uchumi wetu ambao unategemea moja kwa moja uchumi wa dunia. Kwa kweli mpango huo mpaka hivi sasa bado haupo, kwa sababu kwa vyovyote vile watalii watapungua kuja.

Kwa hivyo, hatujui ni kiasi hoteli zetu zitapata hasara kwa kupungua kwa watalii. Je, serikali inajiandaa vipi kuzisaidia hoteli ambapo kwa asilimia kubwa zinachukua mikopo, ili katika kipindi hiki cha mpito ziweze kufanya shughuli zake kama kawaida.

Mhe. Spika, pia tulitegemea kwa zao la karafuu, lakini zao la karafuu halitoathiriwa kwa sababu tokea asubuhi zao hilo bei yake si nzuri. Hata kama ingelikuwa bei nzuri basi tulitegemea kwa vyovyote serikali ifanye *injection* ya fedha kwenye Shirika la *ZSTC*.

Lakini uchumi haujaharibika serikali inadaiwa na Shirika la *ZSTC*, sijui hivi sasa uchumi unayumba duniani shirika litakuwa vipi. Shirika linaidai serikali shilingi bilioni 4 kwa wakati huo ambapo uchumi haujayumba, sijui wakati huu.
Kutokana na hali hiyo, tulitegemea serikali ichukue hatua madhubuti ya kulipa deni hili kwa Shirika la *ZSTC*. Kwa sababu Mhe. Waziri hajatuambia chochote, isipokuwa tunaambiwa karafuu bado ni zao la biashara, kwa namna yoyote ile serikali itaendelea. Ingawa sisi tunavyodai kwamba karafuu wananchi waachiwe wenyewe wakauze wanakotaka.

Mhe. Spika, sura nyengine ya bajeti. Kwa kweli bajeti yetu inatakiwa iwe na sura ya mgawanyo sawa wa rasilimali zetu za taifa. Kwa sababu bajeti zote zinazokuja hapa tunasikia Pemba kumefanywa hivi na Unguja kumefanywa vile. Tafsiri ya mgawanyo sawa wa rasilimali haioneshwi kwenye bajeti zetu.

Waliokwenda kwenye Bunge la Kenya hivi karibuni wametuambia akina Mhe. Ame Mati Wadi kwamba, kiasi gani ule Mfuko wa *CDF* ulivyozuka kutokana na tatizo kama hili. Sasa bajeti iliyokuwa haioneshi mgawanyo wa rasilimali sawa katika nchi, basi bajeti hiyo inakuwa na mapungufu makubwa.

Kwa hivyo, sura ya bajeti kwa tathmini yangu inatakiwa iwe kwenye namna hizo tatu. Lakini uchumi wetu wa Zanzibar Mhe. Spika kama nilivyosema unakua kitakwimu kila mwaka, hali halisi haiko hivyo, yaani wananchi wetu bado wanapata matatizo tena ni masikini wa kipato.

Miongoni mwa matatizo ni kwamba hakuna ongezeko. Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri ongezeko la vianzio vya kodi hakuna, isipokuwa kuna ongezeko la kodi na hili ni tatizo. Kwa vyovyote vile tulitegemea kila mwaka Mhe. Waziri atuletee na mpango wa kutuongezea vyanzo vipya vya kodi na wala asituambie kwamba kodi inakua, lakini ikawa kodi inayokua inatokana na vianzio vile vile. Kwa kweli hili ni tatizo letu kubwa sana.

Kwa mfano, kwenye duka moja linatozwa kodi mara nne mpaka tano, yaani ni sawa na kumkama ng'ombe maziwa ambaye humlishi. Kutokana na hali hiyo, tutafika pahala hata hicho kinachotupa kodi leo basi kesho kitakuwa hakina uwezo wa kutupa kodi tena. Hili pia ni tatizo.

Mhe. Spika, tatizo letu jengine kwa uchumi wetu wa Zanzibar ni kuendelea kutegemea wafadhili. Kwa sababu mtu siku zote huwa anatakiwa akusaidie mara moja au mbili na wala hatakiwi akusaidie siku zote, isipokuwa akikusaidia siku zote atakuvunjia nyumba. Kwa hivyo, hawa wafadhili kama siku zote kazi yetu kupiga magoti na kuwategemea wao watatuvunjia nyumba. Vile vile Mhe. Asaa Othman Hamad alizungumza hapa asubuhi nyumba ya mama itavunjwa na hilo ni tatizo.

Lakini katika hali kama hiyo, Mhe. Spika Zanzibar ni nchi nzuri sana na sijui kwa nini hadi leo tunaendelea kutegemea wafadhili. Kwa nini hadi leo tunaendelea kulia na suala la uchumi na wala hakuna sababu, mimi nasema hakuna sababu.

Kwa kweli hili halitaki mtu mwenye akili sana kama vile Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, yaani mtu wa kawaida anaweza kupanga mambo yake na yakanyooka kwa nchi hii ya Zanzibar. Mhe. Spika, ni

aibu kuwa mpaka leo Zanzibar tunategemea wafadhili, yaani hivi sasa kitu gani ambacho hatuna *(Makofi)*.

Mhe. Spika, Zanzibar tunayo hali ya hewa ambayo mazao ya aina yoyote yanaweza kukua katika nchi hii. Kwa mfano, kuna nchi ni jangwa tu, na bado nchi zile zinazalisha. Lakini Zanzibar leo ukitupa kisiki cha muhogo popote pale na Mhe. Waziri mwenye ni mtaalamu zaidi wa kilimo, yaani hakuna zao utakalolipanda lisiote kwa nini kuwa mpaka leo tunategemea chakula cha kuagiza.

Kwa kweli ardhi yetu bado haijatumika inavyopaswa. Kwa sababu tunayo ardhi nzuri inayokubali kilimo cha aina yoyote na bado hatujaitumia. Mhe. Spika, Zanzibar kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh Salmin jana katika *geographical position* yake iko katika hali nzuri. Kwa hivyo, kama tutaitumia *geographical position* Zanzibar hapa kibiashara na tukaweza kuitumia Zanzibar kufanya biashara na nchi nyengine za Afrika Mashariki na Kati.

Kutokana na hali hiyo, tunaweza tukafanya biashara nzuri, lakini bado hadi sasa hatujaweza kuyatumia maeneo ya visiwa vyetu kwa ajili ya kuikuza Zanzibar kibiashara.

Mhe. Spika, suala la tatu ni kuhusu biashara ya utalii bado. Juzi nilimsikia Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii, alisema kwamba utalii ulipokuja Zanzibar tuliuvamia tu. Kwa mfano, pahala ambapo alipaswa pajengwe hoteli ya nyota tano, leo tunajenga *Bungalow* na sehemu iliyopaswa kujengwa *Bungalow* inajengwa hoteli ya nyota tano, yaani ile kukubali tu kuvamia kuchukua aliyekuwa ndiye na siye na hili ni tatizo.

Kwa hivyo, kama tungeliweza ku-*control* utalii basi peke yake ungeliendesha visiwa hivi vya Zanzibar. Kwa mfano, kuna nchi za wenzetu hawana chochote walichonacho isipokuwa utalii na wanapiga hatua kubwa kabisa.

Mhe. Spika, nilipokuwa kijana kwa kweli nilikuwa ni mtembezi sana wa nchi hizi za Congo. Siku moja nilikwenda Congo nikala pilau na wanajua kule kupika, lakini badala ya kutia pilipili manga wao walitia kokwa za papai, wakati nikiendelea kula nikazitafuna na nilipouliza, niliambiwa ni kokwa za papai, sehemu za Bukavu.
Kwa hivyo, kama tungeweza kuchukua hizi *spice*, kwa sababu Zanzibar ni *Spice Island*. Suala la msingi ni kuangalia namna ya kuviimarisha katika kulitumia Soko la Afrika. Kwa sababu leo Mawaziri wetu ni wazuri sana kwa kwenda Urusi na sehemu nyengine tofauti. Mhe. Spika, kama tungelitumia Soko la Afrika ya Mashariki na Kati, basi ninakuhakikishia *spice* peke yake zingeliweza kuiendesha Zanzibar, lakini leo ziko pahala gani.

Vile vile suala jengine tulilonalo ambalo ni zuri kwa nchi yetu ni *political stability*. Hali hii ya kisiasa tuliyonayo kama tungeliitumia, ingawa kuna wengine wanajaribu kuichafua na nitawaombea dua baadaye. Kwa kweli hali hii nzuri tungeliitumia kujenga pamoja na kuimarisha uchumi wetu basi tungelikuwa tuko mbali, lakini kila nchi ikiwa hivi ndio tunazidi kucheza taarab na wala hatufanyikazi ya kujenga uchumi.

Mhe. Spika, tatizo letu ni Muungano. Kwa kweli tukubali kwamba Muungano tulionao unatuyumbisha kiuchumi. Mhe. Waziri Kiongozi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine tusikilize vizuri kwamba Muungano huu hauna maslahi kwetu kiuchumi. Kutokana na hali hiyo, tukae jamani, tumsalie Mtume (S.A.W) tulirekebishe tatizo hili, kama si hivyo utatuumiza *(Makofi)*.

Suala jengine bado hatujawa na sera nzuri na wala hatutaki. Kwa sababu leo tumezungukwa na bahari, hivi Mwanza wanajenga viwanda. Mhe. Spika, ni kweli hakuna mtu mwenye kuhitaji samaki wetu Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji. Kwa mfano, meli moja juzi ilikwenda kule na tuliambiwa imechukua mabilioni nyinyi tu, kwa hivyo sisi tunashindwa kujenga viwanda.

Kwa hiyo, tunachokiomba hapa ni kwamba kama kila wilaya kungekuwa na kiwanda kimoja tu basi tungepata ajira nyingi tu na lichukuweni hilo Awamu ya Sita na mlifanyiekazi.

Mwisho naiomba serikali iwe na utaratibu mzuri wa kuzisimamia hizi fedha. Suala la msingi lililoonekana ni kwamba hizi fedha hazina usimamizi, yaani kuna wizi huko kwenye mawizara na lazima tufanyekazi kubwa sana, kuhakikisha kwamba fedha hizi kidogo tulizonazo zinakuwa na udhibiti mzuri. Katika hilo basi tuimarishe *Office Tag* pamoja na kamati zetu, ili tuweze kuisimamia serikali kutokana na mambo hayo ya ubadhirifu.

Mhe. Spika, nataka nikuombee dua Mwenyezi Mungu akujaalie hekima, maishi marefu, aijaalie nchi yetu ya Zanzibar ipate maendeleo na wale wote waliokusudia kuwanyima watu vitambulisho Mwenyezi Mungu awatie mchanga macho *(Kicheko/Makofi)*.

Ahsante sana.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, ahsante kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii ya kuchangia na nitajitahidi sana Mhe. Spika kuchangia kwa muda mdogo, ili nisikupotezee muda wako.

Kwa kuanza mchango wangu nianzie kwenye ukurasa wa 12 kuhusu mfumko wa bei. Kwa kweli mfumo wa bei ni kitu kinachotisha na hupelekea nchi yoyote kupata misusuko kama bei za bidhaa hazina msimamo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelezo ya kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Serikali ukurasa wa 12 kifungu 21 kimezungumzia kuhusu Mfumko wa Bei. Bei ambazo zinasababisha mfumko kwa Zanzibar hasa kwa bidhaa za chakula na kiteweo"

Sasa viti hivi vyote vimo kwenye mazingira yetu. Kwa maana hiyo, kinachohitajika ni usimamizi mzuri. Mhe. Spika, hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kushughulikia kushuka kwa bei za bidhaa isipokuwa Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Kwa kweli kama tutajitahidi kulima na tukapewa dhana pamoja na pembejeo, basi mfumko wa bei unaweza kushuka kila siku. Kwa sababu kama mfumko wa bei umefikia kiwango hiki, yaani ni kiwango kikubwa kutokana na kwamba ni mahitaji ya matumizi ya kila siku *(Makofi).*

Mhe. Spika, Bajeti ya Serikali inasema kwamba Kauli Mbiu yake ni Kujenga Miundombinu ya Kilimo na Utalii. Hii ni kauli mbiu nzuri sana.

Lakini tunapopanga mipango hatufanyi mapitio tunaona kwa kiwango gani tumefanikisha. Kwa mfano, mwaka jana Mhe. Waziri katika hotuba yako ulizungumza kwamba baadhi ya pembejeo tutapunguza bei, kama vile mbolea asilimia 50 itapunguzwa kwenye bei ya mbolea. Mhe. Spika, jambo la kushangaza maafisa hawakushughulikia vile ulivyokusudia wewe, yaani kauli ilikuwepo, lakini utekelezaji kwa upande wa maafisa haukuridhisha.

Sasa haya tunapoyapanga tuhakikishe kwamba wapo wasimamizi wazuri. Mhe. Spika, kinachokosena kwa serikali inawaamini sana Wakuu wa Wilaya pamoja na Masheha katika kushughulikia masuala hayo. Lakini baadhi ya wilaya kuna Wakuu wa Wilaya pamoja na Masheha wao hawashughulikii hayo.

Kwa mfano, mzuri zilitolewa mbegu ndogo ambazo ni nzuri, lakini sijui nani miongoni mwetu sisi Wajumbe wa Baraza hili, maana tuachilie upande ule labda wako mbali na masheha na hata sisi wenye masheha *Wallahi* hatukujua mbegu hizo zimekwenda kwa nini *(Makofi).*

Sasa lazima tuone kwamba serikali inapotoa hoja au kuzungumza kitu ni vyema kuwashirikisha watu, ili kuona kwamba wananchi wanafanikiwa katika mazungumzo hayo.

Mhe. Spika, jambo jengine kuhusiana na huu mfumko wa bei na upunguzaji wake kwenye maeneo ya uvuvi. Kwa kweli Samaki wapo, lakini sijui kwa nini kiteweo kiwe ghali sana, pamoja na kwamba utalii unachangia kuchukua sehemu kubwa ya bidhaa za samaki na mboga mboga.

Lakini bado serikali haijatuekea mipango mizuri ya kuvua kwenye maeneo ya maji mengi, isipokuwa maeneo yanayoimarika ndiyo hayo ya maji madogo, ya kugombana baina ya Maafisa wa Idara ya Uvuvi na wavuvi, maana ataambiwa mvuvi asivue kwa nyavu ya nchi mbili, lakini nyavu ya nchi nne haruhusiwi na matokeo yake ni ugomvi tu.

Suala la kushangaza ni kwamba miradi mingi ikiwemo *MACEMP* na mingine inatofa fedha nyingi sana, lakini hakuna utaratibu wa kutoa na wala hujui nani wanaopewa.

Kwa sababu zana za uvuvi zaidi zinalengwa kwa wale watu ambao wako ukanda wa pwani, ili kuhifadhi mazingira. Lakini wanaopata hivyo vifaa au zana ni watu ambao wako katikati ya kisiwa, yaani hakuna bahari wala mito. Kwa hivyo, hatujui tunachokipanga na wala tunachokifanya na kutokana na hali hiyo hatuendi.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira katika mipango yako mara hii umkamate sana Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi au umsimamie, ili atekeleze yale ambayo wananchi wanajengea matumaini.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu kodi ya ardhi. Katika ukurasa wa 26 suala la kodi ya ardhi limezungumziwa sana kuhusu mapitio na kuweka viwango vya kodi ya ardhi. Kwa kweli tunashukuru sana kwamba ardhi inachangia kwa kiasi kikubwa cha mapato. Lakini hivi sasa ukitaka kumuudhi mwenzio mwenye kusimamia ardhi uchangie mambo ya ardhi utamuudhi na wala si peke yake.

Kwa sababu ardhi, hivi sasa imekuwa na mgogoro mkubwa. Mgogoro huu katika kusuluhisha kwake hauwezi Mhe. Waziri wala Mhe. Rais. Mhe. Spika, kuna mfano hai wa kesi mmoja ya rafiki yangu na wala simtaji kwa sababu kanuni inakataza.

Mgogoro huo ulianza wilayani ukashinda, ukapelekwa mkoani ukajadiliwa ukashinda, ukapelekwa kwa Mhe. Waziri Kiongozi umejadiliwa nako ukashinda, mwisho ukapelekwa kwa Mhe. Rais umeshinda, hatimaye umerudi tena mkoani. Kutokana na hali hiyo, hivi nani anayeweza kutatua mgogoro wa ardhi kwa kuoneana muhali, kwa kweli hakuna na ardhi inakwenda.

Mhe. Spika, kule kwa wenzetu sakata la aliyekuwa Mhe. Waziri Mkuu. Lakini hapa kwetu lipo tatizo kubwa kuliko lile, yaani hapa kuna hujuma. Kwa mfano, kuhujumu kitu maana yake unakiona kwamba hiki kitamfaa mtu fulani, mwengine akatumia mbinu pamoja na Katiba kwa ajili ya kumnyang'anya, ili utumie wewe na hii ndio hujuma. Kwa kweli watu wanajilimbikizia ardhi kwa wingi na wala haijulikani wanaifanyia nini, yaani wanaweka *(Makofi)*.

Kwa hivyo, ni lazima kupitia pamoja na kukagua ardhi ili tupate kodi nzuri basi tuwe makini na hii sio kazi nyepesi. Kwa mfano, hivi karibuni Mwenyekiti wangu wa CCM Mkoa wa Kaskazini alipeleka kwa Mhe. Rais siku ya Mkutano wa Mkokotoni, alisema kwamba nyote ni watu wazima kaeni mzungumze nakupeni mtu mzima Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo awe Mwenyekiti.

Kwa bahati nzuri kikao kikafanywa cha Wakuu wa Mkoa wa Kaskazini na mimi nilikuwemo, tulijadili na kwa kweli kila mtu alihisi kuna haja ya kuzungumza na Waheshimiwa Mawaziri walikuwepo wanaoshughulikia masuala ya ardhi pamoja na kilimo. Mhe. Spika, tuliambizana kwamba hali hii tuifanyie kikao na tuone, lakini tulipendekeza iundwe kamati kwa ajili ya kuliondoa hili tatizo.

Ninadhani Mhe. Naibu Waziri Kiongozi hajapata nafasi ya kutoa taarifa. Lakini mpaka leo kamati haijaundwa na wala jibu halikupatikana na hadi hivi sasa wananchi hawajui wafanye nini, kwa sababu tayari wameshamtuma Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini pamoja na sisi wakubwa na mimi si mdogo kwa kule *(Makofi)*.

Mhe. Spika, isitoshe hujuma inayofanyika maeneo mengi ya ardhi yanauzwa, lakini katika kuuzwa kuna utaratibu wa asilimia 10 ipelekwe Halmashauri, ili mapato yale yaisaidie jamii.

Wallahi hivi karibuni kuna sehemu moja iliuzwa shilingi milioni 100/-, nilichukua hatua ya kumpigia simu Mhe. Mkuu wa Wilaya na nilimuuliza asilimia 10 ya shilingi milioni 100/-, yaani zaidi ya shilingi milioni 10/- zitapatikana, alinijibu hazipatikani na kama zitapatikana ni shilingi 800,000/-. Je, hii ni hujuma kutoka shilingi milioni 10, ukapate shilingi 800,000/- *(Makofi)*.

Katika kulizungumza hili tusifanye mchezo kwani mimi nalizungumza hili, lakini naumwa kweli. Naumwa kwa sababu sehemu ya iliyouzwa ya Muyuni kwa Unguja hii ni sehemu pekee yenye ubovu wa barabara. Siku moja Mhe. Rais aliitwa kwa ajili ya kwenda kufungua skuli na alikuwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali anatosha, lakini wananchi wakaona si vyema bora

tumwite na Mhe. Rais naye aje, ili aione hali ya barabara kwa lengo la kupunguza tatizo.

Kwa bahati mbaya aliyetumwa aliitwa chumbani pamoja na mimi basi ifanyiwe matengenezo, lakini haijafanyiwa kwa sababu na yeye hana fedha na wala Mhe. Waziri anayehusika hushughulikii. Sasa sijui Mhe. Rais wakati anapokwenda safari watu hawa huchukua kundi la magari, kwa sababu kwetu chakula cha mchana hakikuwepo, labda walikuwa wakimfuata kwa ajili ya chakula cha mchana *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, nilidhani wale Mawaziri husika wataishughulikia suala lile, lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika. Katika mambo yanayoniudhi ni kwamba Mhe. Rais wakati anapotoa kauli au agizo na halafu lisitekelezwe kwa kweli suala hilo linaniuma. Kwa sababu Rais wa nchi anao uwezo wa kuagiza jambo lifanywe kwa wale ambao amewateua kwa ajili ya kumsaidia kazi, lakini hawamsaidii.

Kwa hivyo, siku hizi bora awe na gari yake pamoja na gari ya ulinzi na usalama basi zinatosha. Kwa sababu ile kazi ambayo anafikiria watamsaidia hawaifanyi na kila mmoja anashughulika na lake na huo si utaratibu mzuri. Kutokana na hali hiyo, mnampaka matope Rais ambaye amewateua watu wenye uwezo, mbona mimi hajaniteua kwa sababu sina uwezo *(Kicheko/Makofi)*.

Lakini kumbe wale aliowateua amewasogezea kwenye chupa ya asali basi, sasa tutakwenda wapi. Kwa kweli mapato ya nchi hayaji, uchumi haukui na hapa tutakuwa tunaimba tu, kwani hapa kila mtu kama utamweka na mwenziwe uweke huo mradi na fedha zije basi hazipatikani. Hivi sasa watu wataalamu kwa kuiba, tena utaalamu wa hali ya juu bila ya kuona haya, yaani aibu moja kwa moja.

Kwa hivyo, nilipoiona hoja hii ya Kupitia Viwango na Kodi ya Ardhi ninadhani tunaweza tukafika sehemu tukaaminiana, kwa sababu fedha zinakwenda nyingi.

Mhe. Spika, hivi leo nimepigiwa simu wakati nilipokuwa na Mhe. Ame Ussi Juma kwamba iko sehemu imefika shilingi milioni 800/-. Kwa mujibu wa utaratibu katika shilingi milioni 800/- karibu shilingi milioni 80/- ziingizwe Halmashauri, sijui kama hazitoingizwa shilingi 800,000/-.

Sasa tunafanya nini. kwa sababu azma ya Mapinduzi nilivyoifahamu kwamba Wakoloni walikuwa wanaichukua ardhi kwa maslahi yao. Kwa bahati nzuri baada ya Mapinduzi kufanikiwa nilishuhudia wale watu waliokabidhiwa eka tatu. Sasa leo tunazitoa wenyewe na huku watoto wetu watakuja kuandika

wamenyang'anywa ardhi na Waarabu sehemu ya ukanda wa pwani. Mhe. Spika, kwa kweli tunaitoa ardhi kiholela na kujenga tamaa kubwa.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anifafanulie hasa miradi iliyopitishwa na Vitega Uchumi kwa mwaka huu kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini ni mingapi na zile fedha ambazo wamelipa. Kwa sababu hawawezi kupewa ardhi bila ya kutoa fedha, kwa maana hiyo jumla ni kiasi gani. Takwimu hizo nataka aniletee kwa karatasi, yaani maandishi sahihi. Ametwambia tu pale Mtondooni hivi na hivi lazima tuone kwamba kiasi gani na miradi hiyo ni ya aina gani ili ile ardhi ambayo watu wengine wameiweka tu hawana kazi nayo basi irudi mikononi kwa wananchi, kwa sababu hawakuinunua wameichukua kwa mujibu wa katiba na kuwababaisha tu wananchi, kwa sababu mwananchi akiambiwa kwa mujibu wa katiba kifungu kumi na tano kiko hivi mlipwe fidia, mnazi mia tano bei ya zamani wakati sasa hivi ni bei ya soko, si wanawanyang'anya. Kwa hivyo, muda wa kunyang'anyana sasa hivi haupo, watu watakuja kupigana migogoro ikizidi hatima yake vita nafikiri nimefahamika.

Mhe. Spika: Mheshimiwa muda.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, kwa kuwa muda haupo nizungumzie miradi ya wananchi hii tumedhulumiwa sana, lakini hivi karibuni mimi na wewe Mhe. Spika tulipata safari ya kwenda Nairobi tukaona wenzetu namna gani fedha zao hazipotei, CDF ina utaratibu wa kumshughulikia kila mtu katika eneo lake namna ya kupatikana kwa pesa na matumizi yake, kwa hivyo litakuwa jambo la busara sana kama mfuko wa maendeleo wa jimbo utakubaliwa na kufanya kazi, hatoiba sheha wala diwani kwa sababu fedha zote zinazopatikana makusanyo ya eneo lile yatakuwa yako mikononi mwa kamati ya maendeleo ya jimbo. Kwa hivyo, CDF kuundwa kwake si kitu cha kudharauliwa nina mengi, lakini siku zipo za kuchangia basi nitakuja kufafanua mfuko wa maendeleo yw jimbo ili tuepukane na migogoro lakini pia kudumaa kwa maendeleo.

Mhe. Spika, nakushukuru mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Matemwe tunaunga mkono bajeti mia juu ya mia, maana ni yetu ya serikali yetu ya Chama chetu. Ahsante sana.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Spika, sina budi kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu subuhanah wataala, kwa kutuwezesha kufikia siku hii ya leo tukawa tuko hai na wale ambao ni wenzetu wameshatangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awape vilalo vyema na awasamehe yale waliyokosea.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa kuwa muda ni mfupi mno nitaheshimu muda huo, lakini na mimi niende tu kidogo katika kilimo. Mwenyezi Mungu sisi katujaalia kwamba nchi yetu ni nchi ya visiwa tena ni vidogo vidogo na hapo zamani hii nchi ilikuwa na rutba nyingi ama kwa sababu watu walikuwa wachache, kwa hivyo eneo la kulima likawa ni kubwa zaidi kuliko sasa na wakati huo ilikuwa labda kuna utaratibu wa hali ya kuwa Wazanzibar ni wao wenyewe tu hawakuingiliwa na maeneo mengine na badala yake wakawa na nafasi kubwa zaidi ya kuitumia ardhi yao katika masuala ya kilimo.

Lakini lilipokuja suala la Zanzibar kuondosha *passport* nadhani limechangia kwa kiasi kikubwa kwamba maeneo yetu yahodhiwe na watu wengine tena maeneo makubwa mpaka maeneo ya kilimo kwa makaazi ya watu, sasa lakini hata hivyo ardhi tuliyokuwa nayo mimi nadhani kuna utaratibu ambao haujakuwa mzuri tunaweza kuitumia kwa kilimo na tukaweza kupata manufaa makubwa na ikawa tunasaidia maisha yetu ya kila siku. Lakini kulingana na hali ilivyo wananchi kwa sasa kwa sababu wanalima eneo kubwa sana, lakini kipato ni kidogo sana, yupo mjumbe mmoja hapa alisema kwa kuwa kuna ukulima wa matrekta haya yaliyokuwa sio ya bei kubwa, lakini hata ya mikono yapo haya yangepatikana yakasaidia wananchi wetu kulima na wakaepukana ile kulima kwa kifua muda mwingi halafu kipato kikawa kidogo.

Mhe. Spika, ni vyema serikali ifikirie mkulima wa kawaida ambae ni mnyonge na ambae kwa kifua tu peke yake hawezi kufikia malengo, lakini hapa kinachohitajika kwa sasa ni taaluma, mimi nimshauri Mhe. Waziri hapa Mhe. Hija alisema kwamba kuna milioni 430 kwa ajili ya kichaa cha hawa mbwa, sasa mimi naona hapa hatuna mbwa wengi kama ingelikuwa milioni 430 hizi ni kama kule nchi za magharibi kwa sababu wenzetu wazungu mbwa ni sehemu ya familia zao, lakini ukichukulia sisi hapa hata mbwa mia mbili hawafiki sasa pesa zote hizi hapa kuna mushkeli mkubwa kwamba pesa hizi zinaweza kutumika kwa malengo hayo.

Kwanza hao mbwa wanaopata kichaa ni wangapi na hawa mbwa katika nchi hii ni wangapi, mbwa wengi wameangamizwa kwa matokeo haya haya wamepigwa wakauliwa, kwa hivyo mbwa ni wachache mno kiasi kwamba haikustahili hata kidogo fedha zate hizi kuchukuliwa zikatiwa katika mradi huu. Sasa mimi naishauri serikali na namshauri Waziri badala ya fedha hizi kuziweka huku bora ziwekwe kwa hii programu ya elimu kwa wakulima nadhani wakulima wetu sasa hivi wanahitaji elimu zaidi, kwa hivyo kama pesa hizi zitahamishiwa huku, basi Wizara itakuwa imefanya jambo la busara lakini wakulima vile vile tatizo lao ni elimu, watu wanajitahidi kulima lakini wanalima walivyozoea na wanavyofahamu wao hawana taaluma yoyote.

Kwa hivyo, naishauri serikali kwamba ipo haja sasa badala ya kushughulikia majibwa sasa hivi zichukuliwe na ziwekwe kwenye hii program ya elimu kwa wakulima itatusaidia mno kwa sababu watu wetu wanalima tu wanavyoona sawa basi, hawapati taaluma na ndio maana mazao yanapungua na halafu wanakuwa wanaumia mno hawapati tijara ya kile wanachokilima. Kwa sababu bajeti hii ni bajeti ya mwananchi, kwa hivyo mlivyopanga mmepanga halafu mkaona kwamba bado iletwe barazani, ijadiliwe yaani mpate mawazo ya wajumbe kwamba wapi tuboreshe na wapi tupunguze nini. Mimi nadhani katika hili uone kwamba lina umuhimu hao mbwa tuwaache kwanza halafu tushughulikie kilimo ambacho kimetajwa hapa kwamba bajeti hii inashughulikia kilimo na utalii, sasa tumwezeshe na waziri wa kilimo tusimpe mzigo mkubwa.

Mhe. Spika, juzi nilikwenda bandarini pale nikaona mahonda mengi sana nilipouliza nikaambiwa yale ni ya Wizara ya Kilimo na wanategemewa kupewa mabwana shamba, lakini ikiwa watawezeshwa na kupewa haya mabwana shamba kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima halafu na hizi pesa wapewe ili ziwawezeshe kufanya kazi hiyo, naamini tutafikia pahali pazuri sana. Kwa hivyo kupanga ni kuchagua naona jambo hili ni zuri zaidi kuliko kufikiria mbwa ambao kuwa hawapo.

Mhe. Spika, nije katika suala la kilimo cha mwani akina mama wengi katika visiwa hivi sasa hivi wanajitafutia rizki zao kupitia kilimo hiki cha mwani, lakini tatizo linalojitokeza na katika yale maeneo ambayo kilimo hiki kinalimwa wanalalamikia kwamba bei bado ni ndogo mno na kweli bei ni ndogo mno kiasi kwamba unamuona mwana mama anachezea maji toka kwenye mguu mpaka maji yanafikia kiunoni yeye yuko baharini tu anapanda mwani, lakini akivuna mwani wake anakwenda kupewa shilingi mia mbili kwa kilo moja tena mwani wenyewe mkavu, sasa hii ni dhulma hamsaidii anajutia kwa nini akapanda, lakini afanye nini mama yule anakuwa hana la kufanya inabidi tu ile kazi afanye.

Sasa mimi naishauri serikali kwamba ione umuhimu wa kumsaidia huyu mkulima wa kilimo cha mwani na itamsaidiaje, mimi nafikiria ipunguze ushuru kwa makampuni haya ambayo yamewekeza katika mwani ili serikali iweze kumpangia bei moja kwa moja mkulima wa mwani, hii bei ipangwe na serikali kutokana na ushuru ambao wamewapunguzia hawa makampuni, ili mkulima wa mwani ajue kwamba bei hii inamsaidia vipi na imetoka kwenye serikali kwa hivyo yeye awe tena hana uwezo wa kubadilisha kwa sababu wao wanapata faida kubwa, lakini hapa anayeathirika ni mkulima. Kama hatutomuonea huduma mkulima huyu itakuwa hatukumfanyia haki, kwa hivyo haya maneno tunayokuja kusema hapa itakuwa kama tunawafanyia kejeli tu.

Sasa mimi naamini Dk. Mwinyihaji ni mtu mmoja mwelewa na ni mtu ambae ni Mzanzibari na miongoni mwa ndugu zake inawezekana wapo wengine wanapanda mwani, kwa hili suala liangalie na nadhani tunaweza kufikia pahali pazuri. Huu sio wakati tena wa kulumbana kisiasa ni wakati wa kuangalia zaidi wananchi tumeshalumbana sana na hakuna faida yoyote tuliyoipata isipokuwa kuwatia matatizo wananchi wetu, sasa tufike pahala tukubaliane na tukishakubaliana tutende yale ambayo tumekubaliana kwa sababu hii kupiga piga makofi halafu ikawa hakuna linalotendeka pia haitusaidii.

Mhe. Spika, Mhe. Muhidyn Moh'd Muhidyn alisema lile suala la utawala bora kwa hivyo tufike pahala tuone kwamba nchi hii kila mtu ana haki ya kutoa mawazo yake akiwa ndani ya serikali au nje ya serikali, kwa hivyo hapa tunachotakiwa kufanya ni kupata fursa ya kutoa mawazo hayo midam tumekubaliana kuwepo na mfumo wa vyama vingi, basi ile haki ya utawala bora itabaki nafasi yake, sisi leo tunasema hapa na tukitoka hapa ndani tukikutana na Janjawid tunawapa maelezo badala yake wanatesa watu bure halafu haki inakuwa haitendeki tukija hapa tunalumbana na kugombana.

Mhe. Spika, sisi tumezaliwa na wazazi wetu na wazazi wengine wameshatangulia mbele ya haki hawapo kwa hivyo sisi tuna watoto tunawarisisha nini katika visiwa hivi, tunawarisisha chuki, fitna, ugomvi, wasielewane katika visiwa hivi, sasa kila tukifanya hivyo ndio tunatoa fursa kwa hao tunaosema ndugu zetu waendelee kututawala ndani ya nchi yetu na kuchukua haki zetu halafu sisi tunakaa hapa na kulalamika. Hakuna kitu kikubwa zaidi kuliko kuelewana, tukishaelewana naamini mambo yetu yote yatakwenda vizuri, lakini kuelewana huku hakutokuja mpaka sote tuwe na nia safi sio mmoja akamate hatamu halafu na mwengine aburure tu sasa wengi hivyo watakuwa hawakubali.

Mhe. Spika, mimi nimefarijika sana kusikia hotuba ya bajeti ya Mhe. Said Ali Mbarouk ambayo imemwelekeza vizuri mno Mhe. Dk. Mwinyihaji na kumbe inatoa kasoro mpaka yeye mwenyewe jinsi ya ahadi ambazo amezitoa hapo siku za nyuma, lakini hazikufikiwa na hazikutekelezwa na hii ni athari ya ahadi zile. Bajeti hii lazima iangalie ukweli kama kuna kitu kimesemwa, lazima kitekelezwe na ameonyesha vitu vingi tu Mhe. Said Ali Mbarouk, sasa na mimi namwomba Mhe. Waziri ile bajeti aichukue imsaidie katika masuala ya kumkomboa mwananchi wa nchi hii kwa sababu kila mmoja ana haki ya kumtafutia unafuu mwananchi wake, ndio maana kukawa na wawakilishi wa majimbo na kila jimbo limetoa mwakilishi wake kuja hapa kusudi kuwasemea watu wake. Kwa hivyo, itakuwa si jambo jema jambo zuri lolote likisemwa na mpinzani, basi lichukuliwe ni nani aliyesema huyo mpizani mwenyewe hapo tutakuwa hatufikii pahali pazuri, lakini ikiwa jambo ni zuri na linaelekea kwa maslahi ya nchi, ni lazima lipewe kipaumbele ili lishughulikiwe.

Mhe. Spika, namwomba Mhe. Waziri awe na umakini mzuri sana katika kuichambua bajeti ya Mhe. Waziri Kivuli ili kusudi ikishirikiana na bajeti yako iweze kupata mwongozo ambao utatuletea unafuu kwa watu wetu ndani ya visiwa hivi, leo tunaathirika sana.

Mhe. Spika, sasa nije katika huu mfumo wa muungano sisi hapa Zanzibar kama wenzangu walivyosema hii nchi yetu sisi ni ndogo na Mwenyezi Mungu vile vile katufanya kidogo, kwa sababu atakachotupa ndani ya nchi yetu iwe kinatutosheleza sisi wenyewe, lakini tumejitia imani kubwa na mapenzi makubwa leo ndio tunalalamika kwa sababu tunataka ndugu, sasa ndugu wametufikisha hapa hawatuoneani tena imani na badala yake sisi tumekuwa tukiwalalamikia wao, wao wanakaza kamba yao na sisi tunaendelea kuathirika.

Mhe. Spika, hii Zanzibar ni nchi na tulipoungana tuliungana kama nchi mbili zilizo huru kabisa na mambo mengi watu walikubaliana enzi hizo baada ya kuungana, moja ya makubaliano hayo ni kila nchi kusimamia uchumi wake sababu ya wananchi wake matokeo yake zile daftari zilizokuwa zikifanywa hapa zote zimeuliwa, watu walikuwa wanakuja kutoka maeneo mbali mbali kama vile Kenya, Uganda na nchi nyengine nyingi tu za jirani wanakuja kutafuta bidhaa zao. Leo watu wote hao pamoja na sisi kuna watu wanatoka ndani ya jimbo langu wanakwenda Dar es Salaam kuchukua bidhaa zao wanakwenda kuuza kule Tumbe, sasa hili ni tatizo kwa nini biashara zimeuliwa, lakini zinauliwa kwa sababu ya kuimarisha upande mmoja na zimeuliwa kwa sababu tunaonekana sisi tutakachogaiwa chochote kile tumeridhika sasa tusiridhike katika hali hii kwa sababu leo tupo sisi hayo yameshatushinda, je watoto wataweza je kuja kuikomboa nchi yetu sisi tulioikwamisha ndio tuikwamue.

Mhe. Spika, ikiwa ndugu hana huruma na wewe kaa mbali mbali kwani sisi tukijitenga na ndugu hawa tukabaki kwa ule umoja wetu, lakini mambo yetu tujiandae tukiwa tunafanya wenyewe tutakuwa na dhambi au tutakuwa tumemkosea Mungu, hii ni nchi yetu na ni nchi ambayo haihitaji kurithiwa na watu isiyowahusu. Hii ni nchi ya Wazanzibari na Mwenyezi Mungu katujaalia neema nyingi tu leo hivi kila kitu kimeharibika kwa sababu ya kuja kuingiliwa ingiliwa utamaduni wenyewe umeharibika, kila kitu kimeharibika hapa kwa sababu ya kuingiliwa mno na hao ndugu zetu matokeo yake wao ndio wamekamata nafasi kubwa zaidi katika nchi yetu kuliko sisi wenyewe hata ukienda kwenye maofisi na maidara au mahoteli unakuta wao ndio wengi kuliko sisi wenyewe, halafu tukisema hapa tunaambiwa hatutaki kazi Wazanzibari ni wavivu sio wavivu ni hali halisi yenyewe ya mambo ilivyo.

Mhe. Spika: Muda.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Spika, la mwisho niseme tu kwamba ili uchumi wetu uimarike miundo mbinu lazima ipewe nafasi kubwa, kule Pemba kuna kile kiwanja cha Ndege cha Karume kile kiwanja labda utafikiri hakitui ndege, utasema labda zile ndege za wakimbizi wanakuja wakitua pale halafu wanakimbia wanatafutwa makwao hakina hadhi ya aina yoyote. Sasa Mhe. Spika, Pemba nako kuna watu, mimi sizungumzii suala la ubaguzi, lakini nakusudia kwamba kinachofanywa hapa kizuri na kule kifanywe na kile kinachofanywa kule kizuri na hapa Unguja kifanywe kwa sababu hivi vyote ni visiwa vya nchi moja, tusiwafanye waliokuwa sio wasemaji wakasema.

Kwa hivyo mimi nadhani tufike pahali tuone yaliyofanywa Unguja kwa sababu ya watu na Pemba ifanywe vile vile kwa sababu ya watu, kwa sababu sisi ni watu na tuko kule, tunapolalamikia usawa inakuwa ni kutokana na yale madhila tunayoyapata kule kwa hivyo watu wasituchukulie kwamba kulalamika kwetu tunahubiri mgawanyiko, sisi hatuhubiri huko kwa sababu Mwenyezi Mungu ameshatuumba kuwa wamoja vyovyote itakavyokuwa sisi ni wamoja tu kwa hali yoyote ile. Lakini tunachukulia ule usawa wa madaraka, usawa wa mambo mbali mbali yakifanyika hayo tutafanya kazi kwa pamoja na nchi yetu itaneemeka.

Mhe. Spika, mimi wakati nasoma kwa Mhe. Dadi Faki Dadi chuoni kwake alikuwa mwalimu wangu mie alinifundisha mambo mengi sana Mhe. Dadi Faki Dadi, lakini katika darasa lake mimi nilikuwa nafahamu vizuri tu, alikuwa anatwambia kwamba bila ya umoja, bila ya mshikamano basi nchi hiyo haiwezi kupata neema hata siku moja kwa sababu Mwenyezi Mungu amehimiza umoja hilo nimefundishwa na Mhe. Dadi Faki Dadi na nashukuru sana yeye yumo humu ndani anasikia. Kwa hivyo nitafarijika sana na yeye akija kutilia mkazo kwamba umoja unahitajika katika kufanya mambo yetu hasa katika visiwa hivi, lakini ikiwa na yeye atakaa katika laini kama alivyosema Mhe. Ame Mati Wadi tutafika pabaya na hatutokwenda vizuri, mimi nadhani tumefika pahali pazuri, kwa hivyo uzuri huu tuuimarishe na tuuchukue kama changamoto wa yale tuliyokosea ili tufike mahali pazuri kila mmoja awe na haki ya kushiriki na kutoa mchango katika nchi yake kwa maslahi ya nchi na vizazi vyetu.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi kuweza kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi, kwanza sina budi kumpongeza Mhe. Said Ali Mbarouk kwa maelezo yake mazuri na kutueleza sisi sote mambo ambayo yanahitajika katika suala zima la bajeti. Kwa hivyo namwomba Mhe. Waziri hotuba ile ya Mhe. Said Ali Mbarouk aizingatie vizuri na aangalie yale ambayo ameshauriwa na yale ambayo yanahitaji kutekelezwa.

Mimi sitaki kuzungumza sana juu ya bajeti kwa sababu imeshazungumzwa kwa muda mrefu takriban waliozungumza wote wanalenga kwenye ncha ile ile, lakini mimi nitazunguka zunguka kwenye sehemu mbali mbali hasa kwenye mapungufu ambayo nimeyaona.

Mhe. Spika, moja katika mapungufu ya bajeti hii nimegundua au tumegundua wakati tulipokuwa tunazunguka kuona hali halisi ya kamati zetu kuna mambo yamejitokeza kwa hivyo naona sina budi kulileta suala hili hapa mbele yako, mapungufu ambayo yalijitokeza wakati wa makadirio na mapato na matumizi, ni kwamba wanapoleta ripoti zao hawatimizi kipindi chao mpaka kufikia mwezi wa juni jambo ambalo tunasema mwisho wa bajeti ni mwezi wa juni, sasa hili suala limejitokeza katika ripoti nyingi za sekta na maidara mbali mbali wanamalizia ama mwezi wa Machi wengine Aprili au Mei, lakini hawatimizi mpaka mwisho wa Juni. Kwa hivyo, hilo namwomba Mhe. Waziri alinukuu na alione kwamba hiyo ni kasoro ya bajeti.

Lakini isitoshe katika hilo hilo wao waone kwamba japokuwa hawakupewa fedha za *other charges*, lakini wakati ule ule wafahamu kwamba mawizara yote, maidara yote pamoja na sekta zote wanapewa mishahara. Kwa hivyo, kama mawizara na maidara wanapewa mishahara katika sekta zote ni wajibu mishahara ile ionyeshwe katika bajeti zao wanazokuja nazo kwa hivyo hilo nataka kukuambia Mhe. Waziri ulione na ulifanyie kazi.

Mhe. Spika, jambo langu la pili nataka nizungumzie juu ya suala la mfuko wa barabara. Suala hili la mfuko wa barabara madhumuni yake hasa ni suala zima la matengenezo ya barabara, lakini mara nyingi katika fedha hizi za mfuko wa barabara haziendeshwi kama vile zilivyopangwa, mfuko huu wa barabara unatumika kwa shughuli nyengine ambazo sio za matengenezo ya barabara kwa sababu fedha zile ni kwa matengenezo ya barabara. Sasa wanaacha matengenezo fedha zile na zikatafutwa fedha nyengine zikachukuliwa katika *other charges* na watu wakafanya shughuli nyengine, kwa hivyo suala hili nataka nimwambie Mhe. Waziri alione kwamba ni moja katika kasoro na mfuko wa barabara, uende kwa maslahi ya mfuko wa barabara pasichukuliwe kwenye *other charges* ikawa mfano anajenga maana kuna kutengeneza barabara na kujenga barabara mpya, hivyo ndio inavyofanyika.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza ni suala la Shirika la Bandari upande mmoja wa bandari ambao unafikia meli za SEPIDEH pamoja na SEA EXPRESS kuna kibanda ambacho watu wanafika pale kwa kupumzika kwa ajili ya jua na mvua, kwa upande huu kitu hicho kipo na watu baadhi ya wakati wanafaidika wakati wa Kaskazi, lakini kibanda hicho hicho ikifika siku za mvua waliomo ndani wanaroa. Kwa hivyo nilitaka nimwambie Mhe. Waziri aliangalie sana hilo suala kwamba marekebisho yafanywe kwenye kile kibanda,

ili watu wasiroe siku za mvua. Lakini vile vile kwa upande wa pili ambao unafika meli kubwa kubwa hivi vibanda vya kupumzikia hapana na humu katika bajeti haikuainishwa kwamba kutajengwa, kwa hivyo hilo nalizungumza kwake kwamba alielewe huku kunahitaji marekebisho na kule kunahitaji kujengwa jengo jipya.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza sasa hivi ni suala zima la zao la karafuu, mimi katika zao la karafuu na shughuli zake zote zilizomo nitaweza kuizungumzia kwa mipango hii ifuatayo, kwanza nataka nizungumze sababu za kuanguka zao la karafuu, halafu kuna bei ambazo zinatolewa na ZSTC ambazo zinaleta hitilafu, halafu katika suala hili hili kuna suala la mchango wa serikali milioni sitini. Katika suala hili hili, kuna suala la kubinafsishwa kwa zao la karafuu, sasa mimi nafikiri katika suala zima la zao la karafuu kwa nini likawa hapo awali likaanzia 24 elfu tani kwa miaka ya nyuma iliyopita, lakini kwa sasa likaambiwa linatoa 3000 mpaka 2000 tani.

Mhe. Spika, tunasema kwamba zao hili limeelezewa kwamba awali yake tulikuwa tunapata tani nyingi sana za karafuu ambazo zilikuwa hazipungui 24 elfu zikaanguka kidogo kidogo mpaka kufikia elfu tatu mpaka elfu mbili ambayo ndio mavuno yetu, sasa mimi nataka niseme tu kwa miaka iliyopita zao hili lilikuwa limenawiri vizuri na pato la taifa lilikuwa ni kubwa sana. Niseme tu kwenye suala hili la zao la karafuu kama tutakumbuka miaka ya nyuma ni kwamba Pemba ilikuwa inatoa zao hili katika kila shilingi mia, basi senti thamanini zilikuwa zinatoka katika zao la karafuu na hili ndilo lilikuwa likisaidia uchumi wa Zanzibar tusisahau hilo. Lakini, ilikuwa hali ni nzuri na mikarafuu ilikuwa inanawiri na kustawi vizuri na watu walikuwa na furaha kubwa na mapato yalikuwa mazuri na serikali ilikuwa inapata mazao mazuri sana katika karafuu, watu walikuwa wanakula vizuri wanavaa vizuri na walikuwa wanajenga sana kipindi hicho na walikuwa na akiba ya karafuu wakati huo kiasi gunia hamsini mpaka sitini ndani, walikuwa wanaweka kwa ajili ya akiba yao kwa kuuza na kupata fedha za kutumia.

Walikuwa na uwezo vile vile wa kusafisha mikarafuu yao kwa kuilimia kwa miaka hiyo ndio maana ukakuta wakati huo zao la karafuu lilikuwa kubwa sana kwa sababu ya kuenziwa vizuri, lakini baada ya usimamizi mbaya pande zote mbili kwa wenye mali na kwa upande wa serikali usimamizi haukuwepo wa kutosha, nini matokeo ya usimamizi kuwa mbaya kwa pande zote mbili kwa mwenye mali na serikali ni kwamba watu walikuwa wanafanya wanavyotaka. Mkarafuu ulikuwa unavunjwa ukikatwa kwa mapanga, ukikatwa kama ni nishati ya kuweza kupikia majumbani matokeo yake ndio hayo ya kuona kwamba kutokana na tani ishirini na nne elfu tumeangukia tani elfu tatu au tani elfu mbili kwa mwaka, sasa hizo ndio sababu kwa nini zikaanguka namna hiyo.

Mhe. Spika, hali hii inaendela kuwa mbaya siku hadi siku, mpaka hivi sasa mikarafuu iliyopo imekuwa ni mvi tupu kwa sababu iko taabani, sasa hapa bado tunasema kwamba usimamizi ni mbaya na hili zao la karafuu kwa Pemba limepuuzwa na halikushughulikiwa inavyopaswa.

Vilevile wakati huo huo tunasema watu wanachuma karafuu kulikuwa na watu wakiangusha kwenye bei, yaani wakulima mikarafuu iko tayari lazima wende watu wakakodi karafuu, lakini kwa bei ya awali ya *ZSTC* inayotoa kwa zao la karafuu huwa lina matumaini makubwa na wakati likitangazwa kwamba bei itakuwa kiasi kadhaa kwa kilo, basi na wale wenye mashamba ya mikarafuu hawana budi kupandisha bei ya ukodishaji. Lakini mara tu baada ya muda hiyo hiyo *ZSTC* huangusha bei ya kununulia matokeo yake wale wanaokodi mashamba hayo wanakula hasara kutokana na kuangushwa kwa bei na hasara ya pili ambayo wanaipata katika uchumaji wa karafuu mara nyingi karafuu ni kitu ambacho kina joto sana. Tunafahamu kwamba joto linapokuwa jingi husababisha mvua, mara nyingi katika uchumaji wa karafuu huweko na mvua nyingi sana. Kwa hivyo, wanapata vipigo viwili cha kwanza cha kuangushwa kwa bei na cha pili katika hali ya hewa ambapo mvua huwa nyingi sana na karafuu huoza.

Kwa hivyo, kipindi hiki ndicho kinachowafanya watu wakose mazao yakutosha. Mimi nasema hali hii tuione na tuielewe, kwamba hii hali imekuwa ngumu, mikarafuu mingi imeshakufa na hali ya ustawishaji wa mikarafuu bado hairidhishi yaani hiyo inayopandwa.

Mzungumzaji wa awali aliyezungumza kwamba si hoja kufanya nasari ya miche kwa kupeleka kwenye mashamba. Lakini pia inahitaji suala zima la ufuatiliaji, kama mikarafuu imewekwa 3,000 au 10,000 kwa kupelekwa mashamba, basi inahitaji mikarafuu hiyo yote iangaliwe je mingapi imeshika na mingapi imekufa pale ndio tutaweza kupata takwimu zilizokuwa sahihi. Lakini kwa kutoa takwimu tu kwamba katika nasari zetu tumekuwa na miche kadhaa na tumepeleka katika mashamba na yote pengine imepandwa, lakini tunajuaje kama imepandwa yote na iko hai? Inawezekana mingine imekufa. Kwa hivyo, hapo vile vile tunaona kuna kitu ambacho hakina ufuatiliaji kwa suala hili, watu wa nasari wakimaliza kazi zao za kusambaza miche kazi imemalizika ufuatiliaji baadae hakuna.

Mimi niseme tu kwa suala jengine kwamba mchango wa serikali wa 60 milioni kwa hali ya mikarafuu ilivyo hivi sasa pesa hizo *is nothing*, kutokana na mikarafuu tangu Kaskazini mpaka Kusini Pemba pamoja na Unguja yake kwa milioni 60 mikarafuu iliyopo 60 milioni hazitoshi hata kidogo, utaona kwamba bajeti hii hapa nafikiri waziri alifikirie sana suala hili kwa sababu mikarafuu

iko katika hali mbaya na ni moja katika uchumi wa nchi hii, hivyo tuna haki ya kulitetea hili suala ili tuhakikishe kwamba nao fedha zao zinaongezwa.

Suala jengine ambalo linazungumzwa katika zao la karafuu, ushauri mwingi unaotoka kwa wananchi wanasema ni vyema kama hili suala la zao la karafuu likabinafsishwa. Hili ndilo suala wanalotaka wananchi, kwamba bora tupewe wenyewe, tukipewa wenyewe tutafanya bidii zote, tutapanda wenyewe kwa hima, tutasafisha mikarafuu yetu, kila kitu tutakifanya, lakini tuuze wenyewe na tupate pesa nzuri, na mimi naamini kama wakipewa wenyewe wataweza kufanya vizuri, hebu tuwapeni tujaribu tuone, wakishindwa tutachukua, lakini hebu tuwape. Wanaweza wakahuisha mashamba yao vizuri na mazao yakapatikana mazuri na faida ikapatikana watu wakajenga wakavaa vizuri, wakala vizuri, na wakanunua wanayoyataka kama magari au kitu chochote.

Kwa hivyo, hilo suala mimi nasema shilingi 60 milioni ni kidogo sana, kama serikali ina wasi wasi katika suala la kubinafsisha haitobinafsisha tu, lakini serikali au *ZSTC* inaweza kutoa ushuru wake katika suala hili. Kwa sababu yale ni mazao ya ndani na mazao ya ndani unaweza ukachukua ushuru wake. Kwa hivyo, tuwape nafasi hii watu waendelee katika suala hili.

Mhe. Spika, suala langu jengine ambalo nataka kulizungumza ni suala la idadi ya watu. Idadi ya watu sasa hivi imeongezeka imekua kubwa, ukuaji umekuwa mkubwa, kwa sababu kuna ukuaji wa watu wanaozaliwa na kuna watu ambao wanaongezeka, sasa ni athari hii watu wakiwa wengi kiuchumi. Zanzibar ni kisiwa kidogo, sote tunahitaji ardhi katika kujenga, katika kulima, katika viwanja vya burudani, tunahitaji viwanja kwa ajili ya mahospitali na maskuli pamoja na viwanda. Vile vile tunahitaji maeneo kwa ajili ya mboga mboga, tusisahau kwamba ardhi yetu ni ndogo kwa sababu sehemu kubwa ni ya mawe, hivyo lazima hiyo tuitie katika tathmini.

Ardhi hii ni ndogo, kutokana na ardhi hii kuwa ndogo inaonesha sasa hivi hapa watu wengi sana katika nchi hii wameanza kuondoka, wengine wako Tanzania Bara takriban mikoa yote, wengine wako Burundi, Rwanda kila pahala watu wapo na wengine wako Afrika ya Kusini. Lakini kama tutawaia watu wote warudi makwao na kutokana na hali ilivyo nafasi itakuwa ndogo na tutaanza kupigana vibao. Kwa hivyo, hilo lazima tuliangalie iwapo hao watu wetu watarudi makwao eneo hili litakuwa ni muhimu sana, itakuwa ni kizaazaa. Hili ni tatizo moja kubwa.

Mhe. Spika, tatizo la pili ni suala zima la uingiaji wa watu bila ya utaratibu mzuri. Huwezi ukajua watu wanavyoingia katika nchi hii nani ni mzuri, nani matata, nani mwizi na nani mhalifu, uhalifu au ubaya wake utajulikana baadae akishakuwa hapa ndani ya nchi kwa sababu tunawaona watu wanavunja

maduka na nini, watu wanaingia ndani ya nchi hii. Hii yote inasababishwa kwa sababu sote tumekuwa na vitambulisho vya aina moja kwa hivyo sasa humjui ni nani, kitambulisho changu na cha yule anayeingia na tunategemea kwamba watu wanaingia kutoka Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda hatuwezi tukajua kama hawa ni watu wa Tanzania. Kwa hivyo, mimi naona hili suala ni gumu na tunahitaji kuliangalia.

Mhe. Spika, sasa ongezeko lililokuwa halina mpango linaleta athari kubwa katika uchumi, chakula ambacho tunakipanga kwa ajili ya watu wetu kinakuwa kidogo hakitoshelezi. Sasa nimuulize Mhe. Waziri, je, hawa wanayo kasma yao? Kwa sababu sisi tunakwenda kwa mujibu wa idadi ya watu wetu je, hao watu wanaoingia kutoka sehemu mbali mbali kasma zao zipo? Kama tukiendelea hivi hivi tutapata wapi hayo maeneo ya kujenga na mambo mengine.

Mhe. Spika, hivi sasa Zanzibar tangu sensa ya mwaka 1988 na ile ya 2002 imetoa hesabu kamili kuonesha kilomita moja mraba ina watu 400 hivi sasa, angalieni kwa Zanzibar hii ndogo na eneo lilivyo. Ulinganisha na Bara katika kilomita moja basi utakuta wau 26 mpaka 38, lakini Bara ni kubwa hata sisi watu wa Unguja na Pemba tukiambiwa tuchukuliwe sote tuingie Bara hatuwezi tukaonekana.

Mhe. Spika, iwapo suala hili litaendelea watu kuingia kiholela fanya tathmini baada ya miaka kumi nini mtokeo yatakuwa katika nchi hii. Tujiandae kwa uzalishaji mkubwa ambao hii huduma za kijamii. Sasa Mhe. Spika, ikiwa watu wataachiliwa watu watakosa ardhi, mahitaji ya kijamii yatakosekana, tutahitaji kupambana hivyo hivyo katika sehemu ya afya na mambo mengine.

Mhe. Spika, nashukuru sana ahsante.

Mhe. Ali Haji Ali: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipatia nafasi nami nipate kuzungumza machache mbele ya hotuba ya Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi.

Pili kama walivyoanza wenzangu namtakia kila la heri Mhe. Asha Moh'd Hilal ambaye amechaguliwa kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magogoni. Kadhalika kama walivyosema wenzangu kwa kuwatakia malazi mema Mhe. Soud Yussuf Mgeni na Daud Hassan Daud Mwenyezi Mungu awajalie walale mahala pema peponi amin.

Naomba nimshukuru na nimpongeze Mhe. Waziri, Manaibu Makatibu Wakuu na Watumishi wote wa wizara hii ya fedha kwa kutafiti, kubuni na kuandaa

hotuba nzuri ambayo hatimaye tuna matumaini kwamba itatuletea maendeleo sisi wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa nianze kwa kusema jambo moja tu kwanza. Mhe. Spika, mimi baada ya kusikiliza tangu jana mjadala huu nimepata mambo mawili, la kwanza nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwa umahiri wao mkubwa na uwezo wa kufahamu kwamba wao ndio walioandaa dira ya maendeleo, dira ambayo ndiyo sukani ya kuhakikisha kwamba umasikini uliokithiri katika nchi yetu hii utaondolewa. Halikadhalika Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili ndio waliopitisha MKUZA nambari moja kwa maana ya Mpango wa Kupunguza Umasikini na Mkakati wa Kupunguza Umasikini katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kumbe sisi ni Wawakilishi mahiri, tunaelewa nchi hii kwa kweli baada ya miaka 20 iweje, kwanza iweje kisiasa, kiuchumi na kijamii. Sasa wapiga kura hiari yao, lakini nadhani ni wawakilishi wazuri wana haki ya kuturejesha. Kwani tunasemaje? Tunasema hivi, kwamba baada ya miaka 20 nchi hii kutakuwa hakuna mtu ambaye halali nyumba nzuri jambo baya jamani hilo? Nchi hii hakutakuwa na mtu ambaye hali chakula kizuri, nchi hii kutakuwa hakuna anayevaa mararu, wala mtu ambaye atakosa elimu na kukosa tiba. Hayo kwa umahiri wetu ndio tunayoyazungumza.

Mhe. Spika, si hivyo tu, ili kuona kwamba jambo hili linatekelezeka na kwa kuelewa kwamba uwezo wetu wa ndani mdogo tumepitisha sera 19 sera hizo kila moja zinatafsiri dira yetu ya maendeleo. Nilikuwa nawasikia wenzangu hapa wanazungumzia utalii sana, lakini tumeshapitisha sera ya utalii hapa hapa sisi wenyewe, ambayo ndani yake inaeleza namna gani utalii katika visiwa hivi utaendeshwa. Tumepitisha sera ya vitega uchumi kwa kuelewa kwamba hali yetu nyepesi tunataka wenzetu watusaidie basi mtu ukitaka akusaidie atakwambia basi nipe utaratibu wako wa kuendesha uchumi katika nchi yako basi utamwambia usiwe na wasi wasi sera ya vitega uchumi hii hapa.

Tuliyoyazunguza tangu jana mpaka leo humu yamo, lakini mimi nakubaliana na nyinyi kwamba liko tatizo la watendaji wetu, kwamba sisi tumepitisha dira, tumepitisha MKUZA nambari moja na mbili, tumepitisha sera zote hizi, lakini wanaziacha, wanapoandaa bajeti wanasahau kabisa kama vitu hivi vipo. Kwa hivyo, tuna ugomvi sisi na watendaji wao ndipo tatizo lilipo hapo.

Kwa mfano, leo hii katika nchi yetu tuna deni la karibu asilimia 33 ya mapato ya taifa letu, lakini tumesema kwenye sera kwamba sisi kulingana na hali yetu basi badala ya kuchukua mikopo basi twende zaidi kwenye hisa. Hilo halifanyiki, tumepitisha sheria hapa au sera ya *BOT*, lakini matokeo yake ni vitu ambavyo vinaachwa.

Mhe. Spika, kwa hili mimi nataka kusema hivi, kwamba kama tulivyo sisi wana siasa tuna miaka mitano kwa nini kazi ya Ukurugenzi, Manaibu Katibu Wakuu na Makatibu Wakuu na wao hawawi na kiwango wakawa katika kipindi cha miaka mitano, wanatakiwa watekeleze haya na haya kama hawaja-*deliver the good*, basi waende. Kwa sababu inaonekana ndio tatizo, hatuna tatizo la sera ukiisoma ile dira nzuri tu haina matatizo yoyote, ukizizungumza na hizi sera nyengine zote ambazo tumezipitisha nzuri.

Mhe. Spika, kwa idhini yako mimi nataka nitaje kwamba kuna Sera ya Wanawake na Watoto, Sera ya Vitega Uchumi, Sera ya Taifa ya Utalii Zanzibar, Sera ya Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu, Sera ya Taifa ya Maji, Sera ya Maendeleo ya Vijana, Sera ya Utamaduni, Sera ya Elimu ya Amali na Mafunzo, Sera ya Vyombo vya Habari, Sera ya Taifa ya Biashara, Sera ya Maendeleo ya Viwanda, Biashara Ndogo ndogo na Kati, Sera ya Taifa ya Ukimwi, Sera ya Michezo, Sera ya Nyumba, Sera ya Uhakika wa Chakula, Sera ya Ajira, Sera ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali. Zote hizi kwa pamoja Mhe. Spika, ndivyo vielelezo vya kuhakikisha kwamba ile zana ya dira ya kuhakikisha kwamba tunaondokana na umasikini uliokithiri hizi ndio nyezo zake. Sasa watendaji kama wanapoandaa bajeti wanadhani pengine labda miongoni mwa hizi sera tulizozipitisha kuna maeneo ambayo yana udhaifu walikuwa watuletee watwambie.

Mhe. Spika, kama wenyewe tutakuwa tumejisikiliza vizuri yote ambayo tumeyazungumza kwenye biashara kumbe tumeshayasema tena tumeshayatungia sera. Ukizungumza Utawala Bora ambao watu wengi wamezungumza hapa kwamba iwe ni nchi ambayo watu wanapendana, iwe ya kidemokrasia zaidi na uwepo uimara katika suala zima la Vyama vya Siasa imetajwa katika sera, lakini hawa wenzetu ndio hawatekelezi, si jambo jipya. Kwa hivyo, hapa tunajikaza tunasema kama jambo jipya sio, si jipya tatizo ni utekelezaji. Hilo Mhe. Spika, nilitaka niliseme la kwanza.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda umekuwa mdogo niende kwenye jambo jengine, niende kwenye *financial bill*. Kwa kawaida hadi kufikia tarehe 30 Juni ndio mwisho wa mwaka katika taifa letu katika maana ya *finance*, lakini baadae hapo kwa sababu kuna kodi mbali mbali zinabadilishwa, lakini *finance bill* mnaipitisha mwisho, mimi nataka kuuliza uhalali wa kukusanya kodi unapatikana wapi? Ndio hoja yangu hiyo, kwamba *finance bill* mnaipitisha mwisho na ndio inayotoa idhini ya mabadiliko ya kodi hivi nyinyi mkifanya hivyo hiyo *right* mnaipata wapi serikali? Mtwambie. *Appropriate bill* sina matatizo nayo maana ndio inayosema kwamba katika mjadala wote wa bajeti nzima sekta hii ya elimu na nyengine zote mlifikia hapa je, Waheshimiwa mnakubaliana ndivyo mlivyopitisha? Ndio maana ya ile, lakini *finance* ndio inayoruhusu hizo kodi, lakini inapitishwa mwisho kwa nini?

Mhe. Spika, jengine nataka nizungumze kuhusu elimu. Mhe. Spika, hapa nataka kuzungumza Lugha ya Kiswahili, Lugha ya Kiswahili inavyosemekana pengine huenda ikawa ndio lugha ya Bara la Afrika, kwa maana hiyo itakuwa ni ajira kubwa kwa hasa sisi ambao Kiswahili ndio chimbuko letu. Lakini naona kunako hotuba hii sikulisikia kuzungumzwa jambo hili hata kidogo. Hilo moja.

Jengine ni kwamba wakati mwingi sana kama utasikia hotuba zetu kunako suala zima la elimu linazungumzia *illiteracy* hatuzungumzii *ignorance* kwamba elimu yetu tunayotoa kuanzia darasa la kwanza mpaka Chuo Kikuu haitoi majibu kwa matatizo yetu. Hili silisemi mimi Mhe. Spika, ndivyo sera inavyosema, kwa sababu ya mitaala yetu, kwa sababu ya sera zetu elimu tunayoitoa haijibu matatizo yetu. Lakini ilielezwa mle kwamba itaundwa taasisi ambayo itasimamia masuala mazima ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na mitaala, mihtasari na sera ambazo zitatoa elimu ambayo itakuwa na majibu, sikulisikia hili.

Mhe. Spika, najitahidi kuchagua moja moja. Nije kwenye vyombo vya fedha, imesemwa sana kwenye mikakati hata na dira pia imesema kwamba vyombo hivi vitatumiwa kuhakikisha kwamba wakulima na wavuvi wanapata mikopo. Mimi najiuliza watapataje kama katika nchi yetu mpaka leo ardhi haijakuwa ni kitu ambacho kinaweza kikakubaliwa na benki mtu akapata mkopo. Hakukusemwa chochote kwamba hii dhamana ya hawa wavuvi wataipata wapi wakati ardhi yenyewe haijahesabika hivyo.

Mhe. Spika, baya zaidi kuliko hilo ni kwamba ardhi yenyewe hivi sasa kuna wajanja wanaoipata na wengine hawaipati. Labda nimnukuu Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi alipokuwa akitoa hoja yake ya mafuta alisema hivi, “Mafuta ni yetu na tutahakikisha lazima tupigane, lakini yawe yetu”. Mimi nakubaliana naye, lakini akasema jengine zuri tu kwamba, “Rasilimali hii ya mafuta ina ugomvi”. Nigeria wanayo, Angola wanayo, lakini inatumiwa na kikundi cha watu wachache kwa hivyo, haileti maendeleo. Sasa na sisi ardhi tunayo tujitahidi tuhakikishe kwamba isije ikatumiwa na kikundi cha watu wachache tutapata matatizo ambayo wenzetu wa Nigeria na Angola wanayo kwa mafuta.

Hivi sasa Kaskazini Unguja tunalo tatizo hilo, namshukuru Mhe. Ame Ussi Juma amelizungumza vizuri zaidi ambapo mimi uwezo wa kuzungumza zaidi ya yeye sina. Mhe. Ame nadhani yeye kalizungumza vizuri kwamba rasilimali hii tusipokuwa imara na wakweli kunako jambo hili tutapata matatizo yaliyokuwa hayana maana yoyote.

Jengine ambalo nataka kuzungumza ni msamaha wa kodi. Mhe. Spika, msamaha wa kodi unasemekana uko karibu asilimia 21 kama takwimu nilizokuwanazo mimi ni sahihi kwa mapato ya taifa letu. Hiki ni kiwango kikubwa ingawa kipo kwa mujibu wa sheria, lakini kinatumiwa vibaya kwa mawazo yangu, kwa sababu wanapewa wenye mahoteli wakanunue gilasi, shuka, vitu hivyo viko hapa hapa. Kwa hivyo, ninachokusudia kusema huu msamaha wa kodi ili tusiwe tegemezi mpaka tunakuwa tunanuka basi hebu suala hili na tulitizame kwani kuna lazima ya kufanya hivyo.

Jengine *procurement*, kwenye ilani ya uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi kuna suala la uwazi na uwajibikaji. Moja katika vyombo vinavyo hakikisha kwamba suala hili limetekelezwa ni Afisi ya Mdhibiti Mkuu na suala zima la *procurement* ambapo kama tunakumbuka tulipitisha sheria wenyewe hapa, lakini elimu ya *procurement* ni ndogo na ndio kwanza inaaza. Ningetarajia Mhe. Waziri wa Fedha jambo hili angalau awe analitaja, ununuzi wa umma tulipitisha hapa hapa, lakini ubaya wake ni kwamba msipokuwa na utaratibu mzuri, mkawa na idara nzuri katika kila wizara jambo hili watu watafanya wanavyotaka, watanunua vitu walivyokuwa wanavitaka wao vilivyokuwa havimo katika mpango mtakuwa mmebakia *purpose*.

Mhe. Spika, kwa mfano nyuma tunakotokea serikali za wakoloni ingawa mbaya lakini walikuwa na sera ya manunuzi. Kwa hivyo, ukija hapa unajua kwamba ukiiona gari tu unajua kwamba gari ile ya serikali, lakini sisi hatuna hata hiyo sera ya manunuzi, lakini sheria tunayo.

Juzi hapa tulinung'unika kwamba serikali imenunua magari wee, wasinunue kwa nini na sisi tumeacha wazi, watafanya tu kwa sababu hakuna kitu kinachowafunga wasifanye hivyo. Sera ya manunuzi haipo, lakini *procurement* kama sheria ipo.

Mhe. Spika, jengine *decentralization* nizungumze kwa kifupi kwa mambo yote matatu, *quality delegation* kwa maana ile kwamba serikali ina *delegate powers* kwa watu kujenga skuli, vituo vya afya, inakwenda vizuri, lakini skuli zilizo nyingi wanafanya biashara zaidi, spitali zilizo nyingi wanafanya biashara zaidi kwa sababu hawasimamiwi wanaachiwa. Mimi ombi langu katika hili, kwa sababu sera ndivyo inavyosema, dira, mkakati ndivyo zinavyosema kwamba mkakati na sekta binafsi zitashirikishwa katika kujenga uchumi imara mimi hilo sina matatizo nalo, lakini basi wasiachiwe holela kama walivyo sasa.

Madaraka Mikoani tumeambiwa kwamba inaandaliwa sera, lakini mimi nimeshasema siku nyingi kwamba huko mikoani serikali nayo angalau ingepunguza ule mzigo wake ikapeleka mikoani na wilayani. Leo unaweza ukamkuta Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali tu ana Afisa wa Elimu wake

pale anashirikiana na Mkuu wa Mkoa, lakini mawaziri wengine hawana habari kabisa, sasa mnawashirikishaje sasa watu hao? Sisi tumesema kwamba nguvu zetu lazima tushirikishe kila mtu, serikali itwambie hivi hii sera itakuja lini?

Mhe. Spika, la mwisho kabisa mawili nitayazungumza kwa pamoja na mengine kutokana na muda nitayaacha. Mhe. Spika, nije katika suala la utandawazi. Wenzangu wamelisema kwa lugha nyengine kwamba tumo katika hali ngumu hivi sasa kwamba uchumi una matatizo na wenzetu walikuwa watwambie kwamba katika hali hii tume *survive* vipi? Kwa sababu utandawazi *concept* yake ni ukoloni mamboleo ni Kaskazini wenye nguvu za teknolojia na mitaji wanawanyonya wanyonge wa Kusini kwa kutumia hiyo teknolojia yao na mitaji yao. Je, sisi katika hali hiyo tunafanya nini? Kwa sababu lile la kwenda kuomba sawa basi hata hili.

Mwisho kuhusu ushirika. Mhe. Spika, katika nchi zilizoendelea Uingereza, Marekani na wengine wengi sana wameendelea kwa sababu wana shirika zilizokuwa imara ambazo nyingi zao za uzalishaji si za kutoa huduma.

Mhe. Spika, mwisho kabisa mimi nataka nitoe wito kwamba nchi yetu itangaze vita vya uchumi. Kuanzia sasa tuhakikishe kwamba vikosi vyetu vinakuwa ndio vyanzo vya kuhakikisha kwamba tunakuwa na mapinduzi ya kilimo na mapinduzi ya kiuchumi. Maana Wakorea ndivyo walivyofanya, Wavietnam ndivyo walivyofanya wakafika ile hatua waliyofika, badala ya kuwa na vikosi ambavyo havifanyi kazi yoyote ndivyo tunavizungumzia tu hapa. Hii ndio kazi ambayo wapewe.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, mimi na wananchi wa Mkwajuni tunaunga mkono hotuba hii.

Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutufikisha katika kipindi hiki cha bajeti, kwani wenzetu wengi nao walikuwa wanatarajia tuwe nao lakini kutokana na mipango ya Mwenyezi Mungu amewachukua. Kwa hivyo, tunawaombea Mwenyezi Mungu awajaalie katika maisha ya *barzakhi* na ya salama. Amin.

Mhe. Spika, mimi nitakuwa na maeneo matatu tu kwa sababu bajeti tangu jana imeshachangiwa sana. Mhe. Spika, nianze katika hivi vitambulisho ID. Mhe. Spika, masheha wetu wamepata mafunzo, naweza kusema wana elimu waliyonayo katika vichwa vyao kwamba vitambulisho hivi hawavitoi kwa wananchi ni kufanyiwa mkakati maalum. Lakini kutokana na hali ya mgando wa mawazo moja kwa moja akenda mtu anaambiwa kwamba kitambulisho kile cha kura. Mimi nina ushahidi wa mwanangu mwenyewe alikwenda pale kwa

sheha siku ya mwanzo alipofika alimwambia wewe hujatimia umri lete cheti chako cha kuzaliwa. Kapeleka cheti kaona katimia umri, siku ya pili anamwambia unataka kitambulisho ili uje kupiga kura, mimi siji kukupa idhini ya kupiga kura kabisa hata nikakupa hicho kitambulisho.

Lakini Mhe. Spika, tujue kwamba vitambulisho hivi vinatumika kwa njia nyingi. Mhe. Spika, mimi nawe tulikuwepo Nairobi basi nilitia kadi simu yangu ya safaricom, baada ya kurejea hapa kutoa line ile kutia line yangu ya Zantel ikakataa kufanya kazi nikabaki sina line. Sasa naitaka line yangu niipate ile ile kwa hiyo niende Zantel. Kwa bahati nzuri kufika Zantel wakanambia lete kitambulisho chako cha Uzanzibari. Tuone kwamba jinsi tutakavyomnyima mwananchi hiki kitambulisho na tutakapomkosesha mambo chungu nzima.

Mhe. Spika, kwa bahati mimi nikarudi. Siku ya tarehe 15 mwezi huu nikatoka nikenda tena Zantel na kitambulisho changu cha Uzanzibari, nilipofika bila ya tabu nikatolewa photocopy nikapewa line nyengine. Lakini katika mkururo ule niliouona waliokuja pale ni watu wengi baadhi wanarejeshwa rudi kalete kitambulisho na namba za watu watano uliokuwa ukiwapigia. Kwa hivyo, hii ni hali ambayo inaonesha kwamba kitambulisho ambacho atanyimwa huyu mwananchi atakosa mambo mengi.

Mhe. Spika, si hayo tu, kuna mtoto mmoja anatoka Uzi alitaka leseni hana kitambulisho cha Uzanzibari akaambiwa katafute. Mhe. Spika, kama tunafanya mikakati wananchi wasipate hivi vitambulisho kwa kweli tutawakosesha wananchi haki chungu nzima. Tunajua kwamba popote unapokwenda sasa hivi upeleke kitambulisho cha Uzanzibari. Hili ni suala ambalo mimi ningeliomba serikali ikae kitako upya ijipange. Kuna wananchi ambao hawana vitambulisho, kuna watoto ambao ndio kwanza wanatimiza sasa hivi miaka 18 na wao tayari wameshafikia hatua ya kupewa hivi vitambulisho basi wapatiwe kabla halijazuka tatizo jengine lolote katika nchi yetu.

Mhe. Spika, la pili nije katika suala la utafiti. Mhe. Spika, Mhe. Mohamed Ali Salim alisema kwamba utafiti unafanywa katika meza na mimi nakubaliana nae. Tarehe 14 mwezi huu nilifika katika kijiji cha Uzi, siku zote tunajua kwamba Uzi ni sehemu inayozalisha muhogo kwa wingi. Ukenda sokoni ukiuliza muhogo aidha muhogo wa Pemba au muhogo wa Uzi ndio unaoulizwa sana pale. Hauna tofauti katika sehemu zao wanapotoa mihogo yao. Lakini hivi sasa wamekumbwa na janga la kuharibikiwa na mazao haya ya muhogo. Kelele zilizokuwepo pale siku ile wanasema mheshimiwa tuna tatizo la kuharibikiwa muhogo wetu hatuna hata la kufanya. Humkuti mkulima hata mmoja safari hii aliyevuna muhogo na hawa mabwana shamba hawajatupitia kwa lolote. Tunakuomba hebu katuulizie huko angalau tuje kufanyiwa huu utafiti tujue kitu gani kinachosababisha hali hii.

Mhe. Spika, Mhe. Mohamed Ali Salim aliuliza hapa ni vijiji gani vilivyofanywa huu utafiti. Kwa kweli bado kuna vijiji haujafika huu utafiti na suala hili lipo mimi nahisi sio Uzi peke yake. Wakulima wa Uzi wanategemea sana kilimo cha muhogo lakini wapo taabani kwa hali hii iliyowafika. Akenda mgeni akifika tu basi anang'olewa muhogo shina moja polo zima. Kwa hivyo, wananchi wa Uzi wana masikitiko makubwa kwa hali hiyo. Ningeliomba huu utafiti wafikishiwe waone ni kitu gani kilichosababisha hali hiyo.

Mhe. Spika, nikiendelea na kilimo kama walivyosema wenzangu wananchi waliitikia sana kulima mwaka huu, hususan Cheju wamelima sana mpunga. Lakini tatizo kubwa linalowakumba utakuta safari hii dawa ilitolewa kidogo. Kwa hivyo, waliokwenda mwanzo waliwahi dawa, waliokuwa hawakuwahi tayari sasa wajanja wakajitokeza hapo. Ilichukuliwa dawa kutoka Bara wakaja wakauziwa wananchi. Waliinunua dawa ile na kuipiga katika mipunga lakini mpunga ule uliteketea. Kwa kweli utafiti uliofanywa inasemekana kwamba dawa hii ni ile ambayo iliyokuwa ikipigwa katika mikorosho. Sasa dawa ambayo inapigwa katika miti mikubwa haibakishi kitu, kwa hiyo wakulima waliobahatika kupiga dawa hii hawakubakia na kitu. Ipo haja wakulima wetu kufuatiliwa ili wasivunjike moyo.

Mhe. Spika, kelele zinapigwa wananchi limeni njaa, njaa, wameitikia wito vizuri na aliyelima mwaka huu amefaidika vizuri. Mhe. Spika, ipo haja hii hali kutengenezewa bajeti hasa katika kilimo.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Ame Mati Wadi alisema kwamba anaona uchungu kudharauliwa kauli ya Rais. Kwa hivyo, ipo haja ya kutaka kujua kwa sababu tangu juzi wananchi waliposikia kwamba kunasomwa bajeti kauli ya Rais ni kauli kubwa anapoitoa popote, ni kauli ya kuheshimiwa. Wananchi wananitumia sana *message* kutaka kujua kwamba siku ya ufunguzi wa Skuli ya Maandalizi Ndijani kauli aliyoitoa Mhe. Rais, alisema mwaka huu nitahakikisha barabara ya Ndijani itatiwa katika bajeti japo kwa kutiwa kifusi kwa awamu ya mwanzo. Awamu ya pili nitahakikisha itatiwa lami.

Sasa walitaka kujua je, hii barabara imo katika bajeti? Lakini baada ya kuangalia mimi sikuiona. Mhe. Spika, wananchi wanataka kujua ile kauli iliyotolewa pale ni kama mchezo wa kuigiza au ni kauli ya Rais imechukuliwa uzito na kuchukuliwa uzani kwamba kauli hii itafanyiwa kazi. Mhe. Spika, suala hili nilitamani kwamba nije nilizungumze katika wizara husika, lakini wakati hii ndio bajeti kuu ya serikali niliona niulizie hapa ili wananchi waliotaka kujua hali hii wasikie kwamba suala la barabara yao na kauli iliyotolewa na Mhe. Rais imo kwenye bajeti, mimi nasema haimo. Mhe. Spika,

namuachia Mhe. Waziri hili suala aje anieleze hii kauli ya Rais ilichukuliwa kwa mzaha au vipi.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru ahsante.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, kwanza na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ili nitoe mchango wangu kidogo katika kuchangia bajeti hii ya serikali.

Mhe. Spika, kwa miaka ya karibuni Afrika ilikuwa inaanza kufanikiwa kutokana na marekebisho ya uchumi na matokeo ya mafanikio hayo yamejionesha katika kushusha mfumko wa bei kutoka asilimia 22 hadi *digit* moja. Lakini ukweli usiopingika kama hotuba ambayo imetueleza kwamba kishindo kilichotokea katika sekta ya fedha Marekani na baadae kusambaa Ulaya na hatimae kurusha cheche pamoja kuuporomoa uchumi athari zake tumeziona. Mhe. Spika, sababu nyingi zimetolewa sina haja ya kuzitaja.

Lakini niseme tu katika hatua za awali za mporomoko wa masoko ya fedha, sisi katika Afrika tulibahatika kutokupata athari za awali kwa sababu uchumi wetu haukuungana moja kwa moja kifedha na masoko yale ya dunia. Kwa sababu matatizo ya kifedha baadae yalijitokeza katika uchumi na kwa kuwa tunategemea uchumi wa dunia katika kuimarisha uchumi wetu kwa hivyo moja kwa moja na sisi sasa hivi tumeathirika. Sasa jukumu letu sisi kama Afrika na kama Tanzania na Zanzibar ni kuchanganua tumeathirika katika maeneo gani na baadae tunachukua hatua zipi kurekebisha uchumi wetu.

Mhe. Spika, nilisikia hapa ikitajwa *stimulus package* na najua hii imefanywa kwa sababu ni hatua ambayo imechukuliwa katika bajeti ya Tanzania Bara. Wengi walifikiria kwamba tungekuwa na *stimulus package* na hasa kwa sababu wengi wanafikiria kwamba tungeelekea katika kilimo. Mimi sidharau mawazo hayo lakini kama nilivyosema ingekuwa ni hatua nzuri sana ya kuchanganua namna ambavyo tumeathirika.

Mhe. Spika, Tanzania Bara katika suala la kilimo inawezekana wanahitaji *stimulus package* kwa sababu mazingira ya kilimo ya kule na ya Zanzibar yanatofautiana kwa maoni yangu. Asilimia 65 ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi Tanzania Bara wamekuwa *engaged* katika kilimo. Matumizi ya pembejeo, zana za kileo, mbolea, pamoja na usambazaji wa mbegu zenye tija uko katika kiwango cha juu zaidi kwa Tanzania Bara. Kwa Zanzibar kwa takwimu za serikali ni asilimia 28 ya watu. Bado kilimo chetu kina watu wachache sana, kina zana duni, matumizi ya mbolea hamna, matumizi ya teknolojia ya leo hamna.

Kwa hivyo, mimi nakubaliana na mawazo ya kwamba kilimo ndio cha kukielekea sasa hivi. Naogopa kusema, lakini ningesema siasa ni kilimo. Kama siasa si kilimo basi angalau uchumi sasa ni kilimo. Kama tunazungumzia uchumi maana yake bajeti ni kilimo.

Mhe. Spika, kwa Zanzibar nakumbuka tunayo sera ya kilimo ambayo mwaka 2002 tuliletewa hapa. Mwaka 2004 kukawa na mpango wa mkakati wa utekelezaji. Kwetu sisi Mhe. Spika, nilidhani na hiyo itakuwa ni kazi ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira atakapokuja na bajeti yake atueleze kwanza tumefikia wapi katika utekelezaji wa mpango wa mkakati wa kilimo kwa Zanzibar. Pengine tusingezungumzia *stimulus package* lakini tungezungumzia suala la ku-*reform* kilimo *completely*.

Mhe. Spika, nakubaliana na mawazo ya watu ya *alternative budget* ambayo kwangu mimi nairekebisha kidogo kwa sababu wapo wenzangu walitoa halafu wakarekebisha. Ningedhani ya kwamba asilimia 5 ya matumizi ya serikali katika kila sekta yangelikatwa yakaelekezwa katika kilimo na nitatoa sababu zangu.

Mhe. Spika, tumeona katika kilimo na Mhe. Waziri ametueleza hapa kwamba hatukufikia katika lile lengo la asilimia 6.8 ya bajeti iliyopangwa ya ukuaji wa uchumi kwa sababu ya matatizo ya kuteremka kwa mahitaji ya Ulaya. Akatwambia hapa kwamba kwa sababu sisi tunasafirisha Ulaya, hii ni sababu moja kubwa ya kushuka kwa *demand* kwa hivyo hatukufikia lengo hili. Kwa hivyo, mimi nilitaka Mhe. Waziri hapa aangalie vizuri zaidi.

Kwa sababu tunasafirisha karafuu zaidi na tunasafirisha mwani, haidhuru kuna *element* hii ya utalii nayo nitaizungumzia. Lakini ukiangalia mwaka 2004, ukaangalia na mwaka 2007 katika karafuu, mwaka 2008 umekuwa ni mzuri zaidi, ushahidi huu unaonekana katika kitabu hiki cha mapitio ukurasa wa 40. Labda niseme tu mwaka 2004 tulisafirisha tani 4,358 tukapata shilingi milioni 10.997. Nimejaribu kuangalia kwa tani moja tulichokuwa tukipata ni karibu milioni 2,523,405/=, nimefanya kwa mwaka 2007 ni karibu shilingi milioni 3 na nimefanya kwa mwaka 2008 nimeona ni karibu milioni 4.6.

Mhe. Spika, hali ya biashara ya karafuu zetu katika soko la Ulaya katika kipindi hiki ambacho uchumi haukufikia lengo lake mimi naiona ni nzuri zaidi. Lakini nimeangalia kwenye mwani nikaona kwamba tumetoka kwenye 216,000 kwa tani kwa mwaka 2004 na tumekuja mpaka 293,000 kwa tani ya mwani katika mwaka 2008. Kwa hivyo, bado hapa *export* haikuwa sababu ya kuporomoa uchumi wetu tusifikie lengo.

Mhe. Spika, ukija katika utalii Mhe. Waziri ametwambia hatukufikia lengo la wageni ambao wanakuja hapa kwa asilimia 10.3. Lakini lengo letu lilikuwa asilimia 6.8 katika ukuaji wa uchumi tukapata asilimia 5.4 na kwa hivyo hatukufikia lengo kwa asilimia 20.5. Kama asilimia 10.3 za utalii ndio zilizokuwa na taathira bado Mhe. Waziri tunamdai asilimia 10.2 angetueleza ni sababu zipi ambazo zimeuporomoa uchumi mpaka tusifikie lengo.

Kwa hivyo, mimi kimsingi nakubaliana ya kwamba taathira ya uchumi wa dunia kuporomoka kwake kunatuathiri. Lakini sio lazima kwamba wakati ule ule ambao uchumi umeporomoka na sisi tumepata taathira hiyo, lazima kutakuwa kuna matatizo mengine ambayo ni yetu sisi wenyewe na inabidi tuyazungumze kinaga ubaga kama kweli tunataka tuzungumzie uchumi wetu.

Mhe. Spika, hata ukiangalia sio hilo la *inflation, inflation rate* bado zimekuwa ni mbaya. Lakini ukurasa wa 10 unatuonesha namna gani ambavyo bei ya mafuta imeshuka kutoka dola 147 hadi dola 40. Sasa kama kushuka huko kwa asilimia kubwa kwa bei ya mafuta na mafuta ndio yenye *content* kubwa sana ya *inflation* ya nchi yetu, ungetarajia lazima inflation ingepata sura nyengine na sio hii mbaya ambayo sasa hivi tunayo.

Mhe. Spika, yapo mambo mengine ambayo yanasababisha *inflation*. Suala la kilimo limezungumzwa sana, lakini suala la kilimo katika bajeti hii lime-*improve* na tumetoka katika asilimia 35 mpaka tumefikia asilimia 40 nadhani ya kuchangia. Kama hivyo ndivyo katika mwaka huu basi kilimo nayo haikuwa *factor* ya kusababisha *inflation* yetu. Lakini *inflation* bado itasababishwa na masuala ya uchumi mkuu ambayo hatuyamiliki. Kwa maana ya uchumi mkuu ni zile sera za kifedha ambazo ni za Muungano lakini Zanzibar haina *control* juu ya sera hizo. Kwa hivyo Mhe. Spika, tutakapojadili masuala yetu ya kiuchumi hili tusilisahau na tuone kwamba bado Zanzibar inaathirika. Mhe. Spika, mimi si-*propose* kusema kwamba sera maana yake iondoshwe isiwepo, lakini ni kuona namna gani sera ya Muungano inavyotumikia uchumi wetu kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, nakubaliana sana na hatua za kukiimarisha kilimo. Sambamba na kuimarisha kilimo ni pamoja na kuimarisha sekta ya viwanda lakini iwe ni *Agro Based Industry.* Kwa sababu kilimo ambacho tutakitegemea sasa hivi si kilimo cha chakula peke yake, lakini itakuwa ni kilimo cha kupata bidhaa za kilimo ambazo tutasafirisha. Bahati mbaya imekuwa ni mazungumzo ya kila siku katika Baraza letu lakini hatuoni hatua ambayo serikali inaichukua. Nadhani jana nilimsikia mwenzangu mmoja akisema tunawasubiri wachumi watupangie watwambie tutakwamuka vipi. Kwa maoni yangu mimi nadhani tulipo si suala la wachumi na tutawaonea sana. Lakini ni masuala ya maamuzi

ya kisiasa ambayo hayamilikiwi na mtu mwengine isipokuwa ni wananchi na sisi ndio wawakilishi wao.

Mhe. Spika, kwa mfano tumelizugumzia suala la mafuta la *resources* hapa na tulizungumza kauli kwa mujibu wa kuwawakilisha watu na wachumi walikuwepo wanatusikiliza wanasubiri nini tuwaeleze. Kama tutashindwa kuiunda kampuni ya kushughulikia *resources* zetu za mafuta hapa mchumi atafanya nini, hana cha kutueleza. Kwa hivyo, maamuzi mengi hapa yanatutegemea sisi.

Lakini sambamba na kuimarisha kilimo pamoja na viwanda vitakavyotumia rasilimali ya kilimo, bado katika hali ya sasa ya kiuchumi ni lazima tuimarishe masoko yetu ya ndani. Masoko ya ndani ni pamoja na kuimarisha sekta binafsi. Lakini juhudi za serikali za kuimarisha sekta binafsi bado hazijawa kubwa, ijapokuwa serikali inajitahidi katika kukaa na sekta binafsi pamoja na kupanga mambo chungu nzima.

Kwa mfano, kuna nyenzo muhimu sana ya kuihamasisha sekta binafsi iweze kushiriki katika uchumi, hii ni pamoja na kuipatia *incentive* ya mikopo ya kibenki. Tunapoisikia taarifa ya bajeti inasema kwamba *Commercial Bank* sasa hivi zinawakopesha *private sector* mimi sikubaliani nalo. Nataka niseme *honestly* kwamba inayokopa ni serikali, lakini serikali ilikuwa zamani inakopa moja kwa moja. Ikikopa moja kwa moja kutoka *Commercial Bank* maana yake sasa itumie njia za kurejesha na kwa hivyo hiyo ingeweza kuongeza *inflation*.

Kwa hivyo, serikali sasa wanakopa wafanyakazi mdhamini ni serikali, *resource* ile inayopelekwa benki inapelekwa kule kule serikalini haitoki pahala pengine. Kama ingelikuwa ni uzalishaji umekopa benki, halafu ni uzalishaji ndio uliosababisha sasa unailipa benki, mimi ningekubali moja kwa moja kwamba hii ilikuwa ni *private sector* tena kwa matumizi ya *private sector*. Lakini ni kusema kwamba bado *Commercial Banks* hazijafanya kazi inayostahiki katika uchumi kuikopesha sekta binafsi ili iweze kushiriki.

Mhe. Spika, nasema hili ni hatari sana katika uchumi kwa sababu tumetangaza wenyewe kwamba sekta binafsi ndio *engine of growth.* Lakini sekta binafsi hii ambayo imedumaa kwetu sisi na hatujakuwa na ile inertial ya kuifanya iondoke hapa ilipo, haiwezi ku-*compete* na sekta binafsi zilizoko katika nchi nyengine. Sisi tukitaka tusitake chumi zinazidi kushirikiana. Tulikuwa na Afrika Mashariki nchi 3 leo tuna nchi 5. Sasa hatuwezi kurudi nyuma lakini ni kuingia katika *speed* na sisi tukaweza kuwa *competitive* kuliko watu wengine. Tutafanya nini katika hayo ndio masuala ambayo yanahitaji maamuzi ya kisiasa.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu moja ya tatizo kubwa linaloukabili uchumi wetu ni ukosefu wa *resources*. Tunasema sisi hapa tunajadili bajeti vyanzo vya mapato, lakini vyanzo vya mapato hivi ambavyo tunavijadili na tunatafuta maeneo mengine ni sawa sawa na kusema ni ng'ombe aliyetoka kukamuliwa na kwa hivyo tunajadiliana namna ya kumkamua zaidi na mwisho atatoka damu. Kuna vyanzo vya mapato hapa ambavyo ni *none income revenue base* na hii ni ya Muungano na imekuwa ikizungumzwa sana. Hakuna sababu ni kwa nini unapopata huduma usilipe kodi pale. Lakini vyombo vya Muungano, *corporations* ambazo zinafanya kazi hapa, *parastatal* za Muungano, zinakwenda kulipa kodi pahala ambapo sipo wanapopata huduma.

Mhe. Spika, mimi nasema hili ni amuzi la kisiasa, ni lazima wanasiasa washirikiane na tutakapofika pahala mashirikiano hayapo lazima wakoromeane. Si lazima kugombana na kupigana lakini lazima kuoneshana misuli ya kuhakikisha kwamba nchi yetu haiendelei kukosa haki zake hata zile haki ambazo wazi wazi zinaonekana.

Mhe. Spika kuna eneo moja hilo la anga tulikuwa sisi mengi hatuyafaham, lakini ndege zinazopita huko zilikuwa zinalipa kila pahala, hatujapata kuambiwa hapa tunapata kiasi gani? Na kama kwenye Muungano wanaelezwa basi wabunge wanaokwenda kule watueleze tusipige kelele bure hapa kusema kule jamani iko keki yetu tunaipata, lakini hatuyasikii hapa hatuyasikii katika muungano.

Kwa hivyo, uchumi wa namna hii ambao sisi hapa tunakaa tunajikaza, tunatafuta vyanzo, tunamtafuta nani mchawi, lakini anaemiliki nguvu za kuendesha uchumi yuko mbali anatusikiliza na katulia ni kazi iliyo pevu sana katika kuufufua uchumi wa Zanzibar.
Kwa hivyo Mhe. Spika, hili ni jambo lazima linataka msukumo na mtazamo wa aina nyengine, ili kuhakikisha kwamba tunaliendesha vizuri.

Mhe. Spika, kwa sababu muda wako haupo, mimi niseme tu kabla ya kuunga mkono, suala la *infrastructure* Mhe. Mwenyekiti limezungumzwa humu na zamani kulikuwa na mpango wa kuijenga barabara ya Mashariki, mimi hii mpaka siku ambayo nitaondoka katika Baraza hili pengine 2010 au zaidi lazima niitaje.*(Makofi).*

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti ukitaka kuufuta umaskini, hatuwezi kuzidharau zile *infrastructure* moja kwa moja unaziona kwamba hizi ziko karibu na matatizo ya watu. Ukanda wa Mashariki umekuwa ukizungumzwa na wachumi hapa ni *phenomena* inayo- *recur* kila baada ya muda unasikia kuna *gross* iliyo kubwa. Watu wangelikuwa wapo karibu na mazingira ya biashara, mazingira ya barabara wangeimarisha biashara. Imetengenezwa barabara hapa

inaimarisha utalii, lakini mwahala mwengine utalii sio *imployment.* Data za Serikali zinaonesha kwamba Pemba watu wengi sana *imployment* yao iko katika kilimo na sehemu hiyo ya ukanda huo ndiko kunakotolewa zaidi kilimo. Watu wa huku Kaskazini tunawapelekea mihogo tu kina Maalim Mulla, lakini sana unatoka Chambani.

Sasa Mhe. Spika, lazima tuangalie tena nyuma *project* ya barabara ile tuelezwe na Serikali ilipotelea potelea wapi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, kabla ya kuunga mkono nipate hayo majibu halafu huenda nikaunga mkono. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na kabla sijaanza mchango wangu naomba nimuombe Mwenyezi Mungu awarehemu wenzetu waliotangulia mbele ya haki, awaondoshee adhabu zote za kaburi na awaweke mahali pema peponi.

Pia nitakuwa si mwingi wa shukurani kama sikumpongeza Mhe. Asha kwa ushindi alioupata kupitia kiti cha Magogoni. Mhe. Asha ametuonesha nyuso nzuri sisi wanawake na kwa kweli ni lazima tumpongeze.

Mhe. Spika, nataka nianze hotuba hii ya Waziri wa Fedha na Uchumi ambayo ameiwasilisha Dr. Mwinyihaji Makame, Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuhusu Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na matumizi kwa Serikali kwa mwaka huu 2009/2010.

Kwanza Mhe. Spika, hotuba hii kwanza ninaiunga mkono na ninaikubali. Ninaikubali ila tu nina mchango wangu mdogo. Nimeona ni vyema kabla Waziri hajaingia kupanga panga mapesa yake haidhuru ameshapanga, lakini na hili nitakalomwambia alitie katika fungu la huruma ili katika bajeti hii wananchi wa Chake Chake nao wapate kufaidika.

Mhe. Spika, nilifanya ziara katika eneo la visima kwa Sharif Ali Chake Chake, nakusudia kujadili kitabu hiki ukurasa wa 35 kifungu namba 66. Nilipofanya ziara katika eneo hili kwa kweli la kwanza nililojifunza ni kwamba eneo lile lina maji mengi. Na eneo lile tayari kwa Kiserikali limeshatengwa kwa ajili ya visima vitatu. Kuna kisima kimoja tayari ambacho sasa hivi kinafanya kazi, kuna kisima cha pili kimeshajengwa kabisa, *well-head* iko tayari, lakini bado hakijamalizika vizuri, lakini nacho tunasema kimo katika mkumbo wa kwamba kitafanya kazi, tena kazi nzuri.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri kuna na kisima cha tatu kimeshachimbwa na sasa hivi kinasafishwa na ujenzi wa *well-head* utafuatia baadae. Kwa hivyo,

tutakuwa na visima vyetu vitatu na visima hivi kila kisima kimoja kitakuwa na uwezo wa kutoa lita 60,000 kwa saa. Sasa hivi visima vinavyofanya kazi ni viwili vinatoa lita 120,000.

Mhe. Spika, bomba kubwa la nchi 8 tayari limeshajengewa kutoka kwa Sharif Ali hadi kwenye tangi la maji Machomane. Kama alivyotwambia Waziri kwamba kulikuwa na mabomba haya ya zamani ambayo yeshachoka, kwa hivyo Serikali imefanya jitihada ya kurekebisha kutoa mabomba yale kuweka mabomba mengine. Kwa hivyo tumebahatika vizuri kwa kweli tumepata bomba la nchi nane ambalo linakwenda moja kwa moja mpaka kwenye tangi la maji Machomane.

Sasa Mhe. Spika, changamoto sasa za Sharif Ali ili mambo yake yende vizuri, *transformer* pale tunayo inafanya kazi, lakini sasa uwezo wa kuendesha pampu zote tatu kwa pamoja kwa kweli haina kwa sababu uwezo wake ni mdogo. Nini sasa tunachokihitaji hapa ambacho tunaomba Mhe. Waziri atushughulikie, tunaomba tupatiwe *transformer* kubwa ambayo itaweza kufanya kazi ya kusukuma maji visima vyote vitatu kwa wakati mmoja na maji haya yatakwenda zake mpaka kwenye tangi kwa kadiri itakavyokuwa, tutategemea sisi tupate visima vitatu, lita 60,000 mara tatu kwa wakati mmoja maji yote yanapelekwa kwenye tangi la maji.

Kwa hivyo, tunategemea kwamba huduma ya maji katika mji mzima wa Chake Chake itakuwa ni nzuri zaidi. Kwa sababu hivi sasa kwa huduma ya maji kwa Pemba nzima tunashukuru alhamdu lillahi ipo. Lakini sasa Serikali yetu katika kuona kwamba hairidhiki tu na hali ilivyo katika jiji kubwa kama lile, ndivyo ilivyochukua jitihada ya kusema kwamba, lazima tuwe na maji mengi ya kutosha tuondoshe hii bughudha jamani, Serikali mbona sisi hatuna maji tutafanyaje, kazi yao kufanya hivi tu, lakini jitihada zetu tunaziona tunavyotaka kupunguza umaskini kwa kuwasaidia watu wapate maji ya uhakika.

Visima hivyo tunatarajia kwamba vitapunguza uhaba wa maji katika mji wote wa Chake Chake kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, bado tutakuwa tuna tatizo moja, bomba la kusambazia maji kutoka tangini hadi mjini Chake kwa kweli ni mabomba ambayo yamechoka sana Mhe. Spika, tunahitaji kupata mabomba mengine mapya ambayo mabomba hayo yataendana na mahitaji ya maji. Vyenginevyo tunaweza tukapata *transformer* kubwa maji yakawa yanasukumwa kwa nguvu kwenda katika tangi, lakini kutokana na hali ya mabomba yanayokwenda kwenye tangi tukashindwa kupeleka huduma yetu vizuri.

Kwa hivyo, kwa heshima na taadhima namuomba sana Waziri tena mimi na yeye damu damu, nadhani atawaonea huduma sana wananchi hawa wa Chake

Chake, tunataka hili tatizo la maji hasa liondoke kabisa kama itakavyofika mwisho wa mwaka huu tutakavyoondoa kabisa tatizo la umeme, basi na maji kwa mji wetu wa Chake Chake litaondoka kabisa. Hizi zote ni jitihada za Serikali yetu ya Mapinduzi awamu ya sita, mimi niseme tumeshavuka lengo katika mambo haya ya maji na tutavuka lengo katika mambo ya umeme. Kwa sababu tuna bahati sana sisi Wapemba kule baada ya kupata umeme ambao utatoka Tanga kwenda Pemba, lakini bado tutakuwa na mashine zile ambazo sasa hivi zinatengenezwa kwa bidii zote kwamba saa zote huku umeme tukiwa nao kutoka Tanga,lakini na sisi wenyewe tuweze kujitegemea kupitia kwenye majenereta yetu tuliyonayo. *(Makofi).* Serikali hii naona ishachaguliwa kabla hata hatujafika huo uchaguzi. *(Kicheko/Makofi)* kwa jitihada zake mbali mbali ishachaguliwa kabla hatujafika uchaguzi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa kweli sikutaka nikupotezee muda wako mwingi isipokuwa mimi namwomba sana Mhe. Waziri tena ninamwomba sana suala hili la jenereta, *transformer* alipe umuhimu wa kwanza tena mkubwa ili tuweze kuweka mambo yetu vizuri ikifika wakati tuchukuwe, tuweke waa. Ahsante Mhe. Spika.

(Saa 1.45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 24/06/2009 saa 3.00 asubuhi)